# Nipashe

Jumatatu Juni 3, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579934

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




**Serikali yatangaza kiwango kipya cha mifuko mbadala**

UKURASA 3







UKURASA 13

# Wakurugenzi wakimbiza vyama uchaguzi udiwani

**VYASEMA** ni kukaidi hukumu ya Mahakama kuwazuia...*Endelea ukurasa wa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**MAKONDA AMUENZI MENGI KUFUTURISHA WENYE ULEMAVU**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amewaomba watu wenye...

UKURASA WA 4

**MABASI 17 YAFUNGIWA KUCHEZEA VING'AMUZI**

ZAIDI ya mabasi 17 yamekamatwa na kufungiwa kwa mwezi mmoja kwa makosa ya...

UKURASA WA 4

**VITUO VYA AFYA 191 KUJENGWA NCHINI**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-Tamisemi), Selemani...





Baadhi ya wafanyabiashara ndogo waliokuwa wamehamishwa kando ya Barabara ya Ali Hassan Mwinyi eneo la Mwenge kupelekwa eneo la Cocacola jijini Dar es Salaam kupisha upanuzi wa barabara hiyo, wamekuwa wakirejea eneo hilo wakati wa jioni kuwavizia wateja kama walivyokutwa jana. Wanalalamika kuwa eneo walilohamishiwa halina miundombinu rafiki na hakuna wateja. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

## Waziri ataka kasi ulipaji mafao NSSF

UKURASA 3



UKURASA 2

## Hoja 6 mtihani kwa Waziri Mpango leo

**MICHEZO** **KAGERE ATOA MALENGO MAPYA SIMBA 2019/20** UK. 32

**MAONI, KATUNI UK.6**

# Majaliwa alishukuru kanisa ujenzi wa shule

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameushukuru uongozi wa Kanisa Katoliki Jimbo la Lindi kwa kutoa sehemu ya eneo lake na baadhi ya majengo kwa ajili ya ujenzi wa shule.

Jimbo Katoliki la Lindi limetoa eneo hilo lilipo katika Parokia ya Mnacho wilayani Ruangwa ambalo awali ilikuwa Shule ya Msingi ya Mnacho sasa imebadilishwa na kuwa sekondari.

Waziri Mkuu alitoa shukrani hizo jana alipokwenda kwenye Kanisa Katoliki la Theresia wa Mtoto Yesu, Parokia ya Mnacho kusalimia waumini.

Amesema lengo la kuibadilisha shule hiyo kuwa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Lucas Malia ni kuwawezesha watoto wa kike wa wilaya hiyo kusoma katika mazingira mazuri.

Waziri Mkuu ambaye aliambatana na mkewe, Mary, alisema shule hiyo ya bweni itawapunguzia vishawishi watoto wa kike, hivyo kuwawezesha kutimiza malengo yao.

Awali, uongozi wa parokia hiyo uliipongeza serikali ya awamu ya tano kwa kuboresha huduma za jamii zikiwamo za afya, elimu pamoja na miundombinu katika wilaya hiyo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Hashim Mgandilwa, amewaomba viongozi wa dini washikamane na wahakikishe wanatatua changamoto ya mmomonyoko wa maadili.

Alisema changamoto ya mmomonyoko wa maadili katika jamii hususani kwa vijana ni kubwa, hivyo ni jukumu lao kuhakikisha kwamba wanawarejesha kwenye maadili bora.

Kadhalika, Waziri Mkuu alikagua ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Lucas Malia na alisema kwamba ameridhishwa na maendeleo ya ujenzi wake.

Shughuli zinazoendelea katika shule hiyo ni pamoja na ujenzi wa mabweni, vyumba vya madarasa, maabara na nyumba nne za walimu ambazo tayari ujenzi wake umekamilika.

# Vyama vyasusia uchaguzi

**Na Elizabeth Zaya**

VYAMA vinane vya upinzani vimesema havitashiriki uchaguzi wa marudio katika kata 32 unaotarajiia kufanyika Juni 15, mwaka huu, endapo Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) haitatekeleza agizo la Mahakama la kuwataka wakurugenzi wa halmashauri kutosimamia uchaguzi.

Vyama vilivyosusia ni Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), ACT-Wazalendo, NCCR-Mageuzi,Chauma, UPDP, NLD,CCK na DP.

Wakizungumza kwa niaba ya vyama hivyo nane, viongozi wa vyama vinne vya ACT-Wazalendo, Chauma, UPDP na NLD walisema kitendo cha NEC kuwaruhusu wakurugenzi kuendelea kusimamia uchaguzi huo ni kuidharau mahakama na kwamba hata vyama vyao haviwezi kushiriki kwa kuwa kufanya hivyo ni kushirikiki katika dharau dhidi ya hukumu ya mahakama.

Akisoma tamko la vyama hivyo mbele ya waandishi wa habari jana jijini Dar es Salam, Mwenyekiti wa Taifa wa UPDP, Fahmi Dovutwa, alisema pamoja na kwamba mahakama ilitoa hukumu ya kufuta vifungu vya sheria vinavyowapa wakurugenzi mamlaka ya kusimamia uchaguzi, lakini vyama hivyo vimekuwa vikipokea barua ya mchakato wa uchukuaji na urudishaji wa fomu kutoka kwa wakurugenzi hao.

"Tume ya Taifa ya Uchaguzi(NEC), ilitangaza kufanyika kwa uchaguzi mdogo wa marudio katika kata 32, Juni 15, mwaka huu na baada ya tangazo hilo, wakurugenzi wamekuwa wakiviandikia vyama vya siasa juu ya mchakato wa kuchukua na kurudisha fomu na kutia saini kama wasimamizi wa uchaguzi huo," alisema Dovutwa.

Aliongeza: "Itakumbukwa kuwa Mei 10, mwaka huu, Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam ilitoa uamuzi wa kuvifuta vifungu vya sheria ya uchaguzi ambavyo vilikuwa vinawapa mamlaka wakurugenzi wa halmashauri nchini kuwa wasimamizi wa uchaguzi katika maeneo yao. Mara baada ya uamuzi huo wa Mahakama, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema serikali itawasilisha kusudio lake la kukata rufani kupinga uamuzi huo, lakini mpaka tunavyozungumza hivi, hakuna rufani iliyowasilishwa wala ombi la kisheria la kusitisha utekelezaji wa hukumu hiyo."

Dovutwa alisema vyama hivyo vinaitaka NEC kupitia mamlaka yake iliyopewa, kuteua wasimamizi wa uchaguzi huo wa marudio mara moja na kama itaendelea na msimamo wake wa kudharau amri ya mahakama, vyama hivyo vitachukua hatua ya kutoshiriki uchaguzi huo na vitawasiliana na wanaharakati waliofungua kesi hiyo kupeleka shauri mahakamani la kukazia hukumu hiyo na kuitaka mahakama iichukulie hatua NEC kwa kudharau amri hiyo ya mahakama.

Pia alisema vitaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika madai ya kuhakikisha wanapata tume huru ya uchaguzi ambayo itakuwa na uwezo kamili na mamlaka ya kuandaa na kusimamia

INAENDELEA UK. 8



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, akikagua ng'ombe bora wa maziwa mwenye uwezo wa kutoa lita 30 kwa siku, wakati alipotembelea mabanda ya maonyesho kwenye Wiki ya Maziwa ambayo kitaifa yamefanyika uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha jana. **PICHA MPIGAPICHA WETU.**

# Hoja 6 mtihani kwa Waziri Mpango leo

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

BUNGE la Bajeti linaloendelea jijini Dodoma, linaingia katika juma la 10 leo, huku wabunge wakitarajiwa kumbana kwa hoja sita Waziri wa Fedha na Mpango, Dk. Philip Mpango.

Ratiba ya mkutano huo iliyotolewa na Idara ya Habari na Elimu ya Bunge, inaonyesha leo kutakuwa na mjadala wa makadirio ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha. Hoja ambazo zinatarajiwa kuibuka wakati wa mjadala huo ni pamoja na kuongezeka kwa Deni la Taifa, kasi ya kufungwa kwa biashara nchini, kufungwa kwa maduka ya kubadilisha fedha, utekelezaji usioridhisha wa miradi ya maendeleo, kutonunuliwa kwa korosho na changamoto katika kuzingatia sera na Sheria ya Fedha.

Akizungumza na Nipashe jijini Dodoma jana, Naibu Waziri Kivuli wa Fedha na Mipango, David Silinde, alisema katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni leo kuhusu makadirio ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha, wanatarajia kuihoji serikali kuhusu kile alichodai Wizara ya Fedha kushindwa kusimamia vizuri sera na Sheria ya Fedha.

Silinde ambaye pia ni Mbunge wa Momba (Chadema), alisema kambi yao pia itambana Waziri Mpango kuhusu kutonunuliwa kwa korosho zilizokusanywa na serikali kutoka kwa wakulima.

Alisema kutonunuliwa kwa zao hilo kumeikosesha nchi fedha nyingi za kigeni, ikizingatiwa mauzo ya zao hilo yamekuwa yanaingiza fedha nyingi za kigeni kuliko mazao mengine yote ya biashara yakikusanywa kwa pamoja.

Vilevile, Silinde alisema kambi yao itambana Waziri Mpango kuhusu kutozingatiwa kwa sera na Sheria ya Fedha, akieleza kuwa baadhi ya wizara zimepewa mabilioni ya shilingi ambayo hayakuidhinishwa na Bunge katika mwaka huu wa fedha. Fedha ambazo zimekuwa zikilalamikiwa na kambi hiyo katika Bunge la Bajeti mwaka huu ni zile zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za wizara maeneo ya Ihumwa na Mtumba jijini Dodoma.

"Msimamizi mkuu wa masuala ya fedha ni Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa hiyo, mambo mengi yanapokuwa yanashindwa kutekelezwa, tuhuma nyingi lazima tunazipeleka huko.

"Kunapokuwa na mambo ya ubadhirifu, utakatishaji wa fedha, kufungwa kwa maduka ya kubadilisha fedha na mambo mengine... jukumu hilo ni la Wizara ya Fedha.

"Hata suala la korosho kutonunuliwa, kupaa kwa Deni la Taifa tunaamini ni kushindwa kwa Wizara ya Fedha kutimiza majukumu yake vizuri.

"Kwa hiyo, tutaibana serikali kesho (leo) kuhusu mambo haya. Yale ambayo yanahusu masuala ya kawaida na maisha ya watu, tutayahoji kwenye mjadala wa bajeti kuu ya serikali," Silinde alisema.

Ratiba ya mkutano wa Bunge la Bajeti inaonyesha makadirio ya bajeti kuu ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha yatawasilishwa bungeni Alhamisi ya wiki ijayo.

Kwa mujibu wa Spika Job Ndugai, baada ya kikao cha leo cha Bunge, shughuli za chombo hicho cha kutunga sheria zitasitishwa kwa siku sita hadi Jumatatu ijao kwa lengo la kupisha Sikukuu ya Eid El Fitri.

## HABARI KITAIFA



Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, akizungumza na Mama Maria Nyerere, wakati wa ibada ya siku ya kumuombea Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere kuwa Mwenyeheri na hatimaye kuwa Mtakatifu katika Kanisa la Watakatifu Mashahidi wa Uganda, Parokia ya Namugongo, Kampala nchini Uganda. **PICHA: PPU**

# Serikali yatangaza kiwango kipya cha mifuko mbadala

**Na Felix Andrew**

WAZALISHAJI wa mifuko mbadala nchini wametakiwa kutumia kiwango kipya cha lazima cha mifuko mbadala kilichotolewa hivi karibuni na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Akizungumza na waandishi wa Habari jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Lazaro Msasalaga, alisema kuwa kiwango hicho ni TZS 2292: 2018 na TZS 2130: 2018.

Aliwataka wazalishaji mifuko mbadala nchini kuanza kupeleka maombi kwa ajili ya leseni za kazi zao.

Alisema shirika bado halijapokea maombi juu ya utengenezaji wa vifungashio na mifuko mbadala tangu katazo la mifuko ya plastiki lilipoanza kutumika wiki iliyopita.

Msasalaga alisema katika kuungana na serikali wao kama shirika la viwango limechukua hatua tatu muhimu kwa wazalishaji wa vifungashio vilivyopigwa marufuku.

"TBS limesitisha uhuishaji wa ubora kwa wazalishaji wa aina hiyo ya bidhaa ya vifungashio, kutopokea maombi mapya ya uzalishaji wa vifungashio pamoja na kuondoa katika matumizi kwa kiwango kilichokuwa kinatumika cha plastiki," alidokeza.

Aidha, Msasalaga ambaye pia ni Kaimu Mkurugenzi Udhibiti Ubora wa TBS, amewatahadharisha wote wanaotumia vibaya nembo ya shirika hilo, na kuwa wakikutwa sheria kali itachukuliwa.

"Kwa Sheria ya TBS; zinasema endapo mtu akikutwa na matumizi ya nembo yetu kama atakubali atatozwa faini ya kiasi cha Sh. milioni 20 ila akikaidi tutampeleka mahakamani na ikibainika atatozwa faini pamoja na kifungo jela," alisema.

INAENDELEA UK. 8

## Waziri ataka kasi ulipaji mafao NSSF

**Na Salome Kitomari**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Vijana na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, ameagiza mifuko ya hifadhi ya jamii nchini kutowasumbua wastaafu na wanaodai mafao yao kisheria, badala yake kuwalipa kwa wakati.

Waziri huyo aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ufunguzi wa mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) la 45, lililokutana mkoani Morogoro.

Aidha, ameitaka mifuko hiyo kuwahudumia kwa haraka wastaafu na wanaodai mafao mbalimbali iliyopo kisheria na kanuni, ili kupunguza au kumaliza malalamiko, ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya uandikishaji wa wanachama.

Pia, aliipongeza Bodi ya NSSF kwa kazi nzuri ikiwamo kuboresha matumizi ya mfumo wa kielektroniki kama mfumo wa malipo wa serikali wa kielektroniki (GePG) unaomwezesha mwajiri kuwasilisha michango yake kirahisi.

Aidha, alisema mfumo mwingine ni mfumo wa kielektroniki wa uhasibu (Orcale Financial System) ambao umeboresha utendaji wa shirika kwa kipindi kifupi.

Kwa mujibu wa Mhagama, mifumo hiyo itapunguza malalamiko ya wanachama ikiwamo ya kupata malipo yao kwa wakati.

"Menejimenti, Mwenyekiti wa Bodi mmenifariji sana, lakini nimeona mmetengeneza mfumo wa kielektroniki wa kihasibu, hongereni mmefanyakazi nzuri sana," alisema Mhagama.

Aidha, aliwataka kuongeza kasi ya uandikishaji wa wanachama wa kuwa sekta binafsi ina wanachama wengi wanaotakiwa kujiunga NSSF kwa mujibu wa sheria.

INAENDELEA UK. 8

## Makonda amuenzi Dk. Mengi kufuturisha wenye ulemavu

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amewaomba watu wenye kampuni katika mkoa wake kutoa nafasi za ajira kwa watu wenye ulemavu ambao wana sifa na uwezo wa kufanya kazi.

Makonda alitoa wito huo juzi, wakati akizungumza katika hafla ya futari, aliyoiandaa kwa ajili ya watu wenye ulemavu zaidi ya 4,000 wa mkoa huo, kwa lengo la kumuenzi aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, aliyekuwa akiandaa chakula kwa kundi hilo kila mwaka.

Makonda alisema endapo kampuni zitaajiri watu wenye ulemavu, zitakuwa zinaongeza hamasa ya watu hao kusoma, wazazi kuacha kuwaficha watoto wenye ulemavu ndani na kuongeza baraka katika kampuni na taasisi zao.

"Watu wote wenye kampuni katika Mkoa wa Dar es Salaam, nawaomba kwa unyenyekevu mkubwa, nisingependa kupita kwenye kampuni zenu kukagua kuona mmeajiri watu wenye ulemavu wangapi, nawaomba sasa muajiri watu wenye ulemavu kwa sababu sifa wanazo na uwezo wanao," alisema Makonda.

Aliwataka pia wakazi wa jiji hilo kuacha tabia ya kuwabagua watu wenye ulemavu na badala yake wajenge upendo na ushirikiano katika shughuli mbalimbali.

Kadhalika Makonda aliwatahadharisha wamiliki wa taasisi za kiraia zilizojisajili kwa lengo la kusaidia kundi la watoto yatima na wasiyojiweza, lakini hawafanyi hivyo.

"Ni laana kutofanya kazi ya kuwasaidia watu wenye ulemavu. Kuna taasisi moja sitaitaja jina, imekuwa ikipokea Sh. milioni 600 kwa miezi mitatu, lakini haiwasaidii watoto na badala yake wamejinunulia magari ya kifahari na kujenga nyumba za kisasa, wanafanya biashara nyingine na ukienda kwenye hizo ofisi hakuna hata kiti cha kukalia," alisema Makonda.

Alisema watu wanaofanya vitendo kama hivyo wanatafuta laana kutoka kwa Mungu kwa sababu watoto hao hawakutamani kuwa wahitaji. Aidha, alisema aliandaa futari hiyo kwa ajili ya kumuenzi Dk. Mengi ambaye alikuwa mstari wa mbele kusaidia watu wenye ulemavu.

"Mzee wetu Dk. Mengi, alikuwa ni mmoja wa wafanyabiashara wakubwa aliyejitofautishwa na wengine kwa kuwathamini na kuwaenzi watu wenye ulemavu, jambo hilo nami nimejifunza na niliahidi kuendelea kumuenzi mzee wetu kwa vitendo na leo nimeanza safari ya kumuenzi kwa vitendo," alisema Makonda. Alieleza matarajio yake ni kuona mbegu aliyopanda Dk. Mengi ianze kutoa matunda.

Kadhalika alisema kazi hiyo wanafanya kama mkoa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao ya kumsaidia Rais John Magufuli kutimiza ahadi zake kwa Watanzania.


**PROTINS REVIEW CLASSES CENTRE**
**P.O.BOX 79696, Dar es Salaam**
**Tel: +255 737 732 57, 1 Mob: +255 759 099 099, +255 654 555000**
**Email: previewcentre@yahoo.com**

**TANGAZO**

Protins Review Centre inatangaza nafasi za kusoma kwa program zifutazo:

- √ Elimu ya secondary kwa miaka miwili (QT) kwa masomo yote
- √ Tuition Sessions kwa wanafunzi wa ordinary Secondary level na Advanced Secondary level
- √ Elimu ya Advanced level kwa mwaka mmoja – michepuo yote.
- √ Kozi za kiingereza levels zote:
  - **Beginners**
  - **Intermediate**
  - **Advanced.**

***Madarasa yenye viyoyozi kwa jili ya kuwezesha mazingira mazuri na ya kuvutia kujifunza.***

**TUPO:** MTAA WA LUMUMBA, Jengo la Furniture Centre, Mnazi mmoja, Ghorofa ya pili.

**WAHI MAPEMA NAFASI NI CHACHE.**

215257902

# Vituo vya afya 191 kujengwa nchini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-Tamisemi), Seleman Jafo, amesema serikali itashirikiana na Poland kujenga vituo 191 vya afya nchi nzima.

Amesema kuwa vituo hivyo vitakuwa vimekamilika vikiwa na vifaa tiba vitakavyosaidia wananchi kupata huduma ya afya katika vituo hivyo, hasa wajawazito na watoto wanaofuata huduma ya kujifungua umbali mrefu.

Vituo hivyo vitakuwa msaada mkubwa kwao kwa kuwa vitakuwa karibu na wananchi, ili kuwarahisishia kero na usumbufu wanaoupata, hivyo imedhamiria kwa dhati kutatua kero ya muda mrefu dhidi ya kinamama na watoto kupata huduma za afya za uhakika mahali walipo.

Waziri Jafo alisema hayo wakati wa kupokea wawekezaji kutoka Poland waliokuja nchini kukutana naye kwa ajili ya kupanga mikakati ya sekta ya afya ya kujenga vituo vya afya kwenye Halmashauri mbalimbali nchini.

Katika mazungumzo hayo kati ya Waziri Jafo na wawekezaji hao walikubaliana kuweka mikakati hiyo ya ujenzi wa vituo vya afya, na wizara yake itaridhia mipango hiyo sambamba na upatikanaji wa fedha zitakazosaidia kuimarisha vituo vya afya.

Aliipongeza Poland kwa kuwa na mahusiano na Tanzania hususan katika miradi ya maendeleo ukiwamo mradi huo wa sekta ya afya.

Alisema mradi huo umekuja wakati mwafaka kwa kuwa serikali inaendelea na ujenzi wa hospitali katika maeneo mbalimbali ili Watanzania wawe na uhakika na huduma za afya ambazo ni muhimu kwa maisha yao.

"Poland ni nchi iliyopiga hatua katika teknolojia ya afya, kilimo na viwanda, hivyo ni muhimu sana kushirikiana nao katika kutuletea teknolojia itakayowezesha wataalamu wetu kuitumia na kufanikisha shughuli mbalimbali za kitaaluma na kijamii ikiwamo sekta ya afya kwenye vituo mbalimbali katika kupata vifaa tiba vya kisasa," alisema.

Mwakilishi kutoka Poland, Julius Zellah, alimpongeza Waziri Jafo kwa mapokezi mazuri waliyopewa na kuahidi kutekeleza yote waliyoyapanga katika kutoa fedha za kujenga vituo vya afya na kuviwekea vifaa tiba kutoka kampuni ya Medical Equipment ya ALVO ya Poland.

Pia wamemualika Waziri Jafo kwenda Poland kushirikiana nao katika kufanikisha mpango huo haraka, ili wananchi waanze kupata huduma mapema iwezekanavyo ya matibabu.



Wachungaji watatu kutoka kanisa la KKKT Dayosisi ya Mashariki na Pwani na mmoja kutoka KKKT Dayosisi ya Ziwa Victoria Shinyanga, wakiwa katika mahafali ya 150 ya Chuo Kikuu cha Luther Seminary Minnesota cha nchini Marekani na sherehe iliyofanyika Kanisa Kuu la Kilutheri Minneapolis. Wahitimu hao ni Mchungaji Dk. Ernest William Kadiva (wapili kushoto) ametunukiwa shahada ya udaktari na wengine waliotunukiwa shahada ya pili ya sanaa ni Mchungaji Kishe Dismas Mhando (kulia), Kanasia Geofrey Msangi na Mchungaji Martha Ernest Ambarang'u wa Dayosis ya Ziwa Victoria Shinyanga. **PICHA: NOAH WILLIAM KADIVA**

# Mabasi 17 yafungiwa kwa kisa kuchezea ving'amuzi

**Na Salome Kitomari**

ZAIDI ya mabasi 17 yamekamatwa na kufungiwa kwa mwezi mmoja kwa makosa ya kuchezea mfumo wa ving'amuzi vya kudhibiti mwendo.

Akizungumza jana na Nipashe, Mkurugenzi wa Udhibiti wa Usafiri wa Barabara wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra), Johansen Kahatano, alisema madereva walichezea mifumo ili waweze kuendesha mwendo kasi.

Alisema baada ya kuwabaini hatua zilichukuliwa kwa mujibu wa kanuni, ambayo ni kuwafungia mwezi mmoja na kuwapa barua ya onyo.

"Tulichobaini walichezea mifumo ya umeme ambayo imeungwanishwa na king'amuzi kinachopeleka taarifa Latra na kumjulisha dereva kuwa amezidisha mwendo. Walifanya hivyo ili wakimbize magari," alisema.

Kwa mujibu wa Kahatano, zaidi ya magari 3,000 yamefungwa ving'amuzi kwa barabara zote kuu nchini na kwa sasa wanaelekea kwenye magari ya njia fupi.

"Tumejipanga ipasavyo baada ya kumaliza njia ndefu kwa sasa tunaandaa utaratibu ili ifikapo katikati ya mwezi huu tuanze njia fupi," alisema.

Alisema utekelezaji wa ving'amuzi hivyo umewezekana kutokana na wamiliki na madereva kukubali mfumo baada ya kuona una faida kwao.

Kuhusu mabadiliko yaliyotokea tangu kuanza kutumika kwa ving'amuzi, alisema ajali na madhara yanayosababishwa na ajali yamepungua kwa kiasi kikubwa na hivyo watumiaji wa vyombo hivyo kuwa salama muda wote wa safari.

"Kabla ya kuwapo kwa mfumo huu kulikuwa na ajali zenye madhara makubwa ziliua kati ya watu 10 hadi 20, lakini kwa sasa ikitokea ajali ni kifo kimoja au hakuna kabisa, tunaweza kusema zimepungua kwa zaidi ya asilimia 90," alisema.

Alisema faida nyingine ni kwa wamiliki wa magari kupunguza gharama za uendeshaji kama vipuri, mafuta na kwa sasa wanaweza kukata bima ndogo tofauti na zamani iliwabidi kukata bima kubwa kutokana na uwapo wa ajali mara kwa mara.

"Tunapata ushuhuda kutoka kwa wamiliki wa magari kuwa zamani walikuwa wanaishi roho juu juu kwamba basi likianza safari hana uhakika kama litafika, lakini kwa sasa wana utulivu na wanakata bima ndogo na fedha inayobaki kufanya mambo mengine ya maendeleo," alisema.

Alisema pia wameeleza kwa matumizi ya matairi, vipuri vingine, breki yamepungua kwa asilimia 30.

Kuhusu mfumo unavyofanya kazi, alisema king'amuzi kimefungwa kwenye basi na kinapeleka taarifa Latra ambako kuna watu wanaangalia, inapotokea dereva kaendesha zaidi ya kilomita 80 kwa saa kinapeleka taarifa na kupiga kelele kwenye gari yake ikimjulisha kuwa anakaribia kuzidisha au amezidisha mwendo.

Katibu Mkuu wa Chama cha Wasafirishaji Tanzania (Taboa), Enea Mrutu, aliliambia Nipashe kuwa mfumo huo ulioanza mwaka 2016, umesaidia kuwadhibiti madereva, kupunguza gharama za uendeshaji na ajali.


***Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-***

- **Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=**
- **Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=**
- **Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima**
- **Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku**

215227501





Waziri wa Maliasili na Utalii, Hamis Kigwangalla (katikati), akifurahia jambo na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Vodacom, Hisham Hendi (kushoto), wakati wa hafla ya futari iliyoandaliwa na Idara ya Biashara ya kampuni hiyo, katika kuadhimisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani pamoja na wateja wake jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela.
**PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Serengeti yashinda tuzo hifadhi Afrika

**Na Salome Kitomari**

HIFADHI ya Taifa ya Serengeti, imeshinda tuzo ya hifadhi bora barani Afrika kwa mwaka 2019.

Hii ni mara ya pili kwa hifadhi hiyo kushinda tuzo za kimataifa kutokana na utofauti wake na hifadhi nyingine duniani.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Kamishna Msimamizi Mwandamizi, Mawasiliano wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Pascal Shelutete, tuzo hiyo ilitolewa juzi nchini Mauritius.

Alisema ilitolewa na Taasisi ya World Travel Awards ambao ndiyo waandaaji wa tuzo hizo kila mwaka.

"Hii ni mara ya pili Hifadhi ya Serengeti kutangazwa hifadhi bora Afrika, baada ya mwaka jana kushinda tuzo hiyo kupitia mtandao wa safari za utalii duniani wa safaribooking.com," alisema.

Alifafanua kuwa washindi wa tuzo hizo hupigiwa kura na wabobezi katika masuala ya safari na utalii duniani kote.

"Ushindi wa Serengeti unatokana na jitihada kubwa zinazofanywa na Tanapa katika kusimamia vyema hifadhi ikiwa ni pamoja na kutangaza ili kuvutia watalii wengi nchini," alisema Shelutete.

Hifadhi ya Serengeti ni ya pili kwa ukubwa baada ya Ruaha, ikiwa ni kati ya 21 zilizopo chini ya Tanapa.

Hifadhi ya Serengeti ni maarufu kwa uhamaji wa nyumbu ambao huenda Masai Mara kwa kukatiza mto Masai Mara na ndiyo hifadhi pekee yenye wanyama wengi ambao huonekana kwa urahisi zaidi kiasi cha kupewa jina la uwanda wa wanyama.

# Museveni ammwagia sifa Mwalimu Nyerere

**Na Paul Mallimbo,** KAMPALA

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, amemwelezea marehemu Mwalimu Julius Nyerere kama kiongozi muhimu zaidi aliyewahi kutokea katika medani za kisiasa kwa Afrika katika historia.

Museveni aliyasema hayo wakati wa ibada ya kuombea mchakato wa Baba wa Taifa kuwa mwenyeheri na hatimaye mtakatifu, ibada iliyohudhuriwa na mataifa mbalimbali wakiwamo zaidi ya Watanzania 500.

Uganda imeitenga siku ya Juni Mosi ya kila mwaka kuwa ni Siku ya Nyerere, kwa ajili ya kuombea mchakato wa kumfanya awe mtakatifu. Ibada hiyo ya misa takatifu hufanyika katika Kanisa la Watakatifu Mashahidi wa Uganda la Namugongo, Kampala, Uganda.

Siku ya Nyerere, ambayo mwaka huu inaadhimishwa kabla ya mashahidi wa Uganda yenye ujumbe: "Taifa lenye furaha ni lile linalowakubali mashahidi", ilikuwa na lengo la kuuombea mchakato wa kumfanya Baba wa Taifa Julius Nyerere kuwa mwenyeheri na hatimaye mtakatifu.

Rais Museveni alisema kuwa yeye ni mtoto wa kwanza wa Mama Maria Nyerere, na alipongeza juhudi za familia ya Nyerere kwa kuungana na wanahija wengine kutoka nchi za Kenya, DRC, Rwanda, Burundi, Nigeria na duniani kwa ujumla kuja kuombea mchakato huo wa Nyerere kuwa mtakatifu.

"Hija siyo suala la kisiasa, lakini ni jambo linalohimiza umoja kwa nchi zilizo katika Umoja wa Afrika Mashariki pamoja na Afrika kwa ujumla," alisema.

Alisema suala hilo linapaswa kuwa la kihistoria, kiutamaduni na kisiasa, lakini zaidi

INAENDELEA UK. 8

# Ndalichako: Mitaala vyuo vikuu iboreshwe

**Na George Tarimo,** IRINGA

WAZIRI wa Elimu Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, Prof. Joyce Ndalichako, alivitaka vyuo vikuu kuboresha mitaala yake na njia za kufundishia wanafunzi ili kuwajengea vijana uwezo wa kutafuta suluhu ya matatizo badala ya kulalamika kwa kukosa ajira.

Waziri Ndalichako alisema hayo wakati akizungumza na Jumuiya Chuo Kikuu cha Iringa (UoI), ambapo alisema mitaala mingi ya vyuo vikuu bado ina mfumo wa kuwajengea hofu wanafunzi ya kutojaribu wala kupenda kutumia fursa zilizopo kufanya mambo na kutegemea kufanyiwa.

Waziri huyo alisema hayo kwenye maadhimisho ya miaka 11 ya Kitivo cha Sayansi na Elimu ya chuo hicho.

Waziri Ndalichako alisema serikali itaendelea kudhibiti ubora wa elimu ya vyuo hivyo na kutoa changamoto ya kuboresha mitaala kwenda na wakati na kuwanufaisha wahitimu.

"Wawe ni vijana ambao watakuwa chachu ya kuleta suluhu katika matatizo badala ya vijana kuwa walalamikaji. Hii tabia ya Watanzania kulalamika lazima mfumo wetu wa elimu uue hiyo tabia mbaya ambayo inajengeka kwa vijana walio wengi, unakuta mtu analalamika sasa nani afanye nchi hii ni ya kwetu lazima suluhu ya matatizo ya Watanzania zipatikane miongoni mwa wenyewe," alisema Ndalichako.

Aidha, aliwataka wanachuo kutokubali kutumika na kuwa wazalendo wa nchi yao.

Pia aliwataka wakuu wa vyuo vikuu kutoa mrejesho kwa wanafunzi kuhusu kozi zilizofutwa badala ya kuwaacha wakihangaika.




# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Kwa uchuro huu, TFF sasa iisuke upya TPLB

**MSIMU** wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2018/19, umemalizika kwa Klabu ya Simba kufanikiwa kutetea taji hilo, huku ikishuhudiwa timu ya African Lyon na Stand United zikishuka rasmi daraja.

Katika msimu huu ambao kwa mara ya kwanza katika historia ya ligi hiyo ulikuwa ukijumuisha timu 20, hatima ya timu mbili, Kagera Sugar na Mwadui FC kubaki Ligi Kuu ama kushuka itajulikana wiki hii.

Hiyo ni kutokana na mpangilio wa kanuni, ambapo timu mbili zilizoshika nafasi ya 19 na 20 zilitakiwa kushuka daraja moja kwa moja, wakati zilizomaliza nafasi ya 17 na 18 zikitakiwa kucheza mechi ya mchujo 'play off' dhidi ya timu zilizoshika nafasi ya pili Ligi Daraja la Kwanza hatua ya makundi na itakayoshinda kupanda Ligi Kuu ama kusalia Ligi Kuu.

Kwa mantiki hiyo, Kagera Sugar itavaana na Pamba mechi mbili, nyumbani na ugenini, huku Mwadui FC ikipepetana na majirani zao, Geita na mshindi wa jumla ndiye atakayecheza Ligi Kuu msimu ujao wa 2019/20.

Tayari Namungo FC na Polisi Tanzania zimepanda Ligi Kuu kuchukua nafasi za Stand United na African Lyon zilizoshuka msimu huu baada ya kumaliza katika nafasi ya 19 na 20 kwenye msimamo wa Ligi Kuu, huku wageni hao waliopanda wakimaliza nafasi za kwanza katika Ligi Daraja la Kwanza kwenye makundi yao. Hata hivyo, pamoja na ligi msimu huu kuendeshwa katika wakati mgumu kutokana na kutokuwa na mdhamini, tumeshuhudia ratiba isiyokuwa rafiki kwa timu kulingana na uchumi wao wakujikongoja.

Lakini pia Bodi ya Ligi (TPLB) mbali ya kuvurunda huko katika ratiba, ikifunga msimu kwa kuonyesha inavyoendesha ligi kienyeji baada ya kushindwa kutunza takwimu zake za msimamo wa Ligi Kuu kwa umakini.

Sote tulishuhudia Jumanne iliyopita baada ya mechi za kufunga msimu, Mtendaji Mkuu wa TPLB, Boniface Wambura, akinukuliwa akisema kuwa timu iliyoshuka daraja ni Kagera Sugar na kwamba Stand United itacheza mechi ya mchujo dhidi ya Pamba. Wambura alitoa kauli hiyo kutokana na takwimu za msimamo wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuonyesha kuwa Kagera Sugar na Stand United zinalingana kila kitu, pointi, tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa. Kwa mantiki hiyo, akaeleza kuwa kwa mujibu wa kanuni, utaratibu wa timu zilizolingana kila kitu, matokeo ya timu hizo zilipokutana ('head to head') huchukua nafasi yake, hivyo yakaibeba Stand United.

Hakika huu ni udhaifu mkubwa kwa TFF na TPLB yake, kwa taasisi kubwa kama hiyo kushindwa hata na kitengo kimoja tu cha michezo cha Nipashe ambacho msimamo wake ulikuwa sahihi ukionyesha Stand United ndiyo inayopaswa kushuka daraja na Kagera Sugar kucheza mechi ya mchujo.


Takwimu za Nipashe ambalo lilikuwa likiandaa msimamo huo tangu ligi ilipoanza, zilikuwa zikionyesha timu hizo zinalingana pointi (44 kila moja), lakini Kagera Sugar ikiwa na hasi 10 ya tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa, wakati Stand United ikiwa na hasi 12, takwimu ambazo ni sahihi kabisa nazilizotumika na TPLB kubatilisha matokeo yake na kuishusha Stand United.

je (mfano livescore) inayotunza takwimu za matokeo ya michezo ikiwamo msimamo ilikuwa ikionyesha kuwa sahihi kama ilivyokuwa kwa Nipashe.

Hii ni aibu kubwa kwa shirikisho la soka nchini kwa mitandao ya nje kuwa makini zaidi kwa ligi yetu kuliko wenye soka lao hao TFF, hivyo kuna haja sasa TPLB kuvunjwa na kusukwa upya ili kurejesha imani kwa wadau wa soka ambao kwa ujumla hawakuridhishwa na uendeshwaji mzima wa Ligi Kuu kwa msimu wa 2018/19. Nipashe tunatarajia kuona hatua kali zikichukuliwa kwa wahusika ikiwamo TPLB kuvunjwa na kusukwa upya kabla ya msimu mpya wa Ligi Kuu 2019/20 Agosti mwaka huu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kasoro TFF ya Karia hata ile ya Malinzi zilikuwapo

Na Adam Fungamwango

**BAADA** ya Ligi Kuu Tanzania Bara kumalizika, wadau wengi wakiwamo wachezaji wa zamani, makocha wamekuwa wakihojiwa jinsi walivyoiona ligi hiyo msimu huu.

Baadhi wameeleza mazuri na upungufu na kushauri jinsi gani ya kupunguza makosa msimu ujao. Lakini wapo ambao wanaponda kuwa hawajawahi kuona ligi mbovu kama hii iliyomalizika.

Sababu inaelezwa kuwa ni viporo vingi kwa Simba. Wengine wanadai Yanga ilipewa upendeleo maalum kwa kucheza mechi zaidi ya 10 kwenye uwanja wake wa nyumbani, Taifa bila kutoka mwanzoni mwa ligi. Wengine ni kwa sababu hakuna udhamini.

Ni kweli kila mtu ana maoni yake, lakini mara nyingi inashauriwa kuwa maoni yaendane na hoja, takwimu na rekodi hasa kwa watu wa michezo.

Binafsi, kwa maoni yangu wale wanaodai kuwa Ligi Kuu ya msimu huu ilikuwa mbovu zaidi kwa sababu wanazozisema, hawajalinganisha na hizo zilizopita na badala yake huenda wanazungumza kwa hisia zao ndani ya mioyo, kufuata mkumbo au vyote viwili.

Kuhusu suala ya viporo vya Simba ambavyo ndivyo vinalalamikiwa sana ni kwamba hata huko nyuma, yaani misimu mitatu minne hadi mitano hakujawahi kuchezwa ligi ambayo haikuwa na viporo.

Nadhani msimu huu viliongezeka kwa sababu mbalimbali, ikiwamo kubadilika kwa Kalenda ya Shirikisho la Soka Afrika (Caf).

Hata TFF iliyopita chini ya Jamal Malinzi ilikuwa na viporo kwa timu ambazo zilikuwa zikishiriki michuano ya kimataifa hasa Yanga na Azam.

Nakumbuka kuna wakati hata Azam ilikuwa ikiomba kwenda nje ya nchi kwa ajili ya mechi za kirafiki, mechi zao zinaahirishwa, lakini ligi inaendelea na yenyewe ikawa na viporo, lakini ligi ilimalizika na hatukusikia sauti za ligi mbovu.

Hakukuwa na sababu yoyote ya maana ya Azam kwenda nje wakati kuna ratiba ya ligi. Sipati picha kama ndiyo ingekuwa sasa wakati wa Wallace Karia Azam ingepewa ruhusa hiyo na mechi zake kuwekwa viporo ingefunika vilivyo kwenye mitandao ya kijamii.

Kuhusu maamuzi tata ya waamuzi, hilo hata halipaswi kujadiliwa kwa sababu miaka nenda miaka rudi lipo kwenye Ligi Kuu, kiasi cha baadhi tulishawahi kuandika makala miaka ya nyuma kuwa imefika wakati kuleta baadhi ya waamuzi kutoka nje ya nchi kwenye baadhi ya mechi, lakini si utawala wa Malinzi wala wa Karia, hakuna kilichotekelezeka. Nashangaa msimu huu eti kuonekana kuwa limekuwa kubwa zaidi wakati matukio ni yale yale tu.

Kuhusu suala ya Kagera Sugar kuonekana kama imeshuka, lakini kumbe mahesabu yalikosewa, hili nalo linaonekana kama jambo la ajabu kabisa ambalo halijawahi kutokea kwenye historia ya soka na kuifanya TFF hii kuhesabika kuwa ni dhaifu, lakini misimu miwili nyuma kulikuwa na suala ambalo hadi leo bado ni kitendawili la Kagera Sugar dhidi ya Simba.

TFF iliyopita eti ilishindwa kujua kama mchezaji wa Kagera Sugar Mohamed Fakhi ana kadi tatu za njano au la.

Baada ya Bodi ya Ligi kujiridhisha kuwa kadi ilikuwapo, TFF iliingilia kati, lakini haikusema kuwa ilikuwapo au la, badala yake iliwaita viongozi wa Kagera Sugar, mchezaji mwenyewe na waamuzi wote, wakawaweka karibuni wiki nzima Dar es Salaama kwa ajili ya kuitafuta kadi au kuwaliza.

Kilichoamuliwa ni matokeo ya mechi kuwa kama yalivyokuwa na haikusemwa rasmi kama ilikuwapo au la, badala yake ikatamkwa tu kuwa mchezaji huyo atatumikia adhabu yake ya kukosa mchezo kwenye mechi inayokuja. Hiki kilikuwa ni kituko cha mwaka kwa sababu mwamuzi wa kati anaweza kuthibitisha kama alimpa mchezaji au la. Lakini ligi iliendelea na ikaisha, hakukuwa maneno mengi kihivyo.

Kwa mifano hii tu michache, inaonyesha kuwa mapungufu ya TFF ya sasa yalikuwapo hata huko nyuma.

Binafsi, sipendi upungufu huo uwe unajirudi, lakini napinga wale wanaoonekana kutaka kuifanya TFF ya Karia ionekane ndiyo imeoza kuliko zilizopita na yote yanayotokea ni maajabu na hayajawahi kuonekana kwenye soka la Tanzania. Tunachotakiwa kushauri ni kuwaambia kuwa msimu ujao wajitahidi kupunguza upungufu uliojitokeza msimu huu.

# Wakati umefika kwa Malamba Mawili kuwa na kituo cha polisi

*NDUGU Mhariri pole na majukumu ya kila siku kwa ujenzi wa taifa letu changa, na pia ninashukuru kupata nafasi katika gazeti lako ili niweze kutoa dukuduku langu.*

*Kwanza kabisa mimi ni mkazi wa Malamba Mawili, jijini Dar es Salaam, eneo hili linakabiliwa na ukosefu wa huduma mbalimbali za muhimu ikiwa ni pamoja na kituo kidogo cha polisi.*

*Tulikuwa tukitegemea kituo cha polisi cha Kwa Yusuf kilichokuwa kando ya barabara ya Morogoro, eneo la Mbezi Mwisho, umbali wa zaidi ya kilometa mbili kutoka Malamba, lakini kimehamishiwa mbali zaidi baada ya bomoabomoa iliyofanyika kando ya barabara hiyo.*

*Kutokana na hali hiyo, tumejikuta tukiwa mbali zaidi na huduma za polisi, hivyo tukikumbwa na matatizo ambayo yanahitaji msaada wao inawezekana ikawa vigumu kuwapata kwa wakati kwa sababu ya umbali.*

*Kwa hali hiyo ndugu Mhariri, naomba zifanyike jitihada za makusudi za kuhakikisha eneo hili linapata huduma za polisi kuliko kutegemea maofisa wa polisi wale wa doria tu, ambao inawezekana likatokea tukio wakati hawapo eneo hili.*

*Nakumbuka sisi wakazi wa eneo hili tulikutana kwa ajili ya mkakati wa kutafuta aneo ambalo linaweza kutolewa ili kujenga kituo kidogo cha polisi, ambapo eneo lilipatikana, lakini masharti yakawa ni magumu, hivyo ikashindikana kuwezesha ujenzi wa kituo hicho.*

*Kuna mtu alijitolea kutoa eneo, lakini ikaelezwa katika kikao kwamba siku hizi ili kujenga kituo cha polisi ni lazima eneo la kiwanja liwe kubwa, hivyo mpango wa ujenzi ukawa umeishia hapo kimsingi pamoja na mtu huyo kuwa tayari kutoa eneo lake.*


*Malamba Mawili kwa sasa imepanuka sana inahitaji kuwa na huduma hiyo, hivyo tunaomba ufanywe utaratibu ambao utasaidia kupata eneo la kutosha ili sisi wananchi tuchangie ujenzi.*

**Mkazi Malamba Mawili_ Dar**

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Azam inapaswa kusukwa upya kumudu ushindani Kombe la Caf




**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Klabu ya Azam FC mwakani itaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika (Caf) baada ya kuifunga Lipuli bao 1-0 kwenye mechi ya fainali iliyochezwa Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi.

Lilikuwa ni bao la Mzambia Obrey Chirwa ambalo limeifanya klabu hiyo ambayo inatakiwa kuwa mfano kwa zingine kuweza kujaribu bahati yake ya kuipeperusha vema bendera ya Tanzania.

Azam iliyowahi kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara msimu wa 2013/14, imeiwakilisha nchi kwenye michuano hiyo kama mara tatu hivi na hii inakwenda kuwa ni mara ya nne.

Pamoja na kuwa ni timu inayojitosheleza kwa kila kitu, lakini haijawahi kufanya vema kwenye mechi za kimataifa mara zote hizo ambazo imeshiriki, si Ligi ya Mabingwa au Kombe la Shirikisho ambalo imeshiriki mara mbili.

Cha ajabu ni kwamba Simba ambayo kwa mwaka mmoja tu ilipopata mwekezaji Mohamed Dewji na kutwaa ubingwa ikaiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa, ilikwenda moja kwa moja hadi robo fainali.

Kiuchumi, Azam haitofautiani sana na Simba na unaweza kusema kuwa mpaka sasa bado Azam inaweza kuwa juu ya Wekundu wa Msimbazi hao kwa sababu yenyewe ina hosteli za kulala wachezaji pamoja na uwanja wake.

Pamoja na hayo yote, Azam si tu kwamba imekuwa haiiwakilishi vema nchi kwenye mechi za kimataifa, lakini hata kwenye Ligi Kuu nako imekuwa ikihaha kupata ushindi hata na timu ambazo zimekuwa zikiishi kwa kuungaunga.

Mfano mzuri ni kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza dhidi ya Yanga ilipofungwa bao 1-0 kwenye mazingira ambayo yanasikitisha.

Ni kwamba wapinzani wao walikuwa wanatoka kwenye mgomo. Wachezaji wa Yanga walikuwa wamegoma, huku wa Azam wakiwa wako kambini. Mgomo ulipokwisha, wachezaji wa Yanga sidhani kama hata kambini walikaa, kwani kesho yake tu waliingia uwanjani na kuitwanga Azam 1-0.

Kushika kwake nafasi ya tatu, nyuma ya Yanga iliyokuwa na matatizo mengi, huku yenyewe mambo yakiwa shwari, lakini pia ikiwa inasumbuliwa na timu za kawaida tu, inaashiria kuwa bado ina kazi kubwa ya kufanya kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho mwakani.

Kwa miaka ya karibuni Kombe la Shirikisho Afrika si la lelemama, kwani huzikutanisha klabu kubwa, lakini pia hupokea timu zilizotoka Ligi ya Mabingwa zingine zikiwa zimetoka kwa bahati mbaya na kuja kuuwasha moto.

Mfano hata mabingwa wa sasa wa kombe hilo, Zamaleki walitoka kwenye Ligi ya Mabingwa na walipofungwa ndipo walidondokea kwenye michuano hiyo.

Timu kama Gor Mahia, Nkana FC, zilikuwa Ligi ya Mabingwa na zilikuwa timu bora, lakini zilitolewa na kwenda shirikisho ambako zilitolewa kwa tabu hatua ya robo fainali.

Hii inaonyesha kuwa kwenye kombe hilo pia hakuna mzaha na mzani wake ni sawa tu na kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika.

Nionavyo mimi ni kwamba kwa kikosi kilichopo kwa sasa hakikidhi kabisa mahitaji ya kucheza kombe hilo kabla ya kufanyiwa marekebisho makubwa.

Kama kilishindwa kupata hata nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu, mbele ya Yanga iliyokuwa hoi kiuchumi, lakini pia hata kwa kiwango cha soka, hivyo kisijidanganye kama kinaweza kupambana hata na Gor Mahia au Nkana FC kwa sasa, achilia mbali Zamaleki, Asante Kotoko, au Raja Casablanca.

Ukikiangalia kikosi cha Azam kwa sasa kuna baadhi ya wachezaji hawastahili kuichezea tena klabu hiyo kuelekea kwenye michuano ya kimataifa.

Kuna baadhi ya wachezaji wachache wa kigeni ndiyo wenye uwezo wa kuichezea timu hiyo, huku wengine viwango vyao vikiwa vimeshuka na wengine kutia shaka.

Ili kufanya vema kimataifa viongozi wa Azam na benchi la ufundi inabidi wakae chini kwanza na kuanza kusajili wachezaji wa Kitanzania wenye uwezo wa hali ya juu, lakini pia kuwapata wachezaji wa kigeni wenye kiwango kikubwa ili kuungana na waliopo kwa ajili ya si tu kushiriki michuano hiyo, lakini pia kuiwakilisha vema nchi kwenye michuano ya kimataifa kama ilivyofanya Simba mwaka huu.

**KABWELA** **NA FADHIL MOHAMMED**



# Vyama vyasusia uchaguzi

INATOKA UK. 2

uchaguzi huru na haki ikiwa ni pamoja na kuwa na watendaji na wasimamizi wake wasiofungamana na chama chochote cha siasa.

**UBORESHAJI WA DAFTARI**

Vyama hivyo vilitumia nafasi hiyo pia, kuikumbusha NEC kutangaza utaratibu wa kuanza kuandikisha wananchi katika daftari la kudumu la wapigakura katika kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa.

"Tunatambua kuwa NEC, imetangaza uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura na imetoa tangazo la nafasi za kazi kwa ajili ya makalani na wasimamizi wa kusimamia kazi hiyo. Kupitia tamko hili, tunaitaka pia iteue wasimamizi wa shughuli hiyo kwenye ngazi za halmashauri kote nchini ambao sio wakurugenzi kwa sababu tayari mahakama imeshafuta vifungu vya sheria ya uchaguzi ambavyo vilikuwa vinawapatia mamlaka wakurugenzi hao kuwa wasimamizi wa moja kwa moja wa uchaguzi," alisema Dovutwa.

Dovutwa alisema endapo NEC itatoa ratiba rasmi ya kuanza kwa uandikishwaji katika daftari la kudumu litasaidia wadau mbalimbali kufanya maandalizi mapema.

"Ni Jambo baya sana mpaka sasa NEC imekiuka Katiba. Sheria ya uchaguzi sura namba 343, kifungu namba 15(5) na kifungu cha 21(5) kimeiamuru kuboresha daftari la kudumu la wapigakura mara mbili kati ya uchaguzi mkuu na unaofuata, lakini tangu kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu mwaka 2015, haijatekeleza agizo hilo la kisheria," alisema Dovutwa.

Aliongeza: "Kupitia tamko hili, tunaitaka NEC kutangaza ratiba ya shughuli hiyo kwa nchi nzima kwa sababu ratiba hiyo ni sehemu ya muongozo wa wadau mbalimbali na kujipanga kufanya maandalizi ya kushiriki katika uchaguzi huo pamoja ikiwamo uhamasishaji na maandalizi ya mawakala."

**KAULI YA NEC**

Hata hivyo, Mkurugenzi wa NEC, Dk. Athuman Kihamia, akizungumza na Nipashe, alisema uchaguzi huo wa madiwani hauathiri kwa namna yoyote hukumu iliyotolewa na Mahakama Kuu.

"Tume inaheshimu maamuzi ya Mahakama Kuu na inawahakikishia kuwa haijagusa au kuathiri sehemu ya vifungu ambavyo Mahakama Kuu imevitolea hukumu.

Aliongeza :"Uchaguzi huu wa madiwani unaofanyika hauathiri hukumu hiyo wala haujavunja matakwa ya hukumu hiyo wala haungiliani na hiyo hukumu iliyotolewa," alisema Dk. Kihamia

# Waziri ataka kasi ulipaji mafao NSSF

INATOKA UK. 3

"Kazi kubwa ya NSSF ni kuhakikisha kila Mtanzania aliyeko sekta binafsi na isiyo rasmi anaandikishwa kwa mujibu wa sheria ya hifadhi ya jamii. NSSF ihakikishe inaandikisha wanachama wapya kwa wingi," alisisitiza.

Alisema watumishi wa mfuko huo hawatakiwi kukaa ofisini, badala yake wanatakiwa kwenda kuandikisha wanachama kwenye maeneo mbalimbali ya sekta binafsi.

Alisema kuwa hatavumilia kwa namna yoyote ile mtendaji ambaye hatafikia malengo yaliyowekwa na shirika.

Kadhalika, aliagiza kutumia baraza la wafanyakazi kupima utendaji wa watumishi, na kwa watakaoshindwa kutimiza malengo wachukuliwe hatua za kisheria.

Waziri huyo alisema kupitia uchumi wa viwanda, vingi vitamilikiwa na sekta binafsi na vitakuwa na wafanyakazi wengi wanaotakiwa kujiunga kwenye mifuko wa NSSF, na kwamba ndiyo wakati wa kutumia fursa kuwasaka wanachama kokote waliko.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya NSSF, Balozi Ali Idi Siwa, alisema katika mwaka wa fedha wa 2018/2019, waliweka lengo la kuandikisha wapya 119,749, lakini hadi Machi mwaka huu wameandikisha wanachama wapya 98,969 sawa na asilimia 82.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Vijana na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama.

Alisema NSSF ilikusanya Sh. bilioni 594.94 ikiwa ni asilimia 104.38 ya lengo la kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 570.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, Sh. bilioni 294.81 zililipwa kwa wastaafu, mafao ya kukosa ajira, kujitoa, uzazi, msaada wa mazishi, matibabu, ulemavu na urithi kwa wanachama 57,572.

Balozi Siwa alisema mwaka 2019/2020 wamejiwekea malengo ya kuandikisha wanachama 210,000 na kukusanya michango ya zaidi ya Sh. trilioni 1.28.

Aidha, alisema shirika hilo limepanga kuwekeza kiasi cha Sh. bilioni 860.4 katika maeneo mbalimbali ya uwekezaji ikiwamo kiwanda cha sukari cha Mkulazi.

# Serikali yatangaza kiwango kipya cha mifuko

INATOKA UK. 3

Mifuko ya plastiki imepigwa marufuku kuanzia Juni mosi, mwaka huu, ambapo sheria kali zitachukuliwa endapo yoyote atakayekutwa anatumia au kuuza bidhaa hizo atapigwa faini au jela au vyote kwa pamoja.

Kifungu au Kanuni namba 8 ya Sheria ya Kuzuia Matumizi ya Mifuko Plastiki ya mwaka 2019, kinatanabaisha juu ya makosa yatokanayo ya uingizaji, kusafirisha nje ya nchi, kuagiza, kuhifadhi na kuagiza kifungu hiki kinakataza uingizaji wa bidhaa hizo.

Adhabu ya wanaosambaza na kuhifadhi ni faini kiasi kisichozidi shilingi milioni 5 na milioni 50 pamoja na kifungo cha miaka miwili jela.

Kwa upande wa wauzaji kanuni zinasema kuwa faini isiyopungua Sh. 100,000 hadi 500,000 pamoja na kifungo cha miezi 3 jela. Kwa watumiaji ni kiasi cha shilingi 30,000 hadi 200,000 na kifungo kischozidi siku saba

Awali Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, ilitoa tangazo na maelekezo ya matumizi ya mifuko mbadala inayoruhusiwa na kutoa miongozo ya nini cha kufanya katika kutekeleza upigaji marufuku mifuko ya plastiki kwa kuwataka wananchi kuikusanya na kuipeleka kwenye maeneo yaliyobainishwa.

Upande wao Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) imesema walishatoa taarifa inayokwenda kwenye vituo vyote vya kimataifa, kuhusu mwisho wa matumizi ya mifuko ya plastiki na kuanza rasmi katazo hilo leo.

Mkurugenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA), Paul Rwegasha, alisema kupitia TAA taarifa za katazo hilo zimeshatolewa. "Hii taarifa inajulikana kitaalamu kama 'timatic pre-information' ambayo inatumwa kwenye centre (vituo) zote duniani, ambapo kuna shirika la ndege ambalo linaleta abiria Tanzania itakuwa rahisi wao kupata taarifa ya katazo hilo na kuwafanya wasibebe mifuko hiyo," alisema Rwegasha.

# Museveni ammwagia sifa Mwalimu Nyerere

INATOKA UK. 5

kiuchumi kupitia kazi na michango zaidi aliyoitoa wakati wa uhai wake, na kwamba ikiwa bado kuna udhaifu mahali, wanapaswa kuelimishwa taratibu ili suala la mashahidi wa Uganda lieleweke na liwe na nguvu zaidi.

Ibada ya kumuombea marehemu Julius Nyerere iliongozwa na Kiongozi wa Kanisa la Kampala Charles Kasibante kwa niaba Askofu Mkuu Cyprian Lwanga, ambaye katika mahubiri yake amehimiza watu kuwa na imani thabiti kwa Mungu, amani katika mataifa na umoja ndani ya familia za waumini.

Alisema Juni Mosi pia ni siku maalumu ya kuwakumbuka mashahidi wa Uganda, akamshukuru mama Maria na mahujaji kutoka Tanzania kwa kutambua umuhimu wa siku hiyo na kuongeza kuwa ushiriki wao unaleta kumbukumbu za Mwalimu Nyerere wakati wa uhai wake.

Siku ya Nyerere huadhimishwa Juni Mosi kabla ya Maadhimisho ya Siku ya Mashahidi wa Uganda ambayo huadhimishwa Juni 3, kila mwaka, huku ikisherehekewa na madhehebu ya Kianglikana na Kikatoliki.

Kiongozi huyo wa kanisa aliitaka serikali kuhakikisha eneo linapofanyikia ibada hiyo ulinzi uimarishwe kama sehemu ya mchango wa serikali kwa maendeleo ya kanisa.

Rais Museveni aliwashukuru Waganda kwa kutambua umuhimu wa siku ya kumuombea Mwalimu Nyerere na kuungana na familia ya Mama Nyerere katika kumuombea. "Nyerere alikuwa mzazi wetu anayeonekana katika kumbukumbu zetu kama mtu aliyejitoa kwa kristo.

"Kwa karibu miaka milioni 4.5 iliyopita, Mataifa ya Magharibi yalilibatiza Bara la Afrika kuwa kipindi cha giza Afrika, hakuna Mwafrika aliyepigania umoja na uhuru kama Mwalimu Nyerere, kwa sisi Waganda, tunafurahi na kushukuru sana, " alisema.

Naye Balozi wa Tanzania nchini Uganda, Dk. Aziz Ponary Mima, aliwathibitishia wanahija waliohudhuria ibada ya kumuombea Mwalimu Nyerere, kuwa alikuwa mwanamapinduzi aliyepambana ili kuhakikisha utu, demokrasia na uhuru unapatikana kwa mataifa yote ya Afrika na mapambano hayo yamekuwa msingi mkubwa kwa nchi za Afrika mpaka sasa.

Naye Profesa Mark Mwandosya ambaye aliwahi kushika nyadhifa mbalimbali wakati wa uongozi wa Nyerere ukiwamo uwaziri, aliwashukuru wananchi wa Uganda na hasa Rais Museveni ambaye alifanya kazi na Mwalimu Nyerere, kwa kuthamini mchango wa Nyerere na kuahidi kuendelea kumuombea Baba wa Taifa mpaka Mungu asikie maombi yao.

Mwakilishi wa familia ya Nyerere, Anna Nyerere alimshukuru Rais Museveni kuwasaidia na kuhakikisha kwamba Siku ya Nyerere inatambulika nchini kwake na inafanyika kwa amani utulivu mkubwa kwa kipindi chote tangu mwaka 2007.

Nacho Chuo cha Stella Maris kilichoko, Wilaya ya Buikwe ambako Mama Maria Nyerere alisomea, pia walijumuika na ujumbe wa Watanzania kuombea mchakato wa kumfanya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere kuwa mtakatifu, imeanzisha ujenzi wa maktaba yatakayobeba jina la Mama Maria Nyerere.

# Serikali yakiri changamoto kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imekiri uwapo wa changamoto nyingi zinazoikabili sekta ya kilimo na kuifanya sekta hiyo muhimu kwa uchumi wa nchi kushindwa kufanya vizuri, licha ya uwapo wa hali ya hewa nzuri zaidi kwa kilimo, uvuvi na ufugaji ukilinganisha na nchi zingine za Afrika Mashariki.

Miongoni mwa changamoto hizo zilizobainishwa na serikali ni masoko, usindikaji, miundombinu ya umwagiliaji na miundombinu mingine kwa ajili ya mifugo na uvuvi, upatikanaji wa pembejeo bora kwa wakati na kwa bei nafuu, uhaba wa maofisa ugani, kero za tozo mbalimbali na mwingiliano wa taasisi za udhibiti.

Hayo yameelezwa mkoani Morogoro na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Mathew Mtigumwe, katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na mkurugenzi msaidizi wa sera na mipango wa wizara hiyo, Osward Ruboha, wakati wa ufunguzi wa mkutano wa wadau wa sekta ya kilimo ulioandaliwa na Baraza la Kilimo Tanzania ili kujadili mchango wa sekta binafsi katika utekelezaji wa mpango wa kuendeleza kilimo nchini ASDP II.

'Serikali itaendelea kufanyia kazi changamoto za uuzaji wa mazao yetu hasa nje ya nchi, wizara yangu kwa kushirikiana na AGRA na ESRF imeshazindua mradi maalum unaohusisha utafiti utakaopelekea kuwekwa mifumo imara ya ukusanyaji wa taarifa na biashara ya mazao ya chakula ndani na nje ya nchi, ili kuondokana na mazuio ya mara kwa mara ya uuzaji wa chakula nchi ya nchi," alisema Mtigumwe.

"Serikali itaendelea kuboresha mifumo ya upatikanaji wa pembejeo bora kwa wakulima, wavuvi na wafugaji kwa bei rahisi, ingawa kwa sasa tumeanza na mbolea ambapo tumekwisha kutoa kodi na tozo ili ipatikane kwa bei nafuu na sasa tumesalia na changamoto ya gharama kubwa za usafirishaji hasa kwa maeneo ambayo hakuna usafiri wa reli, lakini bado serikali nalo hili inalifanyia kazi," alisisitiza.

Kuhusu ASDP I, alisema moja ya changamoto iliyojitokeza wakati wa utekelezaji wake ilikuwa ni kutoshirikishwa kwa kiasi kikubwa kwa sekta binafsi, jambo lililosababisha kudorora kiutekelezaji, na kuwa katika ASDP II wametoa fursa zaidi kwa sekta binafsi, ambapo zaidi ya asilimia 60 ya utekelezaji wake unategemewa kutoka sekta hiyo, hivyo aliwataka kuhakikisha wanauelewa vema mpango huo ili kujipanga katika utekelezaji.

Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Kilimo Tanzania, Jacqueline Mkindi, alisema tangu kuanzishwa kwa baraza hilo ambalo ndilo taasisi kilele cha sekta ya kilimo, kumekuwa na mafanikio mengi ambayo ni ushiriki wake kikamilifu katika uanzishwaji wa Benki ya Kilimo Tanzania TADB, SAGCOT pamoja na ushiriki wake kikamilifu katika uandaaji wa mpango wa kilimo kwanza.

Akizungumzia ASDP II, Mratibu wa mpango huo, Innocent Muyengi, alisema serikali iliamua kuja na mpango huo kwa sababu sekta hiyo ni muhimu ambapo asilimia 25.7 ya pato la taifa linategemea kilimo, asilimia 30 ya mazao ya bidhaa za Tanzania zinazopelekwa nje zinategemea kilimo, huku pia asilimia 65 ya malighafi ya viwanda ikitegemewa kutoka kwenye sekta ya kilimo inatoka kwenye kilimo.

"Serikali imeshaonyesha nia, kwa kushirikiana na Baraza la Kilimo imeweza kufuta baadhi ya tozo mbalimbali kwenye tumbaku, sukari, chai, kahawa, mbegu na nyingine nyingi kwa hiyo kilimo ni eneo muhimu ambalo serikali imedhamiria kufanya kazi na sekta binafsi katika kufanikisha mpango huu," alisema.

Wakichangia katika mjadala huo wa wadau wa sekta binafsi katika kilimo walionyesha utayari wao wa kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika kufanikisha mpango huo wa kuendeleza kilimo nchini na kusema ni muhimu sasa maamuzi yanayofanywa na watunga sera yakazingatia hali halisi ilivyo katika sekta ya kilimo.

Makamo Mwenyekiti wa Baraza la Kilimo Tanzania, Jitu Son, aliitaka Tamisemi kuona namna itakavyowarekebisha maofisa ugani katika ngazi ya kata na vijiji kwani wamekuwa hawafanyi kazi inavyostahili licha ya uchache wao.



Baadhi ya wakazi wa kijiji cha Buanga, Musoma Vijijini, mkoani Mara, wakisomba mchanga juzi, kwa ajili ya ujenzi wa shule ya awali ili kuwapunguzia watoto wao kutembea umbali mrefu kufuata elimu katika shule kijiji cha Bwenda iliopo umbali wa kilometa tano. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Sababu viongozi kupokelewa kwa mabango hii

**Na Dege Masoli,** TANGA

MEYA wa Jiji la Tanga, Mhina Mustaph, ametoboa siri ya viongozi wa kitaifa wanaopokelewa kwa mabango wanapofanya ziara maeneo mbalimbali nchini kwamba ni dalili tosha kuwa waliyopewa dhamana ya kusimamia wananchi sehemu husika wamekosa usikivu na unyenyekevu kwa wanaowahudumia.

Hayo aliyaeleza mwishoni mwa wiki kwenye kikao Chama cha Wasafirishaji wa Abiria Tanzania (Taboa) Mkoa wa Tanga.

Mustaph ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye kikao hicho, alieleza kuwa tabia ya baadhi ya viongozi kukosa unyenyekevu na usikivu kwa wananchi ni changamoto kubwa na kwamba haitatokea siku viongozi wa kitaifa kutokaribishwa na mabango ya malalamiko maeneo yenye viongozi wa aina hiyo. Alisema tatizo ni kwamba waliyopewa mamlaka ya uongozi hawana fikra kwamba cheo ni dhamana ambayo kuna siku kitaondoka na wao watakuwa wananchi wa kawaida.

Kuhusu sakata la agizo la kutaka kufungwa ofisi za kukatisha tiketi katikati ya jiji, aliwataka wamiliki hao kupitia chama chao kumuachia suala hilo ili aweze kukutana na mamlaka husika kwa ajili ya maamuzi ili kulitatua bila kuathiri upande wowote.

Aliutaka uongozi wa Taboa kuvuta subira ili kumpa nafasi ya kuandaa kikao cha pamoja baina ya chama hicho, Sumatra na Jeshi la Polisi ili kulijadili upya kwa kuzingatia sababu za msingi na athari zinazoweza kujitokeza wakati wa kuitekeleza amri hiyo.

Mwenyekiti wa Taboa Mkoa wa Tanga, Abd Awadh, alimweleza mstahiki meya kuwa pamoja na mambo mengine, chama hicho kimekutana kujadili kero inayotokana na amri ya jiji hilo ya kuwapa siku 14 wasafirishaji kuzihamisha ofisi za kukatia tiketi zilizopo katikati ya mji.

## Wajasiriamali waomba msaada

**Na George Tarimo,** IRINGA

KUTOKANA na changamoto ya ajira, baadhi ya wajasiriamali wadogo mkoani Iringa wameishauri serikali na wadau kuweka utaratibu maalumu wa kuwasaidia watu wanaoanzisha biashara wakiwa na mitaji midogo ili kupunguza changamoto hiyo.

Ushauri huo ulitolewa mjini hapa na baadhi ya vijana wajasiriamali mkoani hapa akiwamo kwenye makabidhiano ya vifaa vya uchakataji mazao kwa lengo la kuongeza thamani ili kuingiza sokoni bidhaa zitokanazo na mazao hayo.

Johari Kasuke alisema alikuwa na mashine moja ya kusagisha juisi, lakini tangawizi alikuwa akipeleka kwenye mashine za watu na changamoto aliyokuwa anakumbana nayo kwenye mashine ni wale wahudumu wa mashine wanamwelekeza hawawezi kusagisha kitu kingine tofauti na mahindi.

Alisema baada ya kupata mashine hiyo ana uhakika atarudisha wateja wake wote ambao wameondoka kutokana na kukosa bidhaa kwa muda mrefu.

Ugawaji wa vifaa hivyo ni matokeo ya mradi wa kuinua vijana kupitia Feed the Future unaosimamiwa na Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO), ambapo Ofisa Uendelezaji Biashara wa shirika hilo mkoa wa Iringa, Nico Mahinya, alisema huo ni mwanzo wa kuibua vijana wajasiriamali kwa lengo la kuwawezesha kujiajiri.

Mahinya alisema kuwa wao kama Sido wamewezesha vijana kuanzisha shughuli za kijasiriamali, kulingana na sera yao wameanzisha viwanda vidogo vidogo.

Alisema kuwa sera yao ya ujasiriamali ya mwaka 2002 inatambua mti mmoja mwenye mtaji kuanzia shilingi moja hadi milioni tano anayefanya shughuli za uzalishaji kwa lengo la kuuza na kupata faida kwamba ni kiwanda kidogo.

Akikabidhi vifaa hivyo ikiwamo mashine ya kuchakata zao la muhogo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Robert Masunya, aliwataka vijana hao wapatao 40 kuwa mabalozi wazuri kwa kuonyesha uwezo wa kusimamia shughuli walizobuni ili kuinua pato lao na kuchangia pato la taifa pia.

# TARI yaanzisha mikakati kuongeza uzalishaji miwa

**Na Ashton Balaigwa,** KIBAHA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (TARI Kibaha) iliyopo mkoani Pwani, imeanza mkakati wa kuhakikisha inaongeza uzalishaji wa sukari kwa kuanza kuzalisha mbegu za teknolojia ya kisasa ambazo zitaleta tija kwa maendeleo ya uchumi wa viwanda.

Kupitia mkakati huo, tayari TARI Kibaha kupitia watafiti wake wamefanya ugunduzi wa aina saba za mbegu ya miwa ikiwamo N19,N25,N25, N30, N30, N41,R70,R75,na R79 ambazo zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Akizungumza katika Maadhimisho ya Siku ya Mkulima yaliyoenda sambamba na kuonyesha teknolojia hizo za mbegu ya miwa na mazao ya mizizi, Meneja wa TARI Kibaha, Dk. Hildelitha Msita, amesema mbegu hizo zina uwezo wa kutoa mavuno kuanzia tani 60-160 kwa hekta moja.

Dk. Msita alisema kuwa pia TARI Kibaha tayari imeanza majaribio ya aina nane za mbegu zinazostahimili ukame ambayo yanafanyika katika maeneo mbalimbali nchini yanayozalisha miwa ikiwamo Bonde la Kilombero, Ruhembe, Kagera, Mtibwa na TPC Moshi na katika mbegu hizo aina mbili zimeonyesha matokeo chanya.

Alisema wameanzisha kitalu chenye zaidi ya aina 279 za mbegu za miwa zikiwamo 41 za kienyeji kwa ajili ya kufanyiwa utafiti wa mbegu bora zinazostahimili mazingira ya hapa nchini ili kusaidia uzalishaji wa sukari kuongezeka.

Akizungumzia kuhusu mazao ya mizizi ikiwamo mihogo na viazi vitamu, alisema wamefanikiwa kugundua jumla ya aina 17 za mbegu ya mihogo zinazostahimili ukame na aina 12 za mbegu za viazi vitamu na zimethibitishwa kitaifa.

Naye Mratibu wa Kitaifa wa zao la miwa, Dk. Nessie Luambano, alisema wamefanikiwa kutoa mafunzo kupitia mashamba darasa na mashamba ya mifano, ili kutoa elimu bora kuhusiana na mbinu bora za kilimo cha miwa.

Dk. Luambano alisema kuwa wakulima wamesaidiwa kwa kufanya utafiti wa chanzo cha magugu tishio aina ya kiduha katika mabonde yote yanayolimwa miwa pia wanaendelea na uchunguzi wa wadudu na magonjwa yanayoshambulia miwa.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Wadau wa Sukari nchini, Dk. George Mlingwa, alisema kuwa wakulima wa miwa hapa nchini wana changamoto kubwa ikiwamo ya uchakavu wa miundombinu ya kuingia mashambani licha ya kukatwa kodi kubwa kwenye halmashauri husika.

"Ili ng'ombe umkamue vizuri maziwa lazima umlishe chakula, sasa wakulima wanakatwa kodi kwenye halmashauri zote zinazolima miwa, lakini tukiwaambia watutengenezee miundombinu ya barabara zinazoingia kwenye mashamba hawafanyi hivyo," alisema Dk. Mlingwa.




Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Evodi Mmanda, akizungumza na wageni waalikwa pamoja na wateja wa Benki ya Exim mkoani Mtwara, waliohudhuria hafla ya futari iliyoandaliwa kwa ajili ya wateja wa benki hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki zatakiwa kuchangamkia biashara ya bima

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI zimetakiwa kuchangamkia fursa ya sasa ambayo inazipa uwezo wa kuuza huduma za bima nchi nzima kupitia utaratibu mpya wa Bancassurance.

Ushauri huo ulitolewa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Bima ya Reliance ya Jijini Dar es Salaam, Ravi Shankar, wakati wa hafla ya Iftar iliyoandaliwa na kampuni yake kwa wateja wake na wabia mbalimbali.

Kauli yake imekuja kufuatia uzinduzi wa kanuni za kusambaza bima kwa kupitia benki (Bacassurance), ambazo zilizinduliwa hivi karibuni na Mamlaka ya Uthibiti wa Huduma za Bima Tanzania (TIRA), huku akisema huduma za bima zitasambaa kwa kasi na kwa bei nafuu kwa wananchi.

"Tumejiandaa vizuri kwa utaratibu huu wa Bancassurance na tunaomba benki zichangamkie fursa hii, ili wananchi wengi zaidi wapate huduma hii ya bima. Inawezeka tusiwe na matawi kote nchini, lakini uwepo wetu sasa utakuwapo kwa kupitia benki," alisema Shankar.

Alisema wamejiandaa na bidhaa aina mbalimbali katika soko na wanaimani kupitia utaratibu wa Bancassurance asilimia kubwa ya Watanzania ambayo haijafikiwa na huduma ya bima sasa itaweza kuhudumiwa.

Kwa mujibu wa Shankar, Watanzania wanatakiwa kuondokana na dhana kuwa bima ni kwa watu fulani tu, huku akisisitiza kuwa bidhaa za Reliance Insurance zinakidhi matakwa ya kila Mtanzania.

Naye Naibu Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo, Rukia Goronga, alisisitiza kuwa kampuni yao imejiandaa vizuri kushirikiana na benki mbalimbali kuhakikisha azma hii inafikiwa kwani huduma hii ya bima bado haijawafikia watu wengi.

"Tumekuwapo sokoni kwa zaidi ya miaka 20 sasa, kwa hivyo tunaelewa mahitaji ya wateja na kwa kweli asilimia kubwa ya wananchi hawajafikiwa na huduma ya bima ila tuna imani kuwa utaratibu mpya wa Bancassurance sasa utasaidia kuwafikia watu wengi zaidi," alisema.

Alisema wataendelea kutoa elimu kuhusu bima na hasa utaratibu huu, ili Watanzania wengi zaidi waelewe na hatimaye kukata bima.

Hafla hiyo ya Iftar ilifanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa sekta ya bima zikiwamo benki.

# Tigo yazindua ofa mpya 'Saizi Yako'

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Tigo imezindua ofa mpya ya 'Saizi Yako' inayolenga kuwapatia huduma za intaneti, muda wa maongezi na SMS kutokana na mahitaji mahusus ya kila mteja kwa gharama nafuu.

Ofa hii ya 'Saizi Yako' ni ya kipekee sana kwa sababu inawapatia wateja huduma ambazo ni mahusus kwa kila mteja, hivyo kuwaridhisha wateja wa sasa na wa baadaye wakiangalia gharama wanayoitumia kulinganisha na huduma wanayoipata. Ofa hii pia inapatikana kupitia menyu iliyorahisishwa ili wateja waweze kuipata na kuinunua kwa urahisi.

Akizungumza na waandishi wa habari katika uzinduzi wa ofa hii kutoka makao makuu ya Tigo, Dar es Salaam, Ofisa Biashara Mkuu wa Tigo, Tarik Boudiaf, alisema kwamba lengo la kampuni hiyo ni kutoa ofa bora, zenye mahitaji yote ya mteja sehemu moja, kwa gharama nafuu, na zitakazo kidhi mapendekezo na mahitaji ya wateja wao.

"Tumezingatia tabia, mahitaji na mienendo ya wateja wetu kwa miaka mingi sasa. Na kinachotufanya tuwe wabunifu ni kwamba tunatambua kwamba kila mteja wetu ni wa kipekee. Hivyo, tumeamua kubuni ofa hii ya 'Saizi Yako' ambayo ina mahitaji yote ya mteja sehemu moja na inayozingatia mahitaji yao mahusus. Sasa tunatoa fursa kwa wateja wetu kuweza kupata ofa za kipekee kwa kuzingatia matumizi yao ya kila siku na kwa gharama nafuu," alisema Boudiaf.

Boudiaf pia alieleza kwamba, kama mteja anatumia muda wa maongezi zaidi kuliko intaneti na SMS, basi atapata kifurushi bora cha muda wa maongezi. Na mteja akitumia zaidi intaneti kuliko muda wa maongezi na SMS, mteja huyo atazawadiwa kifurushi bora cha intaneti. Utaratibu huo huo utafuatwa pia kwa ajili ya SMS.

"Tunaamini kwamba 'Saizi Yako' itaendana na mahitaji, bajeti na maisha ya wateja wetu, kuwapatia ofa ambayo wataweza kupata kila wanachohitaji sehemu moja, kwa ajili yao, pia inamaanisha kwamba, sisi kama Tigo, tunatambua na kufanyia kazi mahitaji ya wateja wetu yanayobadilika kila siku. Uelewa wetu wa wateja pia unajenga uhusiano wetu nao na kuwafanya watuthamini zaidi," aliongeza Boudiaf.

# Serikali yapongezwa punguzo kodi taulo za kike

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la World Vision Tanzania, limepongeza serikali kwa kutoa punguzo la kodi (VAT) kwenye taulo za kike na kuomba watengenezaji pamoja na wasambazaji wa bidhaa hizo kupunguza bei, ili ziwafikie walengwa kwa bei nafuu.

Akizungumza mwishoni mwa wiki mtaalamu wa afya na usafi wa mazingira kutoka shirika hilo makao makuu nchini, Rose Riwa wakati alipokuwa katika maadhimisho ya Siku ya Hedhi Salama Duniani yaliofanyika Wilaya ya Karatu katika kijiji cha Endabash, alisema ni muhimu kwa wadau kutoa bidhaa hizo kwa bei nafuu ili maskini wamudu kununua na kuhifadhi mazingira.

Alisema anapongeza serikali kukataza matumizi ya mifuko ya Rambo kwa sababu ilikuwa ikitumika kama njia mbadala ya kuhifadhia na kufungia pedi zilizokwisha tumika na kutupwa ovyo.

"Kwa kufanya hivyo ilikuwa hatari kwa afya na mazingira pia, hivyo tunashauri wasichana kutumia njia mbadala ya karatasi katika kuhifadhi na kufungia pedi zilizokwishatumika na kuepuka kuzitupa ovyo," alisema.

Rose aliomba watengenezaji na wasambazaji wa pedi kuhakikisha wanakuwa na vifungashio maalumu vinavyokidhi haja za kimazingira na kuepuka kutumia nailoni ambazo sio rafiki kwa mazingira.

Aidha, katika kuhakikisha mtoto wa kike na jamii inayomzunguka inakuwa salama, World Vision Endabash na Eyasi kupitia miradi ya maji, usafi na siha (WASH) imefikia jamii, shule na vituo vya kutolea huduma za afya kwa kuchimba, kusambaza maji, kujenga matangi ya kuvunia maji, pamoja na kujenga vyoo vinavyochangia hedhi salama.

"Kupitia huduma hizi watu zaidi ya 24,193 kutoka vijiji 32, Endabash 21 na Eyasi 11 vilivyopo Tarafa za Endabash na Eyasi wamenufaika.

Alifafanua kuwa kwa kushirikiana na serikali, shirika hilo wamejenga miundombinu ya maji kwenye vituo 36 na vimekamilika, huku vituo vingine 15 vikiendelea katika vijiji vya Ayalaliyo, Ngaibara na Umbaungw na zaidi ya Sh. milioni 920 zimetumika kutekeleza miradi hiyo.

Pia wamejenga matundu 20 ya vyoo kwenye Shule ya Msingi Endabash, Buger, Umbaungw na matundu manane kwenye shule za sekondari ya Endabash na Qaru, yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 88.

Alisema vyoo hivyo vina vyumba maalum kwa ajili ya wasichana wanapokuwa katika hedhi na kuwahakikishia usalama wa afya zao.


"Katika kipindi cha miezi mitatu ijayo tutaongeza idadi ya matundu manane ya vyoo kwenye shule za sekondari Marang' na Baray, matundu manne kwa ajili ya wasichana," alisema.

Alisema katika Tarafa ya Eyasi wamejenga matundu ya vyoo 20 kwenye Shule ya Msingi Mbuganyekundu, Mang"ola Nt, na Eyasi pia matundu manane yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 106 na vyote vina vyumba maalum vya wasichana wanapokuwa katika hedhi.

Pia wamejenga vituo vinne vya kunawia mikono kwa ajili ya wanafunzi katika shule za msingi Shangit na Ayalaliyo vyenye zaidi ya Sh. milioni 15 na wanafunzi 1,257 watanufaika na ujenzi huo.

Alisema katika Tarafa ya Eyasi wamejenga vituo vitano vya kunawia mikono kwa ajili ya wanafunzi wa shule ya Dumbechand, Mbunganyekundu, Mang'ola Nt, Murus na Mbuyuni vyenye thamani ya Sh. milioni 37 na wanafunzi 3,415 watanufaika na mradi huo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Theresia Mahongo, alipongeza shirika hilo kwa jitihada zake za kuunga mkono serikali na kuomba watoto wa kike kutunza vyoo kama walivyokabidhiwa ili wasipate maambukizi na kuepukana na magonjwa ya mlipuko.




Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Mhandisi Zephania Chaula (kushoto), akishikana mkono na mwenyekiti wa watu wenye ulemavu wa Mirerani, William Orata na kukabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 230.8 kwa vikundi 71 vya wanawake, vijana na wenye ulemavu waliopatiwa mikopo na halmashauri ya wilaya hiyo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Viongozi wa dini waombwa kuombea amani taifa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

VIONGOZI wa dini nchini wameombwa kuombea amani taifa, watu na viongozi wake ili waweze kuishi kwa upendo na kudumisha amani iliyopo tangu Uhuru.

Wito huo umetolewa na Diwani wa Kata ya Ngarenaro jijini Arusha, Isaya Doita, alipokuwa akizindua upandaji miti katika Zawiya Kuu ya Msikiti wa Zawiyatull Qadiriyyat iliopo Ngarenaro na kusisitiza watu kujituma katika kufanya kazi na majukumu mbalimbali yanayowakabili.

Doita alisema pamoja na kuwaombea viongozi, pia wanapaswa kuwakosoa na kuwausia viongozi wote ili wawe na maadili mema katika utendaji wao wa kazi za kuhudumia jamii na kuepukana na ile tabia ya ubinafsi.

Alisema anawaheshimu viongozi wa dini zote nchini na nje ya nchi na yupo tayari kwa kila kazi atakayoitwa kuifanya na viongozi wa dini yoyote.

Awali Mwenyekiti wa mkoa, Abdi Omar, alimkaribisha mlezi wa Zawiya zote nchini, ambaye pia ndiye Mwenyekiti wa Taifa, Salum Mubarak Darwesh, kuwaasa watu wote kuishi vema na wenzao wakiwa na tabia njema ambayo ndiyo silaha kwa kila jambo.

Mwenyekiti wa Mkoa wa Arusha wa Zawiya hiyo, Abdi Omar, alisema wanaungana na serikali kutunza na kuboresha mazingira ili kuifanya Arusha iwe ya kijani.

Alisema Mkoa wa Arusha una zaidi ya Zawia 30 na kila moja wamepanga kuotesha miti 3,000, ili kuboresha mazingira na kuhakikisha wanapunguza mmomonyoko wa ardhi husussan kando ya mito.

Aliongeza kuwa katika kufanikisha lengo hilo, taasisi hiyo ilipata ufadhili kutoka Shirika la Hifadhi ya Taifa (Tanapa), ambalo liliwachangia Sh. milioni 10 na kusisitiza kuwa upandaji miti ni endelevu nchi nzima na wanatarajia kupanda zaidi ya milioni tano.

# Wananchi waaswa kusaidia wahitaji

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WANANCHI nchini wametakiwa kujitolea kuyasaidia makundi yenye uhitaji maalumu ili kujiongezea baraka na thawabu mbele ya Mwenyezi Mungu hasa katika kipindi hiki cha mwisho wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Wito huo umetolewa na Mratibu wa kikundi cha Who is Hussain, kilichopo jijini Arusha, kinachojihusisha na kusaidia jamii ya watu wenye mahitaji maalumu wakiwamo watoto yatima na waliozalishwa katika umri mdogo.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya kushiriki futari ya jioni na watu wenye mahitaji maalumu, Mratibu wa kikundi cha Who is Hussein, Tehara Abbas, alisema waliamua kushiriki katika hafla hiyo kwa lengo la kutoa sadaka kwa watu wenye mahitaji maalumu.

Alisema hafla hiyo, iliwalenga watu wenye ualbino, pamoja na zaidi ya wasichana 20, waliozalishwa katika umri mdogo wanaolelewa katika kituo cha Faraja kilichopo jijini Arusha.

Abbas alisema, wapo watu kwenye jamii wamebarikiwa kuwa na uwezo, lakini hawakumbuki kuwasaidia watu wenye mahitaji muhimu, jambo ambalo siyo sahihi mbele za Mwenyezi Mungu.

"Katika maisha ya kawaida hakuna mtu asiyekuwa na kitu cha kutoa hata kama ni kidogo ni vyema ukatoa ili ushirikiane na wenzako kwa kuwa kwa kufanya hivyo, utajiongezea baraka na kudumisha umoja na mshikamano katika jamii," alisema Tahera.

Hata hivyo, alisema mwezi wa Ramadhani ni mwezi wa toba kwa Waislamu wote duniani, hivyo, aliwataka kujisogeza mbele za Mungu kwa kufanya ibada mbalimbali ili wavune thawabu.

"Ni dhahiri kipindi hiki cha mfungo wa Ramadhani kuna mabadiliko mengi katika mfumo wa maisha na matendo ya watu," alisema Tahera.

Aidha, alisema zaidi ya wasichana 20, waliozalishwa katika umri mdogo pamoja na watu wenye mahitaji maalumu, walipata fursa ya kupata mafunzo ya kukabiliana na ugumu wa maisha pindi wanapohitimu masomo.

Aliwataka wasichana hao, kusahau changamoto walizopitia wakati walipozalishwa na aliwapa moyo ili na wao waweze kuwa msaada kwa watu wengine wanaopitia katika hali kama hiyo.





# Madiwani wasikitishwa maazimio yao kupuuzwa

**Na Godfrey Mushi,** HAI

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro limeeleza kusikitishwa na baadhi ya maazimio wanayoyaweka katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwamo uimarishaji wa masoko na usafi wa mazingira kutozingatiwa na watendaji.

Moja ya maazimio wanayolalamikia kutotekelezwa hadi sasa ni pamoja na uzoaji wa takataka katika masoko ya walaji ya Kwa Sadala na Mula ambayo yamekuwa yakihudumia wananchi na wafanyabiashara kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Madiwani walitoa malalamiko hayo mwishoni mwa wiki, wakati wa kikao cha kawaida cha baraza hilo. Aliyeibua malalamiko hayo ni Diwani wa Viti Maalum (Chadema), Mwantumu Msangi, aliyetaka kujua watendaji wa halmashauri hiyo ni kwa nini wasijieleze au kuchukuliwa hatua za kinidhamu kutokana na kushindwa kusimamia zoezi la uondoaji wa taka katika masoko ya Kwa Sadala na Mula.

Kwa mujibu wa Msangi, masoko hayo kwa sasa yanakabiliwa na mrundikano mkubwa wa takataka, hali ambayo inatishia afya za walaji pamoja na magonjwa ya mlipuko.

Alieleza: "Ni aibu kwa sababu huko Dar es Salaam tayari ugonjwa wa kipindupindu umeshaibuka na sisi bado tumelala, hatuzingatii maelekezo ya baraza, sasa natake kujua ni njia gani itumike kuzoa taka hizo, ili kuwaepusha wafanyabiashara na magonjwa ya mlipuko hususani kipindupindu kama ulivyotokea katika mkoa wa Dar es Salaam." Baada ya swali hilo, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Helga Mchovu, aliunga mkono hoja hiyo, akisema katika masoko hayo hasa la Kwa Sadala, kwa muda mrefu walikubaliana kwamba halmashauri imwage changarawe za moramu ili kupunguza tope na kuzoa taka hasa kipindi cha mvua, lakini hakuna utekelezaji wake.

"Mnaona na jinsi gani tunavyoweka maazimio ya kutatua matatizo, lakini hayafanyiwi kazi, takataka zimerundikana katika haya masoko, changarawe za moramu hazijawekwa, tunapuuza hata vitu vya msingi na sijui nia ni nini, nadhani tunataka kuwaletea magonjwa wananchi wetu," alisema Mchovu.

Akijibu hoja hiyo ya madiwani, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Jackob Muhumba, alisema serikali imeliona suala hilo na inaangalia namna ya kulitafutia ufumbuzi na kwamba kuna utaratibu unaoandaliwa wa kudumu wa kufanya usafi kwenye masoko hayo.



Meneja Uhusiano wa Jamii Kampuni ya Songas, Nicodemus Chipakapaka (wanne kulia), akimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kisa Makori (kushoto), vifaa vya usafi vyenye thamani ya Sh. milioni 10 katika hafla fupi iliyofanyika katika viwanja vya Manzese Bakhresa, jijini Dar es Salaam, jana. Vifaa hivyo ni sehemu ya mchango wa kampuni hiyo ya kuhamasisha utunzaji na uhifadhi wa mazingira, hasa tukielekea katika maadhimisho ya Wiki ya Mazingira inayosherehekewa duniani kote kila Juni 6. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanesco yatangazia msamaha wadaiwa

**Na Paul William,** MOSHI

WATEJA wa Shirika la Umeme (Tanesco) mkoa wa Kilimanjaro, ambao wako katika wakati mgumu wa kuendelea ama kutoendelea kunufaika na huduma za nishati hiyo kutokana na kupaa kwa riba inayotokana na malimbikizo ya muda mrefu, wametangaziwa msamaha.

Msamaha huo umetangazwa na Meneja wa Tanesco mkoani hapa, Mhandisi Mahawa Mkaka.

Kwa mujibu wa Mhandisi huyo, ili kutoendelea kudaiwa au kukatishiwa huduma, ni lazima mteja husika afike katika ofisi zake na kutimiza masharti yaliyowekwa.

Mhandisi Mkaka alisema zoezi hilo la kukadiria deni la mteja limekuwa chachu ya baadhi ya wateja kuweza kulipa madeni yao.

Kutokana na msamaha huo, amewataka wale wote wenye madeni ya nyuma kufika katika ofisi za Tanesco ili kunufaika na msamaha huo wa riba.

"Tumeanzisha zoezi maalum kwa wateja wetu waliokuwa na madeni ya nyuma ambapo kwa sasa tumekuwa tukiwapa punguzo la msamaha wa riba lengo likiwa ni kuhakikisha tunajenga ukaribu zaidi na wateja ambapo mteja anapokamilisha masharti yanayoweka hupata punguzo hiyo," alisema.

Pia alizungumzia zoezi la ubadilishaji wa mita za zamani na kuwafungia wateja wote mita za luku na kudai kuwa zoezi hilo linaendelea na kuwataka wateja wote wenye mita za zamani kufika katika ofisi za shirika hilo kutoa taarifa ili waweze kubadilishiwa.

Alisema mita hizo za zamani sio rafiki kwa wateja pamoja na shirika kwa ujumla ambapo zinaweza kumuibia mteja na kulipa gharama kubwa ikilinganishwa na umeme anaoutumia au kuliibia shirika kwa kulipa gharama ndogo tofauti na matumizi yake.

"Nitoe wito kwa wateja wenye mita za umeme za zamani kutoa taarifa katika ofisi za shirika la umeme ili waweze kubadilishiwa mita hizo na kufungiwa mita za luku bure ambapo ndio mita rafiki kwa mteja pamoja na shirika kwani mteja utalipia kile unachokitumia," alisema Mhandisi Mkaka

# Msomi ashauri lugha ya kufundishia

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MWANDISHI mkongwe wa vitabu nchini, Prof. Mramba Nyindo, amesema bado kuna changamoto kubwa ya matumizi ya lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi wa vyuo vikuu, huku akiishauri serikali kuweka mkazo zaidi katika lugha ya kufundishia.

Alishauri kufanyika mabadiliko ya kimfumo katika lugha ya kufundishia, baadhi ya nchi za Afrika ikiwamo Afrika ya Kusini na Rwanda zimetangaza kuanza kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya taifa.

Alitoa maoni yake hayo jana, wakati Chuo Kikuu Kishiriki cha Tiba na Uuguzi cha Hospitali ya KCMC (KCMCo), kilipokuwa kikiadhimisha Siku ya Waandishi wa Vitabu.

Prof. Nyindo alisema kuwa hali hiyo inachangiwa na walimu wengi wanaofundisha masomo ya lugha, hususani Kingereza au Kiswahili hawakifahamu vizuri, hivyo kusababisha wanafunzi kutofahamu kabisa lugha hiyo.

"Ukiwatazama watunzi wa vitabu hivi, huchukua muda mrefu kujisomea ili waweze kubobea kwenye lugha, kwani walimu wengi hawaijui lugha vizuri hali inayopelekea wanafunzi nao kushindwa kuelewa wanachofundishwa na kupata maarifa ambayo yanaweza kuisaidia jamii. "Vitabu vilivyozinduliwa vinatoa mwanga kwa kijana kutokata tamaa, kutotaka mambo ya haraka haraka na kuwa mvumilivu kwa kila changamoto anayokabiliana nayo. Hili ndio lengo la taaluma hasa hasa."

Makamu Mkuu wa Chuo cha Tiba cha KCMCo (Taaluma), Prof. Mtata, akizungumza kwa niaba ya Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Ephata Kaoya, aliwataka wanafunzi wa chuoni hapo kizipenda lugha na kuzitumia ili wawe mfano bora wenye kuleta tija kwa jamii.

"Kwa niaba ya Makamu Mkuu wa Chuo, napenda kutangaza rasmi kila tarehe 31 Mei kila mwaka itakuwa siku ya waandishi wa vitabu chuoni hapa na itaadhimishwa kwa mujibu wa sheria za chuo hiki. Tunawaomba wanachuo kujikita katika kuandika majarida mbali mbali ya kitaalumu na mazingira wanayoishi ili kuleta mabadiliko katika jamii," alisema Prof. Mtata.

"Leo tunaadhimisha siku hii kichuo, lakini tuna mitazamo ya kuiadhimisha kwa wiki nzima ili kuwaonyesha watu nini tunafanya, wapi tumetoka na wapi tunaelekea ili kuhakikisha jamii inapata kitu tofauti kutoka hapa. Kunzia Mwezi Januari hadi Mei mwaka huu, tayari maandiko 46 yameshaandikwa na kuchapishwa, hii ni hatua nzuri ambayo italeta mafanikio kwa watunzi wetu wa vitabu," alieleza.

Moja ya waandishi wa vitabu waliopata fursa ya kuzinduliwa rasmi kwa vitabu vyao vya kitaaluma ni pamoja na Dk. Elichilia Shao aliyeandika kitabu cha 'Dream Make It Happen Live It'

Akizungumzia kitabu hicho, Dk. Shao alisema kimesheheni njia mbalimbali za mafanikio ikiwamo kujiamini, kumiliki ndoto kila unapokwama kusimama na kuanza tena bila kukata tamaa, kutunza muda wako wa kila siku na namna ya kumshirikisha Mungu kwa kila unachokifanya.

Alisema kuandika kitabu sio kazi ya siku moja, kwa vile ni lazima uwe tayari kupokea maoni, ushauri na kuufanyia kazi ikiwa ni pamoja na kukabiliana na changamoto zote unazokabiliana nazo wakati wa uwandishi.

"Leo kitabu changu cha tatu kinazinduliwa ambao kinayazungumzia maisha yangu na uhalisi wangu, napenda kuwatia moyo waandishi wote wa vitabu pamoja na vijana wote kutokata tamaa bali kusongambele licha ya changamoto wanazokabiliana nazo," alisema.

Nipashe
# Spotika
JUMATATU JUNI 3, 2019



MABEKI WAKUISAIDIA ARSENAL 2019/18 HAWA UK. 19




# MTOKEA BENCHI...

Mtokea benchi, Divock Origi (mwenye rasta) akipongezwa na wachezaji wenzake wa Liverpool baada ya kuizamisha Tottenham kwa kuifungia timu yake bao la pili, wakati wakishinda 2-0 kwenye mechi ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyopigwa Uwanja wa Wanda Metropolitano jijini Madrid juzi na kutwaa ndoo hiyo. **HABARI UK. 30**

## ISIKUPITE

Klopp amekuwa kocha wa nne Liverpool kutwaa ubingwa wa Ulaya, baada ya Bob Paisley, Joe Fagan na Rafael Benitez, huku kwa upande wa Ujerumani akiwa kocha wa tano kuweza kubeba ndoo hiyo, baada ya Dettmar Cramer, Jupp Heynckes, Ottmar Hitzfeld na Udo Lattek, lakini akiwa Mjerumani wa pili kutwaa taji hilo pasipo kikosi chake kujumuisha mchezaji kutoka Ujerumani (Heynckes pia aliwahi kufanya hivyo akiwa na Real Madrid).



# NI NINI KINAENDELEA KWA SOKA LA NEYMAR?




Neymar

**RIO DE JANEIRO, Brazil**

MAMBO sio shwari kwa Neymar, ndio unavyoweza kusema kwa sasa kuhusu nyota huyo wa kimataifa wa Brazil.

Wiki hii kanda ya video iliosambazwa katika mitandao ya kijamii ilimuonyesha mshambuliaji huyo wa Paris Saint-Germain mwenye thamani ya pauni milioni 200, akiwa katika mazoezi na Brazil kuelekea maandalizi ya Kombe la Mataifa ya Amerika Kusini, Copa America, yanayoanza mwezi huu, akichengwa na kinda wa Klabu ya Cruzeiro, Weverton.

Ni wazi kusema kuwa hakufurahia. Weverton mwenye umri wa miaka 19, aliorodheshwa katika kikosi cha Brazil na kocha, Tite kupata uzoefu, lakini akajikuta ameangushwa chini na Neymar baada ya kupitisha mpira katikati ya miguu ya mshambuliaji huyo wa PSG, maarufu kama kupigwa tobo.

Hatua hiyo ilijiri baada ya Neymar ambaye alikuwa amewasili katika kambi ya mazoezi ya Brazil na ndege ya aina yake yenye thamani ya pauni milioni 11.5 kupokonywa unahodha wa timu ya taifa baada ya misururu ya matokeo mabaya na nidhamu mbovu.

Mchezaji mwenzake pale PSG, Dani Alves alipewa uongozi wa timu hiyo badala yake. Alves alijiunga na PSG katika dirisha la uhamisho mwaka 2017 sawa na Neymar.

Mnamo Mei mwaka huu, Shirikisho la Soka nchini Ufaransa lilimpiga marufuku ya mechi tatu mchezaji huyo baada ya kumkemea shabiki, wakati timu yake ilipofungwa na Renes katika fainali ya Coupe de France.

Pia anadaiwa kuhusika katika mgogoro na mchezaji mwenza katika chumba cha kubadilishia baada ya PSG kufungwa na Montpellier.

Licha ya kuigharimu PSG dau la uhamisho lililovunja rekodi ya dunia misimu miwili iliyopita, hatima ya mchezaji huyo katika klabu hiyo imezua mjadala.

Neymar amekuwa akihusishwa mara kwa mara na uhamisho wa kurudi katika klabu yake ya zamani ya Barcelona ama hata kuanza ukurasa mpya na klabu ya 'Galacticoz' ya Real Madrid.

Mchezaji wa zamani wa Barca na Brazil, Rivaldo amependekeza kwamba Neymar angerudi katika klabu yake pale Nou Camp akimtaja kuwa kiungo kilichokosekana katika harakati za mkufunzi Ernesto Vaverde kutaka kushinda Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Tangu ashinde kombe hilo na Barca mwaka 2015, Neymar ameshindwa kujimudu katika michuano hiyo.

Aliondolewa katika awamu ya robo fainali na Barcelona mwaka 2016 na tangu alipowasili mjini Paris mwaka 2017, PSG imeshindwa mara mbili kuvuka robo fainali, ikishindwa na Real Madrid mwaka 2018 na Manchester United msimu huu uliomalizika Jumamosi iliyopita.

Ushindi huo wa Man United ulimuweka Neymar katika shida licha ya mchezaji huyo kushindwa kushiriki katika mechi hiyo kutokana na jeraha la mguu.

Neymar alimkosoa mwamuzi wa mchezo huo kwa kuipatia Man United penalti iliyojaa utata, akiutaja uamuzi huo kuwa ni wa aibu.

"Watu wanne ambao hawajui chochote kuhusu soka wanatazama penalti hiyo mbele ya runinga," aliandika katika ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Instagram kukosoa maamuzi yake.

"Sasa beki wa PSG, Presenel alitakiwa kufanya nini na mikono yake ambaye mgongo wake ulikuwa umegeuka? Alihoji katika mtandao wake wa Instagram.

**ATAFANYA NINI?**

Bado atasalia miongoni mwa wachezaji bora katika michuano ya Copa America mwezi huu, lakini mashabiki wa soka wanazidi kupoteza subira yao kutokana na vitendo vyake vya hivi karibuni.

Kuhusu iwapo ni wapi huenda Neymar akacheza soka lake baada ya michuano ya Copa America, haijulikani.

Lakini ni wazi kwamba, kuna uwezekano mkubwa akarudi kwa timu yake ya zamani ya Barcelona ambayo nayo imeonyesha nia ya wazi kutaka tena kumsajili, huku pia wapinzani wao wa soka la Hispania, Real Madrid wakiisaka saini yake.

## JE, WAJUA?

Chelsea ni timu ya kwanza kutwaa ubingwa wa michuano mikubwa ya Ulaya bila kupoteza mechi yoyote (ikishinda michezo 12 na sare tatu) tangu Manchester United ilipofanya hivyo msimu wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wa 2007-08.



# MICHEZO



# AZAM WALIVYOREJEA TENA KIMATAIFA

**Na Adam Fungamwango**

BAO la dakika ya 64 lililowekwa wavuni na Mzambia Obrey Chirwa limeiwezesha timu ya Azam FC kutwaa Kombe la FA na kupata tiketi ya kucheza Kombe la Shirikisho barani Afrika mwakani.

Ni bao lililokatisha ndoto za Lipuli ya Iringa ya kucheza michuano ya kimataifa kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa, hivyo kuifanya Azam kutoka na ushindi wa bao 1-0.

Fainali hiyo iliyokuwa kali na ya kusisimua muda wote wa dakika 90, ilichezwa kwenye Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi.

Mara ya mwisho kwa Azam kucheza mechi za kimataifa ilikuwa ni kwenye Kombe hilo la Shirikisho mwaka 2016 na kutolewa kwa jumla ya mabao 4-2 na Esperance ya Tunisia ambayo wiki hii imetwaa tena kwa mara ya pili Ubingwa wa Afrika, Ligi ya Mabingwa Afrika mara ya pili mfululizo.

Azam ilishinda mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Azam Complex, lakini ikaenda kukiona cha moto nchini Tunisia ilipochapwa mabao 3-0.

Hiyo ilikuwa ni raundi ya pili baada ya ile ya kwanza Azam kuisukumiza nje ya mashindano Bidvest Wits ya Afrika Kusini kwa jumla ya mabao 7-3.

Ilishinda mabao 3-0 nyumbani, ikashinda tena ugenini 4-3 kwenye raundi ya kwanza ndipo ilipokwenda kukutana na Esperance.

Hii ni mara ya kwanza kwa Azam kutwaa kombe hilo, lakini ilishawahi kutinga hatua ya fainali msimu wa 2015/16 ilipocheza fainali dhidi ya Yanga na kuchapwa mabao 3-1 yaliyopatikana kwa mikwaju ya penalti baada ya timu hizo kutoka dakika 90 bila kufungana.

Shirikisho la Soka nchini (TFF), liliirudisha tena michuano hiyo msimu wa 2015/16 ili bingwa wake ashiriki michuano ya kimataifa, Kombe la Shirikisho, ambayo Yanga ilikuwa bingwa kwa kuichapa Azam.

Msimu uliofuata 2016/17, Simba ilitwaa kombe hilo kwa kuifunga Mbao FC mabao 2-1 kwenye mechi ya fainali iliyochezwa Uwanja wa Jamhuri Dodoma na msimu uliopita 2017/18, Mtibwa Sugar ilifanikiwa kutwaa kombe hilo baada ya kuifunga Singida United mabao 3-2, mechi ikipigwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid mjini Arusha.

Azam FC haikutwaa ubingwa huo kirahisi, bali ilibidi ivuke mabonde na milima. Na hii ndiyo safari yao hadi kufika hapo.

**Azam FC 2-0 Pamba FC**

Ilianza kwenye raundi ya nne ya michuano hiyo iliyochezwa Januari 28 kwenye Uwanja wa Azam Complex ambapo ilifanikiwa kuichapa timu kongwe ya Pamba ya Mwanza mabao 2-0.

Mabao yote mawili kwenye mechi hiyo yalifungwa na winga wa zamani wa Simba, Ramadhani Singano 'Messi' dakika ya 18 na 53. Ushindi huo uliifanya Azam FC kutinga hatua ya 16-bora ya michuano hiyo.

**Azam FC 3-0 Rhino Ranger**

Azam ilifanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Kombe la FA kwenye mechi iliyochezwa Februari 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, wenyeji wakiifunga timu ya Rhino Ranger ya Tabora mabao 3-0.

Mzimbabwe Tafazwa Kutinyu alianza kuipatia Azam bao katika dakika ya 21, na mabao mengine yalitinga kipindi cha pili dakika ya 58 yakifungwa na Salum Aboubakar, na Obrey Chirwa akifunga bao la tatu dakika ya 69.

**Azam FC 1-0 Kagera Sugar**

Kiungo Joseph Mahundi alifanikiwa kuipeleka Azam FC hatua ya nusu fainali Machi 29 alipofunga bao pekee kwenye mechi ya robo fainali ya michuano hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

Mchezaji huyo alifunga bao hilo dakika ya 80, huku golikipa wake tegemeo Razak Abarola akionyeshwa kadi nyekundu dakika ya 68 baada ya kumchezea vibaya mchezaji wa Kagera Sugar. Ni ushindi ambao uliifanya timu hiyo kukutana na KMC.

**Azam FC 1-0 KMC**

Alikuwa ni Salum Aboubakar alipompenyezea mpira mrefu Nicolaus Wadada, aliyekimbia kwa kasi pembeni ya uwanja na kuwazidi mbio mabeki wawili wa KMC, kabla ya kuingiza majalo safi iliyomkuta Patrick Ngoma akaujaza wavuni na kuwa ni bao la pekee lililowapa ushindi na kutinga hatua ya fainali.

**Azam 1-0 Lipuli**

Chirwa ndiye aliamua matokeo ya mechi ya Jumamosi iliyopita na kuipeleka Azam kwenye michuano ya kimataifa mwakani, baada ya kupigwa mpira mrefu kutoka nyuma, akawa anashindana mbio na nguvu na beki Haruna Shamte wa Lipuli.

Straika huyo wa zamani wa Yanga, alimzidi ubavu Shamte ambaye mwishoni alianguka na kumpa urahisi kufunga bao pekee lililoamsha furaha kwa wachezaji, viongozi na mashabiki wa timu hiyo.

## NJE YA UWANJA

# SALAH WA PILI BAO LA MAPEMA FAINALI UEFA


BAO la kwanza alilofunga mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, wakati wakishinda 2-0 dhidi ya Tottenham katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumamosi, ni la pili kwa kuwa la mapema zaidi kuwahi kufungwa kwenye mechi ya fainali ya michuano hiyo (dakika ya 1:48).

Mpaka sasa bao linaloshikilia rekodi ya kuwa la mapema zaidi kwenye mechi za fainali za michuano hiyo ni la Paolo Maldini alilofunga sekunde ya 50 (00:50) tangu mechi ilipoanza aliloifungia AC Milan dhidi ya Liverpool mwaka 2005.

Bao la Salah lilitokana na Liverpool kuzawadiwa penalti sekunde ya 30 baada ya Sadio Mane kumnawisha mpira Moussa Sissoko ndani ya eneo la hatari na kisha kukwamishwa kimyani na Mmisri huyo baada ya dakika 1:48.

Kutoka bao hilo la Salah, linalofuata kwa kuwa la mapema zaidi ni la Gaizka Mendieta katika dakika ya tatu alipoifungia Valencia dhidi ya Bayern Munich mwaka 2001.

Kisha linafuata la Ivan Rakitic aliloifungia Barcelona mwaka 2015 dhidi ya Juventus, wakati pia mchezaji wa Bayern, Mario Basler akiungana naye kwa kufunga baada ya dakika sita dhidi ya Manchester United mwaka 1999.



# WACHEZAJI WA5 BORA EPL MSIMU WA 2018/19



Sadio Mane

**LONDON, England**

BAADA ya mechi 380 kwenye Ligi Kuu England, mwishowe bingwa wa England amepatikana. Zilikuwa mbio ngumu kati ya Manchester City na Liverpool, lakini mwisho wa siku, City wakajinyakulia kombe.

Manchester City walitawazwa kuwa mabingwa kwa mara ya nne katika historia ya Ligi hiyo tangu ilipofanyiwa marekebisho mwaka 1992. Na wametwaa kombe kwa mara ya pili mfululizo na imekuwa timu ya kwanza ya Uingereza kutwaa mataji matatu ya nchini humo mwaka huu.

Msimu huu ulishuhudia wachezaji wengi wakifanya vizuri na klabu zao na kuonyesha kiwango cha juu zaidi.

Majina machache yaliyozoeleka na yasiyozoeleka yalijitokeza msimu huu. Hapa tunawaangalia wachezaji watano bora kwa Ligi Kuu ya England msimu wa 2018/19, wakiwa wameorodhozeshwa kutokana na viwango vyao kwenye Ligi.

### 5. Bernardo Silva

Bernardo Silva alifanya watu wasimkumbuke Kevin de Bruyne msimu huu kwa kuonyesha kiwango cha juu.

Bernardo Silva alisajiliwa akitokea kule Monaco Mei mwaka 2017 kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni pauni milioni 43.

Huku Kevin de Bruyne akiwa ameonyesha kiwango cha juu zaidi msimu uliopita, Bernardo alikuwa na vitu vichache vya kufanya. Lakini De Bruyne akaingia kwenye matatizo ya majeraha msimu huu na Pep alihitaji kuziba pengo lake na Silva hakumwangusha.

Ingawa Silva kiwango chake hakikuwa kikubwa zaidi kama ilivyokuwa kwa Bruyne msimu uliiopita, lakini alionyesha umuhimu mkubwa kwa City kutwaa taji. Aliingia kwenye kikosi cha kwanza.

Katika kikosi cha wachezaji wa Guardiola, ni Aymeric Laporte tu ameanza kwenye mechi nyingi zaidi kuliko Silva, ambapo amecheza 34 dhidi ya 31 za Mhispania huyo.

Lakini Silva kuanzia benchi kumemfanya acheze katika mechi 36 za City kati ya 38 za Ligi Kuu. Ni golikipa Ederson pekee ametoa mchango mkubwa kwa kucheza mechi nyingi katika kutetea ubingwa.

Silva katika mechi 36 amefunga mabao saba na kutoa pasi za mwisho saba.

### 4. Sadio Mane

Liverpool inaweza kuwa imelikosa taji la Ligi Kuu kwa pointi moja, lakini bado ulikuwa msimu bora zaidi kwako kwa kufikisha pointi 97. Kulikuwa na wachezaji wachache walioonyesha mchango mkubwa kwa Liverpool na Sadio Mane kwa hakika alikuwa mmoja wao.

Mane, akiwa amefunga mabao 22 katika mechi 36, alishinda Kiatu cha Dhahabu msimu huu pamoja na mchezaji mwenzake, Mohamed Salah na nyota wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang. Mane alikuwa winga mmoja muhimu zaidi kwa kocha, Jurgen Klopp msimu huu.

Liverpool walimsajili Mane mwaka 2016 kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 34 kutoka Southampton, na kumfanya mmoja wa wachezaji ghali zaidi Afrika katika historia ya wakati wote.

Tangu alipojiunga na Liverpool, amekuwa mmoja wa wachezaji wakubwa kwenye Ligi Kuu na kutwaa kwake Kiatu cha Dhahabu kumethibitisha hilo.

Akiwa mmoja wa wachezaji wenye mashabiki wengi kwa 'Wekundu' hao, Mane amekuwa anaimarika siku hadi siku katika dimba hilo la Anfield. Mabao yake yamekuwa muhimu kwa klabu na ameonyesha umuhimu wake.

### 3. Eden Hazard

Chelsea huu ni msimu wao bora zaidi na Eden Hazard ndio amekuwa katikati ya mafanikio hayo. Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alikuwa na wakati mzuri katika kipindi chake cha uchezaji hapo.

Eden Hazard alikuwa katika kilele cha uchezaji kwa kipindi cha msimu wote. Alimaliza msimu akiwa anaongoza kwa kutoa pasi za mwisho 15, huku akifunga mabao 16.

Amekuwa na mchango mkubwa kuliko mchezaji yeyote kwenye Ligi Kuu msimu huu, kwani ukijumlisha mabao yake na pasi za mwisho inakuwa ni 31.

Hazard kujumuishwa kwenye kikosi cha mwaka cha Ligi Kuu ya England, (PFA) ni sahihi na kuiwezesha Chelsea kumaliza nafasi ya tatu katika msimamo wa Ligi Kuu, huku pia wakibeba taji la Ligi ya Europa.

Lakini kwa bahati mbaya, huu unaweza kuwa msimu wa mwisho kwa Hazard kuonekana kwenye Ligi Kuu, kwani anapanga kuhamia kwa Real Madrid kipindi cha majira ya joto.

### 2. Raheem Sterling

Raheem Sterling alikuwa mchezaji mwenye thamani kubwa sio tu kwa klabu yake, bali kwa ligi yote kwa msimu huu wa 2018/19.

Sio miaka mingi iliyopita Raheem Sterling alionekana kutokuwa kwenye midomo ya mashabiki wa England. Alikuwa akishutumiwa mno na makocha pamoja na wachezaji wenzake.

Kwa mwaka 2019, Raheem Sterling amecheza mchezo wa kuvutia mno kwenye Ligi Kuu na alikosa tuzo ya mchezaji bora wa mwaka.

Sterling ameonyesha kuimarika zaidi pale Manchester City, hasa tangu baada ya kutua kwa Pep Guardiola kama kocha wa klabu hiyo.

Ameonyesha kiwango cha kuvutia zaidi chini ya Pep na sasa ni mmoja wa wachezaji wenye thamani kubwa kwenye ligi hiyo.

Mwanzoni mwa uchezaji wake, Sterling alionekana kama hafanyi maamuzi yanayoridhisha akiwa uwanjani. Lakini sasa ni mmoja wa wachezaji ambaye anacheza kwa kiwango cha kuvutia na mwenye uwezo mkubwa wa kufunga mabao kwa mguu wa kulia. Amekuwa silaha ya City kwenye safu ya ushambuliaji kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita.

Sterling amekuwa chaguo la kwanza kwa kikosi cha Guardiola kwa msimu wote. Amecheza katika mechi 34 kati ya 38 za City kwenye Ligi Kuu na kufunga mabao 17 na kutoa pasi za mwisho 10. Na hilo limethibitisha kwamba amekuwa mmoja wa wachezaji muhimu zaidi kwa timu.

### 1. Virgil Van Dijk

Ni mchezaji bora wa mwaka wa Ligi Kuu msimu huu na kwa sasa ni beki bora barani Ulaya na yeye Virgil Van Dijk ndio anayeongoza kwenye orodha yetu.

Liverpool imemaliza msimu ikiwa nafasi ya pili kwenye msimamo na ilicheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya pili mfululizo na msimu huu ikitwaa ubingwa huo, katika mafanikio hayo huwezi kuacha kumtaja beki huyo wa Uholanzi ambaye amekuwa na mchango mkubwa.

Mholanzi huyo alisajiliwa Januari mwaka 2018 akitokea Southampton kwa ada ya pauni milioni 75 ambayo wengi walishutumu mwanzo.


Lakini kwa msimu mmoja na nusu, amethibitisha thamani yake na kumfanya kuwa mmoja wa mabeki imara zaidi duniani kwa sasa. Van Dijk amejipambanua kama mmoja wa mabeki bora wa Liverpool.

Van Dijk amekuwa ndio moja ya jina la kwanza katika kikosi cha Liverpool msimu huu. Moja ya ukweli kuhusu Van Dijk amekuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi kwa sasa.

Pamoja na kucheza kwenye safu ya ulinzi, pia amefunga mabao manne kwenye Ligi Kuu msimu huu. Van Dijk sio tu beki bora kwenye Ligi Kuu bali pia duniani kwa sasa.

Na kwa sasa anaipigania tuzo ya Ballon d'Or ambayo ni kubwa zaidi kwa kutambua mchango wa mchezaji binafsi.


## NUKUU



"Arsenal ilikosa moyo wa kujituma. Hii ni taarifa ya kwanza niliyopewa wakati nilipotua hapa, ikiwa na [Arsene] Wenger, ilikuwa ya ushindani na pia aliipa ubora timu, na moyo wa kishindani, uliotengeneza nyakati nzuri Arsenal, lakini miaka yake ya mwisho walipoteza kuwa washindani, na kuwa na ubora tu. Timu ni hatua kwa hatua inabadilika," **kocha wa Arsenal, Unai Emery**



"Hazard ni shida wakati wa mechi, lakini wakati mwingine ndani ya wiki yeye ni tatizo, ni mwenye kipaji sana na ana kera wakati wa mazoezi kwa sababu kila kitu ni rahisi kwake. Kwa sasa, Eden ni mmoja wa wachezaji muhimu zaidi Ulaya na duniani," **Maurizio Sarri, kabla ya kuivaa Arsenal kwenye mechi ya fainali ya Europa League**



"Nia yangu kama meneja na kama kocha ni wazi, ninataka wachezaji wangu wote kubaki hapa PSG na kubaki na mradi wetu. Kazi bado haijamalizika, ndiyo kwanza imeanza. Nia yangu ipo wazi, lakini siwezi kuahidi kwa sababu itakuwa ni kukosa busara na sitaki kukosa busara katika biashara hii," **Kocha Mkuu wa Paris Saint-Germain, Thomas Tuchel akizungumzia tetesi za Neymar na Kylian Mbappe kusepa majira haya ya joto.**



# KAGERE ALIVYOTUNGUA MAKIPA LIGI KUU BARA

Na Adam Fungamwango

NDIYE mfungaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, akiwa amepachika mabao 23.

Alhamisi iliyopita alifanikiwa kupata tuzo mbili za Mo Award 2019 kwenye hafla ya klabu hiyo ya kutunuku wachezaji wao.

Kwanza kabisa alipata ya mfungaji bora wa klabu, lakini baadaye akatangazwa kuwa mchezaji bora wa klabu hiyo kwa mwaka 2019.

Huyu si mwingine bali ni straika wa Kinyarwanda, Meddie Kagere. Straika huyo aliyesajiliwa kutoka Gor Mahia ya Kenya, huu ndiyo msimu wake wa kwanza kucheza Ligi Kuu ya Tanzania na kuwa ndiye mhimili mkubwa wa klabu hiyo kutwaa ubingwa msimu huu akiwafungia idadi hiyo ya mabao.

Mbali na Ligi Kuu, Kagere ameifungia Simba jumla ya mabao sita kwenye mechi za kimataifa, Ligi ya Mabingwa Afrika.

Hata hivyo, leo tutamzungumzia kwenye Ligi Kuu tu. "Tuzo nilizozipata si za kwangu peke yangu. Pia ni za wachezaji wenzangu kwa sababu tunapendana, tunasikilizana, tunashauriana na tunaelekezana na hayo yote ndiyo yanayosababisha mimi nafanya vizuri na kufunga mabao." Anasema straika huyo mpole nje ya uwanja, lakini hatari kama simba mwindaji akiwa ndani ya dimba.

Kagere ni mmoja wa mastraika wachache wanaocheza Ligi Kuu mwenye nguvu, utimamu wa mwili na akili nyingi na ni hatari anapolikaribia lango la timu pinzani.

Kwenye makala haya tunangalia ni jinsi gani straika huyo alivyofunga mabao yote hayo, timu alizozifunga na pia viwanja alivyofunga.

**Mechi 16 mabao 23**

Kagere ametumia mechi 16 kuweza kupata idadi hiyo ya mabao kwenye Ligi Kuu, ukiacha mechi ambazo amecheza bila kufunga na chache ambazo hakucheza.

**Hat-trick moja msimu wa kwanza**

Akiwa kwenye msimu wa kwanza, straika huyo amefunga 'hat-trick' moja kwenye Ligi Kuu msimu uliomalizika wa 2018/19. Aliipata Mei 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru alipofunga mabao matatu kwenye mechi dhidi ya Coastal Union, akisaidia timu yake kushinda 8-1.

**Uwanja wa Taifa umemkoma**

Katika ya mabao 23 aliyofunga, tisa amefunga kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam na ndiyo uwanja ambao amecheka na nyavu mara nyingi zaidi kuliko uwanja wowote ule uliochezwa Ligi Kuu. Kiwanja kinachofuatia kwa kufunga mabao mengi ni Mkwakwani Tanga akifunga manne kwenye mechi mbili tofauti, mawili dhidi ya JKT Tanzania na mawili dhidi ya Coastal Union.

**Amevitoboa viwanja nane**

Mabao yote hayo amefunga kwenye viwanja nane vilivyokuwa vikichezewa Ligi Kuu msimu uliomalizika. Viwanja hivyo ni Taifa jijini Dar es Salaam, Kambarage mjini Shinyanga, Mkwakwani Tanga, Jamhuri Morogoro, Sokoine Mbeya, Uhuru jijini Dar es Salaam, Namfua mjini Singida na Samora mjini Iringa.

**Mabao matatu ya penalti**

Kati ya mabao 23 aliyofunga, matatu ameyafunga kwa mkwaju wa penalti. Alizipata kwenye mechi dhidi ya Ruvu Shooting wakati Simba ikishinda mabao 2-0, dhidi ya Mbao, akiisaidia timu yake kushinda 3-0 na dhidi ya Coastal Union, Simba ikishinda 2-1.

**Mabao matano mguu wa kushoto**

Mabao matano ameyaweka wavuni kwa mguu wa kushoto na mechi hizo ni dhidi ya JKT Tanzania timu yake ikishinda 2-0, Coastal Union mawili kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza na wa pili, ikishinda 2-1 na nyingine mabao 8-1, mawili dhidi ya Ndanda FC, Simba ikishinda 2-0, yote akitumbukiza mwenyewe.

**Mabao saba kwa kichwa**.

Amefunga jumla ya mabao saba kwa kichwa. Matatu dhidi ya Mbeya City, mawili akiyafunga kwenye mzunguko wa kwanza Simba ikishinda 2-0 yote akifunga yeye, na moja kwenye mechi ya mzunguko wa pili kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya, akiifanya timu yake iondoke na ushindi wa mabao 2-1. Mechi zingine ni dhidi ya Mwadui, Yanga, Azam, na Coastal Union.

**Mabao 11 kwa mguu wa kulia**

Kagere amepachika mabao 11 kwa kutumia mguu wake wa kulia. Mabao hayo aliyaweka nyavuni kwenye mechi dhidi ya Prisons, Mwadui, JKT Tanzania, Ruvu Shooting mawili mzunguko wa kwanza na wa pili, Mbao FC, Coastal Union mawili mzunguko wa kwanza na wa pili, Azam, Singida United na Lipuli.

**Timu 12 Ligi Kuu hakuziacha salama**

Amezifunga jumla ya timu 12 kwenye Ligi Kuu, zingine akizifunga mara mbili, mzunguko wa kwanza na wa pili.

Timu zilizopata bahati mbaya ya kufungwa na Kagere mzunguko wa kwanza na wa pili ni Mbeya City, Coastal Union, Mwadui na Ruvu Shooting.

Zingine alizozifunga ni Yanga, Azam, Prisons, Mbao FC, JKT Tanzania, Ndanda FC, Lipuli na Singida United.

## NAJUA WAJUA

Mauricio Pochettino amepoteza mechi zote kubwa za fainali akiwa kocha wa Tottenham, pia alipoteza kwenye fainali ya Kombe la Ligi dhidi ya Chelsea mwaka 2015.



AFRIKA

# MABEKI WAKUISAIDIA ARSENAL 2019/18 HAWA

**LONDON, England**

KIPINDI cha majira ya joto mwaka 2019, unaweza kuwa mmoja wa msimu muhimu zaidi wa usajili kwa Unai Emery ili uweze kujihakikishia nafasi ya kukaa kwa muda mrefu zaidi hapo Arsenal. Ni msimu mwingine tena hawatakuwapo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kumaliza nafasi ya tano na kufungwa kwenye fainali ya Kombe la Europa mjini Baku. Na kwa sasa Arsenal inahitaji kusukwa upya kwa ajili ya msimu ujao. Sehemu ya kwanza ambayo inahitaji kuimarishwa zaidi ni safu ya ulinzi.

Kwa mwaka wa pili mfululizo, Arsenal imefungwa mabao 51 kwenye ligi. Ni Manchester United na West Ham United ndio timu zilizofungwa idadi kubwa zaidi ya mabao katika mechi 10 za ligi hiyo. Wamecheza mechi 8 tu bila nyavu zao kutikiswa msimu huu na kuwa na idadi ndogo zaidi kwenye Ligi Kuu. Wameshindwa kuzuia nyavu zao kutikiswa katika mechi zote za ugenini kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Kwa upande wa ulinzi, msimu huu Arsenal imekuwa ovyo zaidi kwenye Ligi Kuu. Timu inahitajika kufumuliwa yote na hasa kwenye upande wa ulinzi. Laurent Koscielny si tu mchezaji aliyetumika kuwapo uwanjani, lakini Shkodran Mustafi amekuwapo kwa ajii ya safu ya ulinzi.

Nacho Monreal amepoteza nafasi na hayuko fiti kumaliza msimu wote kwa kucheza kila mechi. Stephan Lichtsteiner alikuwa ndiye mchezaji wa akiba. Rob Holding, Calum Chambers na Konstantinos Mavropanos wote ni vijana wanahitaji muda zaidi. Hector Bellerin amekuwa majeruhi kwa kipindi kirefu cha msimu. Ni Sokratis na Maitland-Niles wameonyesha ari ya kupigana kiukweli msimu huu.

Arsenal inahitaji kusukwa upya zaidi. Hapa tunawaangalia mabeki watano ambao wanaweza kuimarisha safu ya ulinzi ya Arsenal...

**5. Djene Dakonam**

Djene Dakonam au anayejulikana kwa jina la Djene ni mchezaji mwenye umri wa miaka 27 kutoka nchini Togo na anacheza nafasi ya beki wa kati katika klabu ya Ligi Kuu Hispania, La Liga, Getafe FC. Getafe imemaliza katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu. Wameonyesha kiwango cha kushangaza msimu huu na wamekuwa na ubora wa kuruhusu mabao machache zaidi kwenye Ligi Kuu kuliko Barcelona na Real Madrid.

Djene amekuwa kwenye kiwango bora zaidi msimu huu. Amekuwa nguzo muhimu zaidi kwa safu ya ulinzi ya Getafe. Akiwa amecheza mechi 34 kwenye ligi msimu huu, amekuwa kwenye kiwango bora kabisa.

Arsenal imekuwa ikimfuatilia kwa muda mrefu hasa msimu huu. Anaingia kwenye wakati bora zaidi kwa kipindi chake cha uchezaji na anaweza kuwa msaada mkubwa zaidi kwa kikosi cha Arsenal kama akisajiliwa.

**4. William Saliba**

William Saliba ni beki mwenye umri wa miaka 18, ambaye anacheza pale katika Klabu ya AS Saint-Etienne kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1. Mchezaji huyu wa kimataifa wa Ufaransa amejiimarisha yeye mwenyewe na kuonyesha ubora wake katika safu ya ulinzi ya Saint-Etienne ambayo imepata nafasi ya kufuzu kucheza ligi ya Europa msimu ujao mbele ya timu kama Marseille na Montpellier. Anaiwakilisha Ufaransa kwenye Kombe la Dunia chini ya umri wa miaka 20.

Ni beki mwenye urefu wa kutosha na amekuwa mzuri kwenye kuokoa mipira ya kichwa. Amekuwa akionekana kama mlinzi imara katika umri wake. Atakuwa mmoja wa wachezaji wenye majaliwa ya muda mrefu zaidi hapo kwenye dimba la Emirates kama ilivyokuwa kwa Matteo Guendouzi, ambaye hakuwa mwoga kuanzishwa katika kikosi cha kwanza.



Kostas Manolas

**3. Kostas Manolas**

Huyu ni beki mwenye umri wa miaka 27, akiwa anacheza pale AS Roma ya Italia anaweza kununuliwa kwa euro milioni 36. Kwa muda mrefu amekuwa akiwaniwa na Arsenal na sasa ni wazi kwamba wanahitaji kumsajili. Kostas Manolas amekuwa mmoja wa mabeki imara zaidi kwa kikosi cha AS Roma kwa miaka kadhaa na ameshaonyesha nia ya kutaka kutua kwa 'Washika Bunduki' hao.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Star, Arsenal imefanya mazungumzo na wawakilishi wa mchezaji huyo, ili kuangalia uwezekano wa yeye kutua pale kwenye dimba la Emirates. Arsenal wapo kwenye mazungumzo na wakala wake, Mino Raiola. Kama atajiunga na Arsenal atakuwa na wachezaji mwenzake wa kimataifa, Sokratis na Mavropanos.

**2. Eric Bailly**

Hili linaweza kuwashangaza wengi, lakini Arsenal imeonyesha nia ya wazi kabisa ya kutaka kumsajili beki huyo wa Klabu ya Manchester United. Tangu alipojiunga na United, Bailly amekuwa na kiwango cha kupanda na kushuka na bado hajaweza kumshawishi kocha Ole Gunnar Solskjaer na bodi ya United.

Majeruhi ya mara kwa mara, yamemfanya Bailly kushindwa kuwa kwenye kikosi cha kwanza chini ya Ole. Kwa mujibu wa gazeti la Metro, Manchester United wapo tayari kusikiliza ofa ya Bailly na wapo tayari kumuachia kama timu ikifikia kiwango wanachokitaka wao. Arsenal wanataka kumsajili Bailly kwa sababu ya uzoefu wake kwenye Ligi Kuu.

**1. Harry Maguire**

Hii ni kubwa kuliko. Harry Maguire anachukuliwa kama mmoja wa mabeki bora kwenye Ligi Kuu ya England. Amekuwa na kiwango kisichoshuka pale Leicester na kumfanya kuendelea kuwa bora zaidi. Amejiimarisha yeye mwenyewe kama ni bora zaidi katika safu ya ulinzi kila alipokuwa dimbani. Sio siri klabu kubwa zote kwenye sita bora ya Ligi Kuu zinawania saini yake.

Kama Arsenal watashinda kwenye mbio za kuwania saini yake, itakuwa moja ya dili kubwa zaidi walilolifanya kipindi cha majira ya joto cha usajili. Sio tu ni beki bora, lakini pia ni kiongozi akiwa dimbani. Kama wakifanikiwa kumsajili watakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kuimarisha safu yao ya ulinzi.



**NDANI YA 18**



Olivier Giroud ni mchezaji wa kwanza kuweza kufunga mabao 11 katika michuano mikubwa ya Ulaya kutoka klabu za England tangu Alan Shearer alipofanya hivyo msimu wa 2004-05 akiwa na Newcastle United.



BAADA ya mechi 380 kwenye Ligi Kuu England, mwishowe bingwa wa England amepatikana. Zilikuwa mbio ngumu kati ya Manchester City na Liverpool, lakini mwisho wa siku, City wakajinyakulia kombe.

Uk.16-17



# KLOPP ALIVYOBEBA 'NDOO' BAADA YA SIKU 2,576

**MADRID, Hispania**

KOCHA Jurgen Klopp ameshinda taji kwenye fainali kwa mara ya kwanza baada ya siku 2,576.

Vijana wa Klopp, Liverpool walithibitisha kwamba wako imara zaidi ya Tottenham kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mjini Madrid, Jumamosi kwa bao la kwanza la mapema la penalti kutoka kwa Mohamed Salah na kuwafanya waelekee kwenye ushindi kabla ya Divock Origi aliyetokea benchi kufunga la pili zikiwa zimebaki dakika tatu mpira kumalizika.

Umekuwa ni mwisho wa gundu kwa Klopp, ambaye alishindwa katika fainali sita zilizopita akiwa hapo Merseyside na katika klabu yake ya zamani ya Borussia Dortmund.

Hapa tunaangalia nyuma, katika fainali zake sita alizoshindwa kabla ya juzi kusherehekea dhidi ya Spurs.

**1. Mwaka 2012 Fainali ya Kombe la Ujerumani: Borussia Dortmund 5 Bayern Munich 2**

Shinji Kagawa aliipa Dortmund uongozi wa mapema, na Mats Hummels akafunga la pili kwa penalti kabla ya Arjen Robben kuifungia Bayern, lakini Robert Lewandowski akaifungia mabao matatu 'hat-trick' na Dortmund ya Klopp kutuwaa mataji mawili ya ndani msimu huo, kabla ya balaa la kufungwa fainali kuanzia hapo.

**2. Mwaka 2013 Fainali Ligi ya Mabingwa Ulaya: Borussia Dortmund 1 Bayern Munich 2**

Fainali hii ilipigwa katika dimba la Wembley, lakini vijana wa Jupp Heynckes, Bayern wakanyanyua tena mabega. Mario Mandzukic alianza kuifungia Dortmund, kabla ya Ilkay Gundogan kusawazisha dakika ya 68 kwa mkwaju wa penalti. Pasi ya kisigino ya Franck Ribery ilitosha kumfanya Robben kufunga bao la ushindi na kuwafanya Bayern kutwaa mataji matatu msimu huo.

**2. Mwaka 2014 Fainali Kombe la Ujerumani: Borussia Dortmund 0 Bayern Munich 2**

Pep Guardiola na Klopp walikutana kwa mara ya kwanza kwenye fainali baada ya gwiji huyo wa Catalunya kuchukua mikoba ya kuinoa Bayern kutoka kwa Heynckes msimu wa 2013-14, huku akitwaa taji la Bundesliga. Dortmund ilimaliza Ligi ikiwa nyuma kwa pointi 19, lakini fainali ya Kombe la Ujerumani mwaka 2014 ilikuwa ngumu, kwani kwa dakika zote 90 timu hazikufungana. Robben na Thomas Muller kila mmoja alifunga bao moja kwenye muda wa ziada na kuiwezesha Bayern kuibuka na ushindi wa 2-0.

**3. Mwaka 2015 Fainali Kombe la Ujerumani: Borussia Dortmund 1 Wolfsburg 3**

Huu ulikuwa ni msimu wa mwisho kwa Klopp hapo Dortmund na alikuwa na ndoto ya kulibeba taji hilo. Lakini ndoto zake ziliyeyuka. Pierre-Emerick Aubameyang aliifungia bao la ufunguzi Dortmund, lakini mabao ya Kevin De Bruyne, Luiz Gustavo na Bas Dost yakiwa yamefungwa ndani ya dakika 16 yakamnyima tena ushindi.

**4. Mwaka 2016 fainali Kombe la EFL: Liverpool 1 Manchester City 1 (Penalti, 1-3)**

Wakiwa wametoka kuwa na msimu mbaya kutoka kwa kocha, Brendan Rodgers, Klopp alichukua mikoba ya kuinoa Liverpool msimu wa 2015-16. Philippe Coutinho alilazimisha mchezo kwenda muda wa ziada baada ya kusawazisha bao la Mbrazil mwenzake, Fernandinho aliyeanza kuifungia Manchester City. Kwenye changamoto ya mikwaju ya penalti golikipa, Willy Caballero aliokoa penalti ya Lucas Leiva, Coutinho na Adam Lallana - na kumruhusu Yaya Toure kufunga ya ushindi kwa Man City.

**5. Mwaka 2016 fainali Kombe la Europa: Liverpool 1 Sevilla 3**

Ilionekana ni kama fainali ya 'Wekundu' hao, Klopp akiwa ametoka kuwatoa nishai waajiri wake wa zamani Dortmund na kutinga fainali hiyo. Daniel Sturridge alianza kufunga dakika ya 35, lakini Sevilla walirudi mchezoni ambapo Kevin Gameiro alisawazisha kabla ya Coke kufunga mara mbili na Sevilla iliyokuwa chini ya kocha wa sasa wa Arsenal, Unai Emery ikatwaa taji hilo kwa mara ya tatu mfululizo.

**6. Mwaka 2018 fainali Ligi ya Mabingwa Ulaya: Liverpool 1 Real Madrid 3**

Hapa ilionekana ni dhahiri kwamba Liverpool wangeshinda taji hili. Hata hivyo, kukosekana kwa Salah kwa kuumizwa dakika za mwanzo na Sergio Ramos kulizima matumaini hayo. Vijana wa Klopp waliweza kusawazisha kwa bao la Sadio Mane, lakini makosa ya Loris Karius na bao la maajabu la Gareth Bale likawapa ushindi Real Madrid.

## USILO LIJUA

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Mohamed Salah ni Mwafrika wa tano kuweza kufunga katika mechi ya fainali ya Kombe la Ulaya, baada ya Rabah Madjer, Samuel Eto'o, Didier Drogba na Sadio Mane.





# Vijana 15,000 wanufaika na ujasiriamali

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

VIJANA 15,000 kutoka mikoa ya Mbeya na Songwe wenye umri kati ya miaka 18 hadi 30, wamenufaika na mradi wa Uimarishaji wa Maendeleo ya Vijana Vijijini kupitia ujasiriamali (STRYDE), ambao unashirikiana na Mfuko wa Master Card Foundation na Tecno Serve, kwa kuboresha maisha kupitia shughuli zao za kilimo na ujasiriamali.

Hayo yalisemwa juzi na Meneja wa STRYDE, Nicolata Chipa, wakati wa shughuli za maonyesho ya bidhaa mbalimbali za vijana, alisema lengo la kuanzisha mradi huo ni kutoa ruzuku ili kuboresha biashara, kujifunza shughuli mbalimbali za kiuchumi kama kilimo cha mboga na matunda, ufugaji na kuunganishwa kwenye fursa za ajira.

Nicolata alisema mradi huo wa miaka mitano ambao ulianza tangu mwaka 2014, unatarajiwa kumalizika Desemba mwaka huu na una lengo la kuwanufaisha vijana 15,000 kutoka katika halmashauri za Wilaya ya Mbeya Jiji, Wilaya ya Mbeya, Rungwe, Mbozi, Kyela, Busokelo na Mbarali.

"Mradi huu umekuwa na msaada kwa vijana hasa wanaoishi kwenye mazingira magumu, tumewapa elimu ya ujasiriamali na kulima kilimo chenye tija, sasa kila mmoja anaweza kutengeneza bidhaa zake na kuongeza thamani ya mazao yake, lakini changamoto iliyopo ni uhakika wa masoko, mradi unaendelea na jitihada za kuwatafutia masoko," alisema Nicolata.

Akisoma risala ya utekelezaji wa mradi huo, Burton Julius, alisema katika awamu tano za mafunzo katika wilaya sita na halmashauri moja za mikoa ya Mbeya na Songwe jumla ya vijana 11,181 sawa na asilimia 62 ya wanawake walipatiwa mafunzo ya moja kwa moja yanayotekelezwa na Tecno Serve.

Aliongeza kuwa katika kukabiliana na changamoto za mitaji kwa vijana hao, Mradi wa STRYDE, umetoa Sh. milioni 291, fedha ambazo zimewafikia walengwa moja kwa moja.

Aidha, alibainisha changamoto zinazoukabili mradi huo kuwa ni baadhi ya vijana kutotambua umuhimu wa mafunzo waliyopewa kama fursa ya kuongeza ujuzi na kujiendeleza kiuchumi sababu ya gharama kubwa za usajili wa vikundi.

Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, James Kasusura, aliupongeza mradi huo kwa kuwafikia vijana wengi na kuwahimiza kujiunga katika vikundi ili kupata mikopo.

Alisema vijana wengi walionyesha bidhaa zao katika maonyesho hayo hawana vikundi, hivyo hawawezi kunufaika na fursa mbalimbali zitakazotokea.

Baadhi ya wanafaika wa mradi huo akiwamo, Fredy Ndabila kutoka Kata ya Igurusi wilayani Mbarali, alisema ametambua fursa mbalimbali za kiuchumi na kutunza akiba ya fedha.

Alisema anatokea familia maskini ambayo alishindwa kumpa mtaji wa kufanya shughuli zake na kupitia mradi huo alipata mtaji na elimu ya ujasiriamali ambayo imemwezesha kutengeneza bidhaa mbalimbali kama batiki na kujiingiza kipato.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (katikati) na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, wakishiriki kukusanya mifuko ya plastiki kwenye maduka na maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mazao jamii ya mikunde yapaisha uchumi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TANZANIA imetajwa kuwa nchi ya pili barani Afrika katika uzalishaji wa mazao jamii ya mikunde na mazao hayo yamekuwa yakiliingizia taifa fedha nyingi kuliko madini ya tanzanite ambayo yanapatikana Tanzania pekee.

Hayo yalisemwa juzi na Meneja Programu wa Baraza la Nafaka Ukanda wa Afrika Mashariki Ofisi ya Tanzania, Ikunda Terry, wakati wa maonyesho ya kilimo biashara yaliyokuwa yameandaliwa na baraza hilo kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti (Tari), tawi la Uyole jijini Mbeya.

Alisema uzalishaji huo unatokana na Tanzania kuwa na ardhi kubwa ambayo inafaa kwa kilimo ikilinganishwa na mataifa mengine hasa ya ukanda wa kusini mwa Jangwa la Sahara.

Terry alisema Tanzania pia ni miongoni mwa nchi zinazofanya vizuri kwenye uzalishaji wa mahindi kwa kushika nafasi ya nne barani Afrika.

"Nchi yetu inashika nafasi ya pili barani Afrika ikiongozwa na Nigeria na tunashika nafasi ya 10 duniani kwenye uzalishaji wa mazao jamii ya mikunde kwa hiyo hizi teknolojia zinazoonyeshwa hapa ni lazima tuendelee kuzisambaza," alisema Terry.

Hata hivyo, alisema pamoja na kuonekana ni nchi inayoongoza kwenye uzalishaji huo, lakini bado uzalishaji upo chini kiasi cha kufanya mazao hayo zikiwamo soya kuagizwa kutoka nchi jirani ya Malawi.

Aliwataka wakulima kuendelea kuchangamkia fursa ya soko la mazao hayo ili kujiinua kiuchumi na kuhakikisha kunakuwa na uhakika wa chakula nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari), Geofrey Mkamilo, alisema lengo la kuandaa maonyesho hayo ni kuwakutanisha wakulima na wataalamu ili wajifunze teknolojia za kilimo cha kisasa.

Alisema kutokana na Sera ya Taifa ya kutaka kufikia uchumi wa kati ifikapo 2025 ni lazima wakulima wabadilike kutoka kwenye kilimo cha kujikimu kwenda kwenye kilimo biashara ambacho kitawafanya wazalishe kwa tija zaidi.

Alisema wakulima hao walikutanishwa pia na kampuni ya ununuzi na wasindikaji wa mazao na kuwa na nafasi ya kuinuka kiuchumi.

"Kilimo ni chakula, kilimo ni biashara na kilimo ni viwanda, hivyo vituo vyetu vya utafiti vinafanya kazi kwa karibu na wakulima ili kuhakikisha wanaongeza tija kwenye uzalishaji," alisema Mkamilo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, akimwakilisha Mkuu wa Mkoa, Albert Chalamila, aliwataka wakulima kuzitumia kwa ufanisi teknolojia walizofundishwa ili wazalishe kwa tija.

Alisema kwa sasa Tanzania imepata soko la mahindi nchini Zimbabwe ambako Rais Dk. John Magufuli alitembelea hivi karibuni na hivyo wakulima wanatakiwa wachangamkie fursa hiyo.

"Nawaagiza maofisa ugani wa vijiji na kata wa mkoa huu wahakikishe wanasambaza teknolojia hizi ambazo ni za kisasa kwa wakulima, ili manufaa ya maonyesho haya yaonekane," alisema Ntinika.

Alilishukuru Baraza la Nafaka na Taasisi ya Utafiti kwa kuyaleta maonyesho hayo mkoani Mbeya badala ya Arusha ambako yalikuwa yanafanyika kila mwaka.

# Bei mifuko mbadala yalalamikiwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADA ya serikali kuanza kutekeleza katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki nchini, baadhi ya wananchi jijini Mbeya wamelalamikia mifuko mbadala wakidai sio imara na inauzwa bei ghali kuliko ile ya plastiki waliyokuwa wamezoea kuitumia.

Wakizungumza na Nipashe katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya, wananchi hao walidai kuwa wazo la serikali kuzuia matumizi ya mifuko ya plastiki ni zuri, lakini wakashauri mifuko mbadala iboreshwe na bei zake zipungue.

Mmoja wa wananchi hao, Joyce Sokolo, alidai kuwa mifuko mbadala inapatikana kwa wingi, lakini sio imara na pamoja na hivyo mtu akibebea mzigo mkubwa ni rahisi kuchanika na kuharibu mali za watu.

Aliiomba serikali kupitia Mamlaka ya Kudhibiti Ubora (TBS) kuhakiki ubora wa mifuko yote inayozalishwa na inayoingizwa nchini ili kuhakikisha ufanisi wa mifuko mbadala. "Mimi nauza ndizi, lakini wateja wakija hapa wakinunua ndizi hata za 2000 hazitoshi kwenye mifuko hii maana ni tumifuko tudogo mno na ni gharama kubwa, pia ni rahisi kuchanika endapo mtu atabeba ndizi nyingi," alisema Joyce.

Naye Neema Mwambene alisema mifuko hiyo inauzwa bei ghali hali ambayo inawalazimu na wao kupandisha bidhaa zao. Aliiomba serikali kusimamia bei elekezi ya mifuko hiyo ili wafanyabiashara wasitumie vibaya dharura ya kusitisha matumizi ya mifuko ya plastiki. Alisema mfuko imara wa kuweza kubeba mzigo wa kawaida inaanzia Sh. 500 wakati mifuko ya plastiki ilikuwa inaanzia Sh. 50.

Akizungumza wakati wa kukusanya mifuko ya plastiki katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliwataka wananchi kuepuka matumizi ya mifuko hiyo ili mkono wa sheria usiwapate.

Alisema kwa sasa mifuko ya plastiki inapatikana kila mahali kwa maelezo kuwa wafanyabiashara wameleta mifuko mbadala ya kutosha katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo. "Kwa sasa wananchi wanatakiwa kuiogopa mifuko ya plastiki kama wanavyoogopa kukutwa na bangi maana sheria ni kali na watakaokamatwa watashughulikiwa vizuri kwa mujibu wa sheria," alisema Chalamila.

Alisisitiza kuwa kulikuwa na muda wa kutosha wa wananchi kujiandaa kuachana na mifuko ya plastiki, hivyo kwa sasa baada ya kuanza kutekelezwa kwa katazo hilo hakuna anayetakiwa kuitumia, kuiuza ama kukutwa na mifuko hiyo.





# Viwango vifungashio changamoto

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma, Simon Odunga, amekiri na kusema kuwa kukosekana kwa viwango na ubora wa vifungashio vinavyotengenezwa kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali nchini bado ni changamoto kwao katika upatikanaji wa masoko ya ndani na nje.

Odunga alisema hayo alipokuwa akizungumza na wazalishaji wa bidhaa mbalimbali alipokuwa akifunga maonyesho ya wajasiriamali jijini Dodoma.

Alisema kuwa pamoja na jitihada zinazofanywa na wajasiriamali, wazalishaji wa bidhaa bado wanakabiliana na ukosefu wa vifungashio venye viwango na ubora hali ambayo inaweza kuwasababishia kukosa masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi.

"Pamoja na baadhi yao kuwa na bidhaa zinazoweza kuingia kwenye ushindani wa masoko, bado kuna wajasiriamali wengi ambao vifungashio ni changamoto kubwa kwao, hali ambayo inaweza kuwasababishia bidhaa zao kutopata masoko hata ya ndani ya nchi," alisema.

Hata hivyo, aliwataka wajasiriamali hao kutoka katika utengenezaji wa bidhaa zao kwa hali ya chini na kwenda kwenye ubora ikiwa na wale wanaosambaza wabuni vifungashio ambavyo vina mvuto na vilivyo bora ukizingatia kuwa biashara ni ushindani.

Alisema kuwa hata hivyo, serikali inaendelea na jitihada zake kuhamasisha kupata viwanda vya kuzalisha vifungashio vizuri na vyenye ubora.

# Waziri ahamasisha amani, utulivu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amewataka Waislamu kuhakikisha wanaimarisha amani na utulivu nchini.

Jafo alitoa kauli hiyo juzi katika msikiti wa Gadafi jijini hapa kwenye hafla ya kufuturisha makundi mbalimbali ya watu wenye mahitaji ikiwamo yatima na wajane, iliyoandaliwa na Jumuiya ya Wanawake wa Kislamu Mkoa wa Dodoma.

Alisema Waislam wanapomalizia Mwezi Mtukufu wa Ramadhan wahakikishe wanajenga Taifa imara ambalo watu wake watakuwa na hofu ya Mungu.


"Tuhakikishe sisi kama taifa katika mambo tunayoyafanya tumtangulize Mungu mbele kwenye kujenga uchumi wa nchi yetu," alisema.

Aliongeza: "Kipindi hichi kilikuwa cha mafunzo ili baada ya Ramadhan tuweze kuwa wacha Mungu, naamini baada ya Ramadhani tutakuwa tumeshika njia ambayo Mungu anahitaji."

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Shamimu Daudi, alisema kuwa wamefuturisha makundi mbalimbali ikiwamo watoto yatima na watu wasiojiweza.

"Leo tumeona tufanye jambo la tofauti tukae nao tuzungumze nao ikiwamo changamoto zinazowakabili, lengo letu ni kurudishiana furaha," alisema.

Aliwahimiza Waislamu na Watanzania kwa ujumla kutendeana vyema na kuachana na matendo maovu yakuwafarakanisha.




Mwanafunzi wa mwaka wa tatu fani ya utatibu Chuo cha City College of Health and Allied Science (CCOHAS) cha Dar es Salaam, Felecian Rubanda, akiwapa maelezo wageni waliotembelea banda la chuo hicho, juzi kwenye maonyesho ya vyuo yaliyofanyika Uwanja wa Jamhuri, Dodoma. **PICHA: IBRAHI JOSEPH**

# Lugola aagiza ukaguzi shirika Jeshi Magereza

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, ameiagiza Bodi mpya ya Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Magereza kuanza mara moja kukagua mahesabu ya shirika hilo. Sambamba na hilo, ameagiza kuhakikisha ndani ya miezi miwili inakusanya madeni yote ya shirika hilo kiasi cha Sh. bilioni 6.5 ambazo taasisi mbalimbali zinadaiwa.

Waziri Lugola alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki katika uzinduzi wa bodi hiyo ya kwanza kuundwa tangu kuanzishwa kwa shirika hilo mwaka 1983. Aliagiza kuitwa mkaguzi wa hesabu ili akague vitabu vyote vya malipo.

"Ili mwisho wa siku tujue tuna madeni gani, tunadaiwa na nani na sisi tunawadai watu gani na hilo deni la Sh. bilioni 6.5 limetokana na madeni gani ili mwisho

wa siku nasi kama taasisi tutoe gawio kwa serikali," alisema.

Lugola aliongeza: "Hakikisheni taasisi zote za kiserikali zinazodaiwa na shirika hilo zinawekewa utaratibu maalum wa kulipa madeni hayo kwa wakati."

Aidha, Lugola aliitaka bodi hiyo kuhakikisha kuwa mahabusu wote na wafungwa wanajitegemea katika chakula bila kutegemea hela kutoka kwenye mfuko mkuu wa hazina kwa ajili ya manunuzi ya chakula. "Hakikisheni mnatumia vizuri ardhi inayomilikiwa na Magereza nchini kuzalisha chakula na miti ya ambayo itatumika kama malighafi kwenye kiwanda chao cha samani kilichopo Arusha," alisema.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Meja Jenerali Jacob Kingu, alisema bodi

hiyo itakuwa msaada mkubwa kwenye utatuzi wa migogoro ya ardhi ambayo ilijitokeza baada ya wananchi kuvamia maeneo ya magereza kwa kujua kuwa ardhi hiyo haina matumizi.

Alisema uvamizi huo umeleta migogoro kati ya wananchi na magereza na kuitaka bodi hiyo kutafuta hati miliki za ardhi za magereza yote nchini ili kuondoa migogoro hiyo. Naye Kamishna Jenerali wa Magereza, Faustine Kasike, alisema shirika hilo lina jumla ya miradi 23 inayotekelezwa ambapo kati ya hiyo miradi 15 ni ya shughuli za kilimo na mifugo na miradi nane ni ya viwanda vidogo vidogo.

Alifafanua zaidi ya kuwa shirika hilo limeingia ubia na mashirika ya mifuko ya hifadhi za jamii ya PSSSF na NSSF kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za uzalishaji katika kiwanda chao cha ngozi kilichopo mjini Moshi na ya kilimo cha miwa na ujenzi wa kiwanda cha sukari.





Viongozi mbalimbali wa serikali akiwamo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (wa kwanza) Issa Haji Gavu, wakipakua chakula cha futari kilichoandaliwa na Kampuni ya RAK GAS ya Ras Al Khaimah. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# UWT Z'bar yajipanga CCM kushinda 2020

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UMOJA wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Tanzania Mkoa wa Mjini Unguja, wametakiwa kujipanga kuhakikisha CCM inapata ushindi mkubwa wa kihistoria katika Uchaguzi Mkuu mwaka 2020.

Wito huo umetolewa na Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Abdulla Juma Saadalla Mabodi, wakati akifungua mafunzo elekezi ya kuwajengea uwezo viongozi mbalimbali wa UWT kuanzia ngazi za wadi hadi Mkoa wa Mjini, yaliyofanyika mjini Unguja.

Dk. Mabodi alisema wanawake wa CCM wanatakiwa kuwa mstari wa mbele kuandaa mazingira rafiki ya upatikanaji wa ushindi wa CCM katika uchaguzi mkuu ujao kwa kuongeza wanachama wapya na kuhakikisha wanaipigia kura nyingi CCM katika uchaguzi mkuu ujao.

Alisema wanawake wana historia kubwa na nzuri ya kufanikisha harakati za ushindi wa chama na mikakati mbalimbali ya ukombozi wa nchi za Afrika.

Alisema UWT pamoja na jumuiya zingine za CCM zinatakiwa kushirikiana kuandaa mazingira ya ushindi katika uchaguzi ujao, ili kutimiza kwa vitendo kaulimbiu ya umoja ni ushindi ndani na nje ya CCM.

Akizungumzia mafunzo hayo, Dk. Mabodi alisema, mafunzo ni jambo muhimu katika shughuli za kisiasa kwa kuwa viongozi na watendaji wanajengewa uwezo wa masuala mbalimbali ili watekeleze majukumu yao kwa uhakika.

"Mafunzo haya yasiishie katika ngazi ya wadi tu bali yashuke mpaka ngazi za matawi hadi mashina kwa lengo la kuhakikisha jeshi letu linakuwa na uwezo mkubwa wa kufanikisha ushindi wa CCM mwaka 2020," alisema Dk. Mabodi.

Aidha, aliwasihi kutojihusisha na masuala ya makundi ya kubeba wagombea wa nafasi za urais, ubunge, uwakilishi na diwani kabla ya chama kutoa maelekezo ya kampeni na atakayebainika kufanya hivyo chama kitamchukulia hatua za kimaadili.

Alisema CCM imekuwa mstari wa mbele kuhamasisha jamii kuenzi amani na utulivu ili kutoa nafasi pana kwa serikali kutekeleza kwa ufasini shughuli mbalimbali za maendeleo.

Alisema kwa kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa awamu ya pili ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, nchi imepiga hatua kubwa za kimaendeleo kutokana na kuimarika kwa amani.

Naibu Katibu Mkuu wa UWT Zanzibar, Tunu Juma Kondo, alisema umoja huo unaendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo viongozi na watendaji wake ili waingie katika harakati za uchaguzi mkuu ujao wakiwa na uwezo mzuri wa kiutendaji na kiuongozi.

Mbunge wa Viti Maalum kupitia Mkoa wa Mjini Unguja, Asha Abdallah, alisema watayafanyia kazi maelekezo waliyopewa kwa lengo la kuimarisha UWT na CCM.

Alisema wanawake wa mkoa huo wapo tayari kupambana na vita ya kisiasa na kuhakikisha CCM inashinda kwa kishindo katika ngazi mbalimbali uchaguzi mkuu ujao.

# Utafiti mafuta, gesi wakamilika hatua ya kwanza

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MTENDAJI Mkuu wa Kampuni ya RAK GAS ya Ras, Al Khaimah, Nishant Dighe, amesema mchakato wa utafiti wa mafuta na gesi Zanzibar kwa hatua ya kwanza umekamilika na kinachofanyika sasa ni kutafsiri takwimu kazi itakayokamilika Septemba, mwaka huu.

Alisema hayo katika hafla ya futari iliyoandaliwa na RAK GAS Zanzibar, mjini hapa.

Alisema RAK GAS imejizatiti kutekeleza makubaliano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikiwamo kuzijengea uwezo taasisi za elimu pamoja kusomesha wataalamu watakaohudumu katika sekta hiyo.

Naye Meneja wa RAK GAS Zanzibar, Damascene Makaty, alisema baada ya kazi ya kutafsiri takwimu kukamilika takayofuata ni wataalamu wa miamba (Geologist) kuelekeza kuchimbwa kisima cha mafuta au gesi, hata hivyo, alitahadharisha kuwa haimaanishi kusema Zanzibar ina mafuta.

"Kwa sasa kazi yote ya kutafisri takwimu tumemaliza isipokuwa takwimu za kina kifupi cha maji na nafikiria ifikapo Septemba tutakuwa tumemaliza kazi yote ya kutafsiri takwimu kwa hivyo tunakuwa na uwezo wa kusema wapi tuchimbe kisima," alisema.

Hata hivyo, alisema kuchimba kisima hakuna maana kwamba Zanzibar ndio ina mafuta isipokuwa ni sababu za kuamini kuwa eneo hilo kuna rasilimali ya mafuta au gesi.

"Hatua itakayofuata ni kuangalia jee yapo kwa kiasi gani, tukiyachimba tutarejesha gharama kupata faida na serikali kupata pesa, kwa hivyo kuna hatua nyingi za kufanya mbele na inaweza kuchukua muda mrefu na kuchimba kisima si jambo dogo ni gharama kubwa," alisema.

Kuhusu mazingira, alisema wamechukua hatua madhubuti kuhakikisha hakuna uharibifu ikiwamo kufanya tathmini ya kimazingira (EIA) na ikionekana kuna eneo ambalo hatufanyi vizuri, serikali na mamlaka zinazohusika na sekta hiyo zinachukua hatua.

Alisema katika utafiti uliokamilika, hakuna athari kubwa za kimazingira zilizojitokeza, lakini zilishughulikiwa na hazikuiathiri jamii.

"Tunashirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMA) na tunatekeleza masharti ya sheria ya mazingira, ndio maana tunawashirikisha katika kila hatua," alisema.

Alisema mbali ya ZEMA wanafanyakazi na taasisi zote ambazo zinagusa sekta hiyo ikiwamo ZRPA na ZPDD na kwamba wanatarajia mwezi Julai kufanya mkutano na serikali kuzungumzia sekta hiyo.

"Tunataka kukutana wadau wengine kwa mfano Shirika la Umeme na Mamlaka ya Maji ili kuzungumzia masuala mbalimbali kuhusu rasilimali hizi," alisema.

Kuhusu kumlinda mzawa, alisema ajira kwenye kampuni hiyo kipaumbele ni kwa vijana kutoka Zanzibar isipokuwa wafanyakazi watatu, wawili kutoka Tanzania Bara (akiwamo yeye) na raia wa kigeni kutoka India ambae ni mtaalamu wa gesi.

"Lakini tumemwajiri binti mmoja wa Kizanzibari yuko chini yake na anafanya vizuri sana, tunatarajia ndani ya miaka miwili atachukua nafasi ya raia huyu wa India."

# Ubalozi China watoa msaada kwa watoto Mazizini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UBALOZI mdogo wa China ulipo Zanzibar umekabidhi msaada wa chakula na vifaa mbalimbali kwa watoto wanaoishi nyumba ya kulelea watoto yatima Mazizini, ikiwa ni mwendelezo wa kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia wa muda mrefu katika ya Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China.

Vifaa vilivyotolewa ni pamoja na mabegi ya shule, kalamu, madafatari, mipira ya kuchezea, maziwa, sabuni na manukato ili visaidie kuwafariji kuelekea Sikukuu ya Eid na maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika.

Akikabidhi msaada huo kwa niaba ya Ubalozi wa China, Mke wa Balozi wa China, Liu Jie, alisema nchi rafiki wa China zimeongezeka duniani, lakini kamwe China haiwezi kuisahau Tanzania ambayo imekuwa rafiki wa muda mrefu.

Alisema China itaendeleza uaminifu wake wa kisiasa na Tanzania na kushirikiana katika nyanja za kiuchumi na biashara.

Lui alisema kuwa China itazidisha nguvu ya misaada kwa Tanzania kwa lengo la kuwasaidia wananchi wake kuishi kwa furaha na amani.

"Miaka ya 1970 ambapo uchumi wa China ulikuwa mdogo tuliweza kusaidia kujenga reli ya Tazara, hivyo tutaendelea kusaidia mambo mengine muhimu katika kipindi hiki ambacho uchumi wa China umekuwa na kuwa taifa la pili duniani kiuchumi," alisema Mama Lui.

Kwa upande wake Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Moudline Cyrus Castiko, aliishukuru China kwa kuendelea kuisaidia Tanzania katika nyanja mbalimbali za kimaendeleo.

Alisema watoto ni nguvu kubwa ya kujenga makabila na taifa hivyo ni wajibu wa kila mmoja kuwasaidia, ili kutimiza malengo yao.

Alimpongeza mke wa balozi huyo wa China kwa misaada mbalimbali anayoitoa kwa watoto, mwaka 2017 akiwa na mke wa Rais Shein, waliwaletea vyakula, vifaa vya kusomea na kupima afya za watoto kituoni hapo.

Waziri Castiko alitoa wito kwa jamii kutoa misaada ya mahitaji kwa watoto wanolelewa katika kituo cha Mazizini ili kuwafariji.

"Kila mtu anahitaji kuguswa na watoto hawa ambao hawana wazazi na wito wangu anayetaka kuwasaidia aje kituoni, kwa wale wasio na uwezo hata kuwapa maneno ya faraja ni msaada mkubwa kwao," alisema Castiko.

HABARI MIKOANI

# Jenga Afya yatarajia kuuza hisa bil. 7/-

**Na Mary Geofrey**

KATIKA kukuza sekta ya viwanda nchini, Kampuni ya Umma ya Jenga Afya, Teketeza Umaskini (Jatu TLC), ambayo inawajengea wakulima viwanda, imejipanga kuingia kwenye soko la hisa la Dar es Salaam (DSE) kuanzia Agosti, mwaka huu na wanatarajia kuuza hisa za thamani ya Sh. bilioni 7.5 kwa ajili ya kuendeleza miradi ya kilimo.

Mkurugenzi wa Jatu TLC, Peter Isare, aliyeleza hayo mbele ya waandishi wa habari juzi katika mkutano mkuu wa wanahisa wa Jatu waliokutana kwa ajili ya kufanya uchaguzi wa viongozi wake.

Alisema watahakikisha wanawasaidia wakulima kulima kilimo cha kisasa kupitia kwa wataalamu wake na kuhakikisha malighafi zinawafikia shambani kwa kuwawekea viwanda ambacho kitakuwa kinazalisha hapo hapo, ili kuepuka gharama za usafiri wa kutoa mazao shambani na kupeleka viwandani. "Kama Tanzania ina wilaya 200 tunatakiwa kwenda katika kila wilaya na kuhakikisha tunapata hekari isiyopungua 500. Jatu TLC tutahakikisha tunaweka kilimo cha kisasa katika mashamba hayo na kuhakikisha tunafunga kiwanda ambacho kitazalisha malighafi hiyo hapo inayolimwa na tunaipeleka wenyewe sokoni," alisema.

Alisema watawezesha wakulima kulima kilimo cha kisasa na kuwapatia wataalamu ambao watawapa elimu ya kilimo cha umwagiliaji.

Alisema Jatu ni kampuni iliyosajiliwa mwaka 2016 na imefanikiwa katika kiilimo cha mpunga Kilombero na Manyara, alizeti na mahindi mkoani Tanga na maharage. Aidha, alisema katika ripoti ya mwaka 2022 inaonyesha kampuni hiyo itawafikia watu wapatao milioni tano katika kuboresha viwanda, kilimo na Saccos ya kampuni waliokuwa nayo katika kilimo.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Felix Lyaniva, akifungua mkutano huo, aliwatahadharisha kuzingatia kanuni za katiba ya chama chao katika kuelekea soko la hisa ili kusiwapo na sintofahamu kati yao.



Baadhi ya wafanyakazi wa Kampuni ya TBL Mwanza, wakishiriki kupata futari iliyoandaliwa na kampuni hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkemia Mkuu awafunda wakaguzi maabara

**Na Mary Geofrey**

MKEMIA Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, amewataka wakaguzi wa kemikali na maabara za kemia kuzingatia weledi, uadilifu na uaminifu katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotumwa kwa vyombo vya habari jana, Mkemia Mkuu wa Serikali aliyeleza hayo jijini Dar es Salaam, wakati akifungua mkutano wa mwaka wa wakaguzi wa kemikali na maabara za kemia kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA).

"Serikali imetupa majukumu ya kusimamia Sheria ya GCLA, Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Nyumbani na Sheria ya Vinasaba vya Binadamu, hivyo tunapaswa kuzingatia weledi, uadilifu, uaminifu na upendo ili kuhakikisha tunatekeleza majukumu yetu kwa ufanisi.

Tutambue serikali yetu imejielekeza katika kujenga uchumi wa viwanda na inajitahidi kuwekeza mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara ikiwamo wanaojihusisha na kemikali, hivyo tunapotekeleza majukumu yetu tunapaswa kuelewa uelekeo huo wa serikali na kufanya uamuzi kwa wakati na haraka, ili kutokwamisha wadau wetu huku tukizingatia sheria," alielelza.

Aidha, alisema Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti inawapongeza wakaguzi hao kutokana na kazi kubwa wanayofanya na inawahamasisha kuboresha zaidi huduma kwa wadau kwa kufuata sheria, taratibu na kanuni zinazowaongoza kama watumishi wa umma.

"Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti inatambua mchango mkubwa wa wakaguzi katika kusimamia sheria na kuingiza maduhuli ambayo taasisi inatumia katika kuboresha huduma na kujiendesha. Tunatambua changamoto zipo na tunaendelea kuzifanyia kazi kama kuongeza watumishi na vitendea kazi," alisema Dk. Mafumiko.

Alisema wana maeneo ya msingi ya kuyawekea kipaumbele hasa kwenye uwekezaji wa mitambo ya kisasa ya maabara na teknolojia, ili kuwawezesha wakaguzi kutoa huduma bora na za haraka kwa wadau.

Kwa upande wake, Mkaguzi wa Kemikali, Jovitus Mukela, aliwasihi wakaguzi wenzake kuzingatia yale yote yalinayotakiwa katika utekelezaji wa majukumu yao na kushirikiana kutoa huduma nzuri.

"Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeitendea haki Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, sisi wenyewe na nchi kwa ujumla," alisema Mukela.

## Shirika kushirikiana na TRA kukagua ushirika

**Na Mwanandishi Wetu**

SHIRIKA la ukaguzi wa hesabu la Coasco liko kwenye mpango wa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutoa elimu kwa wanaushirika, kulipa kodi itakayosaidia kuleta maendeleo ya huduma za kijamii hapa nchini.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Zavery Mkingule, alisema lengo la kushirikiana na TRA ni kutoa mafunzo kwa wanachama wao ambao ni wanaushirika kufahamu umuhimu wa kulipa kodi na faida zake, ili wanapo timizi wajibu wao wa ukaguzi wa mahesabu ya wanaushirika wawe wameandaa na mfumo mzima wa ulipaji kodi, ili shirika hilo liweze kufanikisha azma yake ya kiukaguzi ikiwa ni pamoja na mapato ya serikali.

Alisema wanaushirika wamekuwa wanapata changamoto kutokana na kukosa elimu ya mlipakodi kutokana na shirika hilo kukosa bajeti ya kutoa elimu kwa wanaushirika inayohusu kodi na ukaguzi kwa wanaushirika kupanga hesabu zao kwa umakini ikiwamo kutunza mahesabu kwa usahihi.

Shirika la Coasco limekuwa likikagua hesabu za taasisi mbalimbali za ushirika na kuzifanya zijiendeshe kwa faida badala ya kujiendesha kwa hasara na kunufaika na mikopo kutoka taasisi za fedha na ruzuku kutoka kwa wafadhili ikiwamo serikali kusaidia baadhi ya vyama ushirika kupata fedha zakujiendesha na kujimarisha kwenye ushirika wao.

Mkingule alisisitiza kuwa wanaushirika wana wajibu wa kulitumia shirika hilo katika kukagua hesabu zao, ili kuepuka ubadhirifu na matumizi mabaya ya fedha za ushirika pamoja na kutunza hesabu zao kwa makini ili wana ushirika wawe na imani na viongozi wanaosimamia taasisi hizo.

## Trump aitaka Uingereza kujitoa EU bila makubaliano

**LONDON, Uingereza**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ameliambia gazeti la Uingereza The Sunday Telegraph katika mkesha wa ziara yake mjini London, kuwa Uingereza inapaswa kuchukua uamuzi wa kujitoa kutoka Umoja wa Ulaya bila ya makubaliano.

Aidha, ameahidi kulipa Euro bilioni 45 (sawa na Sh. trilioni 115.6), kama fedha ya kujitoa.

Kauli ya kiongozi huyo imekuja siku chache baada ya Waziri Mkuu wa Uingereza, Theresa May, kutangaza kukusudia kujiuzulu Juni 7, mwaka huu, baada ya kushindwa kukamilisha hatua za Uingereza kujitoa EU yaani Brexit.

Trump aliliambia gazeti la Sun la Uingereza kwamba anafikiria kwamba Waziri wa zamani wa Mambo ya Kigeni wa Uingereza, Boris Johnson, atakuwa Waziri Mkuu bora kuchukua nafasi ya May, waziri mkuu ambaye atajiuzulu Juni 7.

Trump anaanza ziara ya siku tatu nchini Uingereza kesho, na kwamba atakutana na malkia Elezabeth wa pili na kuwa na mazungumzo na May.

**DW**



# Mwenyekiti wa chama cha SPD Ujerumani ajiuzulu

**Berlin, Ujerumani**

MWENYEKITI wa chama cha Social Democrat-SPD cha Ujerumani, Andrea Nahles, ameamua kujiuzulu nyadhifa zote mbili baada ya mivutano ya muda mrefu ya kuwania madaraka katika chama hicho.

Katika taarifa yake aliyowatumia wanachama wa chama hicho, alisema "Mijadala miongoni mwa wabunge na taarifa zinazonifikia zinanidhihirishia kuna ukosefu wa imani kuweza kuendelea kutekeleza nyadhifa zangu ipasavyo."

Aidha, alisema leo atawasilisha taarifa rasmi sababu ya kujiuzulu kwa mwenyekiti wa chama mbele ya kamati ya uongozi na kesho atajiuzulu kama mwenyekiti wa kundi la wabunge.

Alisema anataka kurahisisha zoezi la kumchagua au kuwachagua watakaoshika nyadhifa hizo lifanyike kwa njia inayostahiki.

Nahles alisema pia anapanga kuachana na wadhifa wake kama mbunge wa SPD.

Aidha, habari zilizopatikana zinaeleza kuwa upo uwezekano wa Waziri Mkuu wa Jimbo la Rheinland Pfalz, Malu Dreyer, kukabidhiwa kwa muda wadhifa wa mwenyekiti mkutano wa dharura wa chama cha SPD utakapoitishwa. Taarifa hizo zinaeleza kuwa wadhifa wa mwenyekiti wa kundi la wabunge wa chama cha SPD akabidhiwe Naibu wake Mwenyekiti (Nahles) wa kundi hilo, Rolf Mützenich, kama hadi kesho hakutakuwa na wa kuwania wadhifa huo.

Wadau mbalimbali wa siasa na uchumi wamepongeza uamuzi huo kwa siasa za Ujerumani.

Mwenyekiti wa chama cha kiliberali FDP, Christian Lindner, alimtaja Nahles "kuwa mwanasiasa muaminifu na mwenye uwezo. Kujiuzulu kwake sio jibu la suala kuhusu mwongozo wa chama cha SPD, badala yake uamuzi huo unazidi kuidhoofisha serikali ya muungano."

Walinzi wa mazingira die Grüne pia wamemvulia kofia Andrea Nahles. Viongozi wenza wa chama hicho, Annalena Baerbock na Robert Habeck wameelezea matumaini yao kuona nani atakabidhiwa wadhifa gani katika chama hicho kikongwe zaidi cha kisiasa nchini Ujerumani linapatiwa ufumbuzi haraka.

***Chanzo: DW***




Mwonekano wa mahali lilipohifadhiwa jeneza la Dk. Tshisekedi kwa ajili ya mamia ya waombolezaji kutoa heshima za mwisho, mjini Kinshasa. **PICHA: BBC**

# Tshisekedi azikwa kifahari Congo

**KINSHASA, DRC**

KIONGOZI wa zamani wa upinzani wa Jamburi ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Dk. Etienne Tshsekedi, amezikwa katika mazishi ya kufahari, ikiwa ni miaka miwili baada ya kifo chake.

Mwili wake ulisafirishwa kwenda nyumbani wake Alhamisi iliyopita, baada ya kumalizika kwa mgogoro kati ya familia yake na serikali iliyopita ya Joseph Kabila ambao ulikwisha baada ya mwanawe kuwa rais mwaka uliopita.

Maelfu ya watu walihudhuria ibada ya wafu iliyoongozwa na Askofu Fridolin Ambongo katika uwanja wa mashahidi mjini Kinshasa.

Kanisa Katoliki lenye ushawishi mkubwa nchini humo liliwataka wafuasi wake kuhudhuria kwa wingi katika mazishi hayo.

Marais waliohudhuria mazishi hayo ni Paul Kagame wa Rwanda na Joao Lourenco wa Angola, ambao walitoa heshima za mwisho kwa marehemu.

Jeneza lililobeba mwili wa Etienne Tshisekedi lilibaki katika uwanja huo usiku kucha kwa ajili ya wananchi kutoa heshima za mwisho.

Baada ya sherehe hiyo ya mazishi, Dk. Tshisekedi atazikwa katika makazi yake ya Nsele yapata kilomita 40 mashariki mwa katikati mwa Mji mkuu wa Kinshasa.

Alifariki akiwa na umri wa miaka 84 mjini Brussels, Ubelgiji na mwili wake uliwekwa katika nyumba ya kuhifadhi maiti hadi uliposafairishwa nchini humo.

Ijumaa iliyopita katika uwanja wa Martyr uliopo mjini Kinshasa wenye uwezo wa kubeba watu 80,000 ulikumbwa na pongezi, wakati ambapo jeneza hilo lililokuwa likiubeba mwili wa Tshisekedi ulipowasili wafuasi wake walipiga kelele na kupiga miluzi

Tshisekedi alihudumu kisiasa kwa miongo kadhaa, lakini akashindwa katika jaribio la kuwa rais, aliwahi kuwa waziri wa masuala ya ndani katika serikali ya Mbobutu Seseko, kabla ya kujiunga na siasa za upinzani.

Baada ya kuhudumia kifungo jela, alianzisha chama cha UDPS mwaka 1982 na aliteuliwa kuwa Waziri Mkuu na serikali ya Mobutu licha ya kwamba wawili hao walizozana mara kWa mara.

Mwaka 1997, Mobutu aling'atuliwa madarakani katika upinzani ulioongozwa na babaake Joseph Kabila, Laurent.

Tshisekedi alikuwa mpinzani wa utawala mpya wa Joseph Kabila baada ya Laurent Kabila kuuawa mwaka 2001.

BBC

## Wachimbaji watishiwa magonjwa

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WACHIMBAJI wadogo wa madini ya dhahabu katika mgodi usio rasmi kijiji cha Kakola Namba Tisa, Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wako hatarini kupata magonjwa ya mlipuko kutokana na kujisaidia vichakani.

Hayo yalibainishwa jana na Mwenyekiti wa kijiji hicho, Emmanuel Nkenze, wakati akizungumza na waandishi wa habari alivyotembelea mgodi huo, na kusema kuwa tatizo hilo linahitaji kupatiwa ufumbuzi wa haraka ili kuzuia kuzuka kwa magonjwa ya mlipuko.

Alisema kuwa vyoo vilivyo ni matundu kumi ambayo yanaonekana ni machache ukilinganisha na idadi ya wachimbaji wadogo walipopo, ambao idadi yao inazidi kuongezekana siku hadi siku.

"Mgodi huu una wachimbaji wengi, na vyoo vilivyopo vipo kumi tu, hali ambayo wachimbaji wengi hujisaidia vichakani na kusababisha mazingira ya mgodi kuwa machafu sana. Na hapa mvua ikinyesha tu lazima wachimbaji wote wapate ugonjwa wa mlipuko," alisema Nkenze.

Alisema kasi ya ujenzi wa vyoo vinne kwa ajili ya kuwanusuru wachimbaji wadogo na magonjwa ya mlipuko ni mdogo, huku pia wachimbaji wakiwa hawana elimu ya umuhimu wa kujisaidia vyooni kwa kutumia uchache wa vyoo kumi vilivyopo.

Naye Msimamizi Mkuu wa mgodi huo, Husein Makubi, alikili kuwapo kwa tatizo la ukosefu wa vyoo nakuongeza ofisi yake imewekeza nguvu kubwa katika ujenzi wa vyoo ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa matundu ya vyoo ikilinganishwa na idadi ya wachimbaji.

Alisema kuwa, tatizo la upungufu wa vyoo mgodini umetokana na uongezeko la wachimbaji wadogo ambao wamekuwa wakiongezeka kila siku kutokana na eneo hilo kuwa na wingi wa madini.

**"Mgodi huu una wachimbaji wengi, na vyoo vilivyopo vipo kumi tu, hali ambayo wachimbaji wengi hujisaidia vichakani na kusababisha mazingira ya mgodi kuwa machafu sana. Na hapa mvua ikinyesha tu lazima wachimbaji wote wapate ugonjwa wa mlipuko," alisema Nkenze.**

# Waziri atoa maelekezo kupambana na dengue

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ameitaka mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani na mingine ambayo imeathirika na ugonjwa wa dengue kupuliza dawa mara moja kwa ajili ya kuua mbu wakubwa.

Waziri Ummy alitoa agizo hilo jana jijini Dar es Salaam alipofanya ziara katika maeneo mbalimbali jijini Dar es Salaam.

"Niko hapa mimi pamoja na wenzangu kutoka wizarani kwa ajili ya kutoa maelekezo kwa Mkoa wa Dar es Salaam, Tanga, Pwani na mikoa yote ambayo imeathirika na ugonjwa wa dengue, kwa sababu mvua zimekatika kutoa maelekezo ya kuanza kupulizia dawa mara moja kwa ajili ya kuua mbu wanaoambukiza ugonjwa huo," alisema Waziri Ummy.

Alisema tayari wamekubaliana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam kwamba kazi hiyo ianze mara moja na isizidi ndani ya siku tano.

Pia alisema Wizara ya Afya imetoa viuadudu kwa ajili ya kuua viluilui vya mbu.

"Sisi kama Wizara ya Afya, tuliwapa pia viuadudu kwa ajili ya kuua viluilui vya mbu, kwa hiyo pia tuhakikishe dawa hizo zinatumika mara moja na zisiwe zinafungiwa katika store mbalimbali," alisema Waziri Ummy.

Alitoa agizo kwa watu wote wanaoendesha biashara za saluni, baa, migahawa, hoteli, shule za msingi za sekondari, pamoja na makanisa na misikiti kufanya jitihada za kupambana na mbu hao.

"Kwa hiyo lazima kwanza wahakikishe wanasafisha maeneo yanayowazunguka, kufukia madimbwi ya maji, kuondoa vitu vyote vinavyoweka mazalia ya mbu yakiwamo matairi ya gari," alisema Waziri Ummy na kuongeza:

"Lakini pia jambo jingine ambalo tunalielekeza, ni kuhakikisha katika kila nyumba, kila mtaa tuhakikishe tunasafisha mazingira yetu ili kupambana na mbu."




Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Masoko wa Kampuni ya Tigo, William Mpinga (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa ofa mpya inayojulikana kama 'Saizi Yako'. Katikati ni Ofisa Biashara Mkuu Tigo, Tarik Boudiaf na Balozi wa kampeni hiyo, Lucas Muhavile maarufu kama Joti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Hakuna mfuko wa bure tena'

**Na Waandishi Wetu, DODOMA**

JIJI la Dodoma limefanikiwa kwa asilimia 99 kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki, huku baadhi ya wafanyabiashara wakidai kuwa kwa sasa mteja ananunua bidhaa na mfuko, hapewi bure tena.

Hali hiyo imetokana na awali walikuwa wakinunua mifuko ya plastiki 50 kwa Sh. 800, lakini sasa mifuko mbadala 12 kwa Sh. 5,000. Kutokana na mifuko ya plastiki kupatikana kwa bei nafuu walikuwa wakitoa bure kwa wateja wanaonunua bidhaa zao, lakini sasa wanalazimika kuwauzia mifuko na bidhaa.

Wakizungumza wakati wa ukaguzi wa mifuko hiyo baada ya serikali kuagiza kusitishwa kwa uzalishaji na usambazaji wa mifuko hiyo Mei, 31 mwaka huu, walisema kwa wastani matumizi yao kwa mwezi ya mifuko ilikuwa Sh.11,200, ambapo inakuwa mifuko 700 waliitoa bure kwa wateja.

Walisema kwa gharama iliyopo ya mifuko wameokoa fedha zao ambapo sasa wananunua mifuko hiyo mbadala ya kuuza kwa wateja wao na si kuwapa bure.

Mfanyabiashara wa matunda Soko la Sabasaba, Gilbert Marwa, alisema: "Hili zoezi nimefurahi kwa sababu mifuko ya Rambo ilikuwa inachafua mazingira, lakini imetupunguzia gharama sisi wafanyabiashara wa matunda, sasa mteja ananunua bidhaa ananunua na mfuko hakuna kupewa bure tena."

Aliishukuru serikali kwa kudhibiti mifuko hiyo kutokana na athari za kimazingira, huku akitoa wito kwa serikali kuhakikisha inapatikana kwa wingi ili kupunguza gharama iliyopo sasa. "Akinunua hata parachichi mbili tunamwambia mfuko upo lakini Sh.300 au 500, maana bila kufanya hivyo tutapata hasara, kwa hiyo binafsi naona imetusaidia kupunguza gharama za uendeshaji hela iliyokuwa kwenye mzunguko wa mifuko sasa itabaki kwenye mtaji," alisema.

Naye Mariam Mbaruku, alisema ilikuwa ni gharama kwao kwenye suala la mifuko kutokana na mteja kuhitaji mfuko hata akinunua kitu cha Sh. 200.

"Kwa hiyo kwanza imetufanya tuwe na machungu na hii mifuko mbadala hatutumii ovyo, maana unakuta mtu sokoni mifuko ya plastiki alikuwa anaenda nayo nyumbani zaidi ya 10 kwa kuwa kila kitu akinunua anataka mfuko wake, lakini kwasasa hakuna hali hii," alisema.

Aidha, alisema mifuko hiyo ilikuwa na athari nyingi ikiwamo kuua mifugo na Taifa lilikuwa linapata hasara.

Mfanyabiashara wa Soko la Majengo, Saidi Hassan, alisema mifuko mbadala inapatikana kwa gharama kubwa si rahisi mfanyabiashara kununua kuhudumia wateja wake wote. "Kama mfuko wa kati unanunua kwa Sh. 300 mmoja kwa maana hiyo mifuko 10 tu unapata kwa Sh. 3,000 ni vigumu, hivyo hatutoi bure kwa zamani. Pia kuna changamoto ya ubora wa mifuko husika kwenye maduka ya nyama wangepata mifuko mizuri," alisema.

Katika hatua nyingine, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Joseph Malongo, alisema serikali inaendelea kuhamasisha uagizaji na utengenezaji wa mifuko hiyo mbadala nchini.

"Kuna malalamiko kidogo ya uhaba wa mifuko, sisi kama serikali tutaendelea kuhamasisha utengenezaji na uingiza mifuko nchini naamini hali hii itapunguza hata bei na upatikanaji utakuwa mzuri," alisema.

Aliwapongeza viongozi wa mkoa wa Dodoma kwa hamasa na kuitikia wito kuhusu matumizi ya mifuko mbadala na kuachana na ya plastiki.

Alisisitiza serikali itaendelea kufanya ukaguzi katika maeneo mbalimbali ili kubaini kama kuna wafanyabiashara wanaendelea kutengeneza mifuko ya plastiki na watakaobainika watachukuliwa hatua kali za kisheria.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**MAGARI NA VIPURI**

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.

**NAFASI ZA KAZI**

**SALES LADY ANAHITAJIKA,** SALES LADY ANAHITAJIKA MWENYE UZOEFU WA COMPUTER, MITANDAO YA KIJAMII INSTAGRAM NA FACEBOOK. KWA MAWASILIANO PIGA SIMU NAMBA: 0715 88 55 33

**MAGARI NA VIPURI**

**CRANE FUSO FOR SALE,**
(1.) Fighter 2002, SAKAI_340, 3 stages, New in TZ,
2. Magnum 1991, TADANO_290, 2 Stages, 3 years in TZ.
**"Dalali Hatakiwi" Simu 0692 469 669**

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0767 223311

*Uza,*

*Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza*

*Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223 311*

**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO,
NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311**


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## GRIEZMANN SASA AIPONZA BARCA

**MADRID, Hispania**

KLABU ya Atletico Madrid inapanga kuchukua maamuzi ya kuishtaki Barcelona baada ya miamba hao wa Catalunya kufanya mazungumzo na mchezaji wao wa kimataifa wa Ufaransa, Antoine Griezmann, Novemba mwaka jana kabla ya kujaribu kumsajili Machi.

Griezmann tayari amethibitisha uamuzi wake wa kuondoka Atletico, ambako alishinda taji la Ligi ya Europa, UEFA Super na Supercopa de Espana, huku Barça ikionekana kuwa ndio mahali atakapotua.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Gazeti la AS, Griezmann ameshafanya mazungumzo na Barcelona.


Mwishoni mwa Novemba, Atletico walikuwa wamepitwa pointi mbili na waliokuwa vinara wa ligi ya Sevilla, huku Barcelona wakiwa mbele kwa pointi moja, huku Machi walikuwa wanaongoza kwa mabao mawili katika mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano wa timu 16-bora dhidi ya Juventus.

Los Rojiblancos hao walimaliza nafasi ya pili kwenye ligi na walitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Juve kwa mabao matatu 'hat trick' ya Cristiano Ronaldo.

Hata hivyo, bado hawajathibitisha kama watachukua maamuzi hayo dhidi ya Barcelona na wanataka kuchunguza kwanza kabla ya kuchukua maamuzi.

Mkataba wa Griezmann na Atletico unamalizika mwaka 2023, lakini kama akitaka kununuliwa kwa sasa thamani yake ni kuanzia euro milioni 200 hadi 120.

Griezmann alifunga mabao 15 na kutoa pasi za mwisho nane kwenye La Liga msimu huu.





## POCHETTINO:
### SIJUTII KANE KUANZA BADALA YA MOURA

**MADRID, Hispania**

MAURICIO Pochettino hajutii kumuanzisha Harry Kane mbele ya Lucas Moura kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambapo Tottenham ilifungwa na Liverpool juzi Jumamosi.

Kane alicheza kwa dakika zote 90 akiwa amerudi dimbani baada ya kuwa nje kwa miezi miwili, lakini hakuwa na athari yoyote kwa vijana wa Jurgen Klopp ambao walibeba taji hilo kwa mabao mawili ya Mohamed Salah na Divock Origi na kuwafanya waondoke na ushindi wa 2-0 dhidi ya Spurs.

Huku akiwa shujaa kwenye mchezo wa nusu fainali kwa kufunga mabao matatu 'hat-trick', Moura alikuwa benchi pamoja na Dele Alli na kumuacha nahodha huyo wa England akiongoza jahazi la mashambulizi ya Spurs.

Mara baada ya mchezo huo Pochettino alisema: "Yale yalikuwa ni maamuzi na sio maigizo. Kwa upande wangu Harry Kane, baada ya mwezi na nusu, alimaliza vizuri mchezo.

"Hakufunga, lakini yalikuwa ni maamuzi yangu kumuanzisha kwa kutegemea mfumo wa mchezo wetu. Sijutii kwa hilo."

Majaliwa ya Pochettino kwenye klabu hiyo pia yameanza kuzungumzwa mara baada ya mchezo huo, kwani awali alikuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka hapo Tottenham.

Raia huyo wa Argentina awali alikuwa akihushwa na mpango wa kuchukua mikoba ya kuzinoa Manchester United, Real Madrid na Juventus, ambazo zinatajwa kwamba nitataka makocha wapya.

"Tutakuwa na muda wa kuzungumzia majaliwa yangu," alisema Pochettino.

# Chelsea wapo tayati kuiachia Juve Sarri

**LONDON, England**

KLABU ya Chelsea inajiandaa kumpa ruhusa Maurizio Sarri kuhusu maombi yake ya kutaka kujiunga na Juventus, ESPN FC imeripoti.

Sarri aliwasilisha maombi yake kwa mkurugenzi wa soka wa Chelsea, Marina Granovskaia Ijumaa iliyopita kwamba anataka kurudi nchini Italia kwenda kuchukua mikoba ya Massimiliano Allegri, ikiwa ni siku mbili tu baada ya kushinda 4-1 dhidi ya Arsenal na kutwaa taji la Ligi ya Europa, likiwa ndio kombe lake la kwanza.

Chanzo kimoja kimeiambia ESPN FC kwamba, Chelsea wasingemtimua Sarri hata kama asingeshinda kwenye fainali mjini Baku, lakini walikuwa tayari kumuachia kocha huyo kuondoka kama yeye mwenyewe akiamua.

Sarri alisaini mkataba wa miaka miwili na kulikuwa na kipengele cha kuongeza mkataba wa mwaka mmoja wakati alipojiunga na Chelsea akitokea Napoli kipindi cha majira kilichopita.

Rais wa Juventus, Andrea Agnelli, alipigwa picha akiwa na Mwenyekiti wa Chelsea, Bruce Buck, katika hoteli iliyofikia timu hiyo mjini Baku kabla ya mchezo wa fainali wa Ligi ya Europa, huku pia Granovskaia alisafiri kwenda Azerbaijan.

Makubaliano zaidi ya Sarri kuhamia Juventus bado hayajakamilika, lakini Chelsea sasa watatafuta mrithi wake.

Ripoti kutoka nchini Italia, zinamtaja Sarri kama ndio mrithi sahihi wa Allegri, huku Chelsea ikionekana kumnyatia Laurent Blanc kuwa kocha wao mpya.

Frank Lampard pia anatajwa kuwa kwenye orodha ya kuwaniwa na klabu yake hiyo ya zamani baada ya kumaliza msimu wake wa kwanza akiinoa Derby.



## HABARI MICHEZO




# BONDIA JOSHUA ACHEZEA KICHAPO KIKALI ULINGONI

**NEW YORK, Marekani**

BONDIA Anthony Joshua amechezea kichapo kikali kutoka kwa Andy Ruiz Junior na kuchukua mataji yote matatu aliyokuwa anayashikilia bondia huyo katika masumbwi ya uzito wa juu.

Joshua ambaye alikuwa anapewa nafasi kubwa kumrithi bingwa wa zamani katika uzani wa juu, Mohamed Ali, aliangushwa mara nne kabla ya mwamuzi kuingilia kati katika raundi ya saba na kumaliza pambano.

Andy Ruiz Jr sasa amefanikiwa kushinda mataji ya IBF, WBO na WBA yaliyokuwa yakishikiliwa na Joshua.

Katika pambano hilo lililovutia wengi kwenye ukumbi maarufu wa ndondi nchini Marekani wa Madison Square Garden, Ruiz alimuangusha Joshua mara nne kabla ya kumuangusha katika raundi ya saba.

Joshua alikuwa anapewa nafasi ya kushinda kiurahisi, huku wachambuzi wakifananisha pambano hilo na lile la Lennox Lewis na Mike Tyson kama mabondia walioshindwa na kusababisha hali ya sitofahamu katika ndondi duniani.

Baada ya kupigwa ngumi kali ya kushoto, Joshua aliangukia kamba za ukumbi wa ndondi.

Na kabla ya kukamilika kwa dakika tatu za raundi hiyo aliangushwa tena kufuatia Ruiz kumshambulia kwa mchanganyiko wa makonde.

Ruiz alishirikishwa katika pambano hilo baada ya raia wa Marekani Jarell Miller kupatikana na hatia ya kutumia dawa za kusisimua misuli wiki sita tu kabla ya pigano hilo.

Na ilipofikia raundi ya saba, wakati Joshua alipoangushwa mechi hiyo ilikuwa imekwisha kutokana na kupigwa ngumi nyingi zilizomchanganya na kulazimika kutema kifaa kinacholinda meno.

Hakuwa nacho mdomoni na mwamuzi alipoona Joshua kachanganyikiwa aliingilia kati na kusitisha pambano.

Ruiz ambaye kwa sasa ameshinda mara 33 na kupoteza mara moja aliruka ruka katika ukumbi wa ndondi wa Madison Square Garden baada ya mwamuzi kusitisha pambano hilo.

Sasa anajiunga na James Buster Douglas ambaye alimshangaza Tyson na Hashim Rahman aliyempiga Lewis mwaka 2001 kama mmojawapo wa mabondia waliooshangaza ulimwengu.

# Reyes alililiwa kila kona

**SEVILLA, Hispania**

KLABU ya Arsenal imetoa salamu zake kwa mchezaji wake wa zamani, Jose Antonio Reyes ikisema 'wameshtushwa na taarifa kuhusu kifo chake.

Mchezaji wa zamani wa Arsenal, Thierry Henry, ambaye alicheza sambamba na Reyes kati ya mwaka 2004-2007, amemuita 'Mchezaji mahiri, mchezaji mwenza mzuri na binadamu wa kipekee.'

"Ninaombea familia na marafiki waendelee kuwa na nguvu ya kuhimili kipindi hiki kigumu," aliandika Henry kwenye ukurasa wake wa twitter.

Freddie Ljungberg ambaye pia aliwahi kucheza na Reyes amesema, "nimepigwa na butwaa kutokana na taarifa za kifo cha Antonio Reyes."

Klabu aliyokuwa akiichezea hivi karibuni ya Extremadura UD ilitangaza taarifa za kifo cha mchezaji huyo mapema Jumamosi asubuhi.

Reyes alifariki kwa ajali ya gari akiwa



na umri wa miaka 35 na klabu yake ya zamani ya Sevilla ilitangaza.

Reyes mwenye asili ya Hispania alijiunga na Arsenal akitokea Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, Januari mwaka 2004.

Baadaye aliichezea Real Madrid kwa mkopo mwaka 2006-2007, ikashinda taji la Liga. Reyes ameelezwa kuwa 'mkongwe' mmoja kati ya wachezaji wa thamani katika historia ya soka.

Aidha, Reyes ameacha mke Noelia Lopez, ambaye alimuoa Juni mwaka 2017, na watoto watatu, wasichana Noelia na Triana na wa kiume Jose Antonio Jr.

# NEYMAR
## ATUHUMIWA KUBAKA

**SAO PAULO, Brazil**

NYOTA wa timu ya Taifa ya Brazil, Neymar anatuhumiwa kumnyanyasa kingono mwanamke mmoja mjini Paris nchini Ufaransa.

Kwa mujibu wa ripoti ya polisi iliyowasilishwa mjini Sao Paulo, mwanamke huyo amedai kwamba shambulio hilo lilifanyika katika hoteli moja mjini hapo ambapo Neymar anaichezea Klabu ya Paris Saint-Germain, PSG.

Neymar kwa sasa yuko nchini Brazil akifanya mazoezi na timu ya taifa tayari kwa maandalizi ya Kombe la Copa America.

Kwa mujibu wa ushahidi wa polisi, mwanamke huyo ambaye jina lake halijatajwa alijuana na Neymar kupitia mtandao wa Instagram na wakakubaliana naye kwamba wakutane mjini Paris.

Alimtumia tiketi ya ndege kutoka Brazil kuelekea Ufaransa na pia alimlipia chumba cha kulala katika Hoteli ya Sofitel Paris arc Du Triomp.

Mei 15, mwaka huu baada ya mazungumzo Neymar alidai kujaribu kumbaka kwa lazima na kwa nguvu akashiriki naye tendo la ngono kinyume na matakwa yake, kwa mujibu wa hati hizo za polisi.

Baadaye mwanamke huyo alidaiwa kurudi Brazil siku mbili baadaye, bila kuripoti tukio hilo kwa maofisa wa polisi wa Ufaransa, kwa kuwa alikuwa amejawa na hofu kuwasilisha malalamishi yake katika taifa jingine, imesema ripoti hiyo.

Baba wa Neymar, aliiambia runinga ya Band nchini Brazil Jumamosi kwamba ilikuwa wazi kuwa mwanawe alikuwa amewekewa mtego.

"Iwapo umma hautaambiwa ukweli kuhusu kisa hiki na iwapo hatuwezi kuonyesha ukweli kwa haraka, tuhuma hizo zitakuwa kubwa. Iwapo tutalazimika kuonyesha mawasiliano ya Neymar ya WhatsApp na msichana huyu," aliongezea.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 amepokonywa unahodha wa Brazil kutokana na madai ya utovu wa nidhamu hivi karibuni.

Shirikisho la a Soka nchini Ufaransa lilimpiga marufuku Neymar kwa mechi tatu baada ya kumshambulia shabiki mmoja kufuatia kufungwa kwa PSG na timu ya Rennes katika mchuano wa kuwania taji la Coupe De France mwezi uliopita.

Kombe la Copa America linaloshirikisha timu za America Kusini linafanyika nchini Brazil kuanzia Juni 14 hadi Julai 7, mwaka huu, huku wenyeji wakiwa wamepangwa Kundi A pamoja na Bolivia, Venezuela na Peru.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KLOPP: UEFA IMEMALIZA GUNDU, SASA MATAJI TU

●●● Mara zote tulikwenda likizo mara sita na bila kupata taji, iliniumiza, lakini ni tofauti kwa mwaka huu...

**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema hatimaye amehitimisha gundu la kutokuwa na bahati na ameshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya timu yake kuifunga Tottenham Hotspur mabao 2-0 juzi Jumamosi usiku.

Bao la kwanza la penalti la dakika za mwanzo kabisa kutoka kwa Mohamed Salah na lile la Divock Origi liliwapa ushindi huo Liverpool kwenye fainali iliyozikutanisha timu zote za Ligi Kuu ya England mjini Madrid, na Klopp hatimaye akibeba taji hilo la Ulaya.

Kabla ya mchezo wa Jumamosi mjini Madrid, Klopp alipoteza fainali sita mfululizo. Aliiongoza Liverpool kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa msimu uliopita ambapo alifungwa na Real Madrid, na alimaliza mshindi wa pili kwenye fainali hizo wakati akiiongoza Borussia Dortmund mwaka 2013.

Pia alishatinga fainali mbili za Kombe la Ujerumani na kupoteza na Kombe la Ligi ya Europa na lile la Ligi akiwa na Liverpool.

"Hatimaye najiona nimemaliza gundu, hasa kwa familia yangu," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo kwenye dimba la Wanda Metropolitano mjini Madrid.

"Mara zote tulikwenda likizo mara sita na bila kupata taji, iliniumiza. Lakini ni tofauti kwa mwaka huu, hii ni kwa ajili yao.

"Wachezaji wangu walikuwa na ari kubwa uwanjani, kwa sababu kulikuwa na hisia kali, na hisia kubwa. Najua jinsi Tottenham wanajihisi vipi kwa sasa, lakini la msingi nimebeba taji."

Aidha, Klopp alisema Liverpool, ambayo ilikuwa kwenye mbio moja na Manchester City kwenye mbio za Ligi Kuu ya England kwa kupitwa pointi moja, sasa wanajiona kama wameanza upya.

"Ni muhimu mno kwamba, sasa watu hawatatuuliza tena kuhusu kushinda mataji," alisema Klopp.

"Tunataka kushinda vingi pia, kwa asilimia 100 hili ni kundi la wachezaji ambao ni kama wameanza upya. Huu ni mwaka wao bora kabisa.

"Nimekuwa na medali nyingi za fedha na sasa nimepata medali ya dhahabu, lakini nina furaha kubwa zaidi kwa wachezaji wangu.

"Tulikuwa na kundi la wachezaji waliochanganyika na vipaji vya ukweli na wale wenye uzoefu mkubwa na sasa ni wakati wetu wa kufurahia kwa kile tulichokifanya."

Naye beki wa pembeni wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold alisema: "Mimi niko poa tu na najisikia furaha Liverpool kutimiza ndoto yake ambayo sasa imekuwa ya kweli.

"Ilituchukua muda, ni muhimu kwa maendeleo yetu, hii inatuonyesha kwamba tumefikia kwenye wakati gani na nini cha zaidi cha kufanya, hakika ni wakati bora zaidi kwetu kwa sasa."

"Ni ngumu kuzungumza kwa maneno mengi. Msimu tuliokuwa nao, tulistahili hili kuliko timu yoyote. Tulifanya kitu fulani maalumu, tulitawala mchezo."

"Hatutaangalia nyuma wapi tulipotoka, tunajiangalia kama mabingwa wapya wa Ulaya."

## KWA UFUPI

### SARRI AANDALIWA MKAKATI JUVE
Juventus inaandaa ada ya fidia kuilipa Chelsea ili kumng'oa kocha Maurizio Sarri hapo Stamford Bridge. ***(Independent)***

### HYSAJ AZIWEKA SAWA CHELSEA, UTD
BEKI wa pembeni wa Napoli, Mualbania Elseid Hysaj, 25, amethibitisha kwamba ataondoka klabuni hapo majira haya ya joto, baada ya kueleza anahitaji kushinda kitu fulani katika kazi yake hiyo. Anawindwa na Chelsea pamoja na Manchester United. ***(DigitAlb via Talksport)***

### COUTINHO ANUKIA CHELSEA
Chelsea itajaribu kumsajili kiungo mshambuliaji wa Barcelona, Mbrazil Philippe Coutinho, 26, kama itaweza kupindua kifungo chao cha usajili. ***(Gianluca di Marzio)***

### RODGERS KUMBAKISHA TOWNSEND
KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers, atajaribu kutatua changamoto ya kumbakisha winga wa Crystal Palace, Andros Townsend, 27. ***(Mirror)***

### LUKAKU APIGIWA HESABU PSG
Paris St-Germain inavutiwa kumsajili straika wa Manchester United, Mbelgiji Romelu Lukaku, 26. ***(Express)***

### FEKIR AZIVUTIA UNITED, LIVER
Manchester City na Liverpool zinajiandaa kuwania saini ya kiungo wa Lyon, Mfaransa Nabil Fekir, 25. ***(Express)***

### DAU LA BOATENG LATAJWA
Bayern Munich imetangaza dau la pauni milioni 20 kwa beki wao, Mjerumani Jerome Boateng, 30, ambaye anawindwa na Arsenal na Manchester United. ***(Bild - in German)***

### LIVERPOOL HAIUZWI - WERNER
MWENYEKITI wa Liverpool, Tom Werner amefunguka kuwa Fenway Sports Group haina lengo la kuiuza klabu hiyo iliyotwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa wa Ulaya. ***(Liverpool Echo)***

### MEUNIER KUVUTWA ARSENAL
Arsenal inavutiwa kumsajili beki wa kulia wa Paris St-Germain, Thomas Meunier, 27. ***(Paris United)***

### MESSI AFUNGUKA WHATSAPP YAO
MSHAMBULIAJI kinara wa Barcelona, Lionel Messi amesema wana kundi lao binafsi la WhatsApp linalomjumuisha yeye, Neymar na mchezaji mwenza wa kikosi hicho, Luis Suarez. ***(Marca)***

### KOLAROV AIKUNA INTER MILAN
Inter Milan inavutiwa na beki wa pembeni wa Roma, Mserbia Aleksandar Kolarov, 33. ***(Gazzetta dello Sport - in Italian)***

### FIORENTINA YAWEKWA SOKONI
Fiorentina, ambayo imeepuka kushuka daraja kutoka Serie A wiki ya mwisho ya msimu, imewekwa sokoni. ***(Corriere della Sera - in Italian)***

### BARCA KWA NEYMAR, GRIEZMANN
Barcelona inataka kumsajili mshambuliaji wa Atletico Madrid, Mfaransa Antoine Griezmann, 28, na kumrejesha kwa mara nyingine straika wa Paris St-Germain, Mbrazil Neymar, 27. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### NEWCASTLE YAMKANA GATTUSO
Newcastle United haijazungumza na kocha wa zamani wa AC Milan, Gennaro Gattuso kuwapo na uwezekano wa kurithi mikoba ya kocha wa sasa, Rafael Benitez. ***(Newcastle Chronicle)***



## HABARI MICHEZO

# KOMBO RAIS MPYA ZFF

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAKATI Seif Kombo akiibuka kidedea katika nafasi ya urais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), kufuatia kushinda kwa asilimia 57 katika uchaguzi mkuu wa shirikisho hilo uliofanyika jana, ametakiwa kushirikiana vema na viongozi wenzake walioshinda katika uchaguzi huo kuhakikisha soka la visiwani hapa linapiga hatua zaidi kwa kumulika vipaji maeneo ya vijijini.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya ZFF, Fadhir Ramadhani, jana alimtangaza mgombea Kombo kuwa rais wa shirikisho hilo baada ya kuibuka mshindi kwa kupata kura 16 sawa na asilimia 57 kati ya kura 28 za wajumbe wote zilizopigwa.

Kombo ameibuka kidedea baada ya kuwabwaga wagombea wenzake, Khamis Abdalla Said aliyepata kura saba sawa na asilimia 25 pamoja na Ame Abdalla Dunia aliyeambulia kura tano sawa na asilimia 17.85.

Kwa upande wa makamu wa shirikisho hilo, mwenyekiti huyo alimtangaza Salum Ubwa kuwa mshindi wa nafasi hiyo kufuatia kupata kura 25 sawa na asilimia 89.2, akimbwaga mpinzani wake, Khamis Shaali aliyeambulia kura tatu sawa na asilimia 10.7.

Aidha, Ramadhani aliwatangaza wajumbe wa Kamati ya Utendaji kwa ngazi ya mikoa ambapo kwa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Suleiman Haji aliibuka kidedea kwa kupata kura 18 sawa na asilimia 64.21, akimbwaga Faina Idarous aliyepata kura 10 sawa na asilimia 35.7

Mkoa wa Kusini Unguja, Salim Ali alitangazwa kuwa mjumbe wa Kamati ya Utendaji kwa kupata kura za ndio 27 kati ya kura 28. Wakati katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, Seif Bausi aliibuka kidedea kwa kupata kura 19 sawa na asilimia 67.85, akimpiku Rashid Tamimu aliyepata kura 9 sawa na asilimia 32.14

Aidha, kwa upande wa Mikoa ya Pemba Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi, amtangaza Omar Awadhi kuwa mshindi wa nafasi hiyo kwa mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kupata kura zote 28 sawa na asilimia 100.

Mkoa wa Kusini Pemba, Seif Mohmmed, alitangazwa mshindi wa nafasi hiyo kwa kupata kura zote 28 sawa na asilimia 100.

Awali akifungua mkutano huo mkuu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Vijana Utamaduni na Michezo, Omar King, aliwataka wagombea watakaochaguliwa wahakikishe wanasimamia vema soka la Zanzibar kwa kuibua vipaji katika mikoa na wilayani husuan maeneo ya vijijini badala ya kuangalia maeneo ya mjini pekee.

King alisema wakati umefika kupitia vyama vya mikoa kuhakikisha mpira wa Zanzibar unakua kuanzia katika mikoa yao hadi wilaya zote za Zanzibar kama ilivyokuwa katika miaka ya 80.

**MSAADA..**




Nahodha wa timu ya soka ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars', Mbwana Samatta (wa pili kushoto), akikabidhi msaada wa vitu vidogo vidogo kama sabuni na vinginevyo, kwa kinamama waliojifungua katika Hospitali ya Mwananyamala, Manispaa ya Kinondoni jijini Dar es Salaam jana, kabla ya mechi yao ya hisani iliyopigwa Uwanja wa Taifa kati ya timu Samatta na timu Kiba (Ally Kiba). Samatta anayechezea KRC Genk ya Ubeligiji amefanya zoezi hilo kwa kushirikiana na Doris Mollel Foundation. **PICHA: BIN ZUBEIRY**

# Chirwa sasa azikana Simba, Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kufanikiwa kuipa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika hapo mwakani, mshambuliaji wa Azam FC, Mzambia Obrey Chirwa amesema yeye bado ana mkataba na mabingwa hao wa Kombe la FA Tanzania.

Chirwa alifunga bao pekee katika mechi ya fainali ya Kombe la FA iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Ilulu mjini Lindi dhidi ya Lipuli FC kutoka Iringa.

Mzambia huyo amekuwa akihusishwa na tetesi za kutakiwa katika klabu yake ya zamani ya Yanga pamoja na mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba zote za jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Chirwa alisema kuwa mkataba wake na Azam FC haujamalizika na anaheshimu makubaliano ambayo aliingia na klabu hiyo.

Chirwa alisema amefurahia kufanya kazi na klabu hiyo, huku akiongeza kwamba alipata fursa nyingine ya kujifunza kuishi na familia mpya hapa Tanzania.

"Nasikia wanasema mimi naondoka, si kweli, mkataba wangu bado upo," alisema mshambuliaji huyo.

Aliongeza kwa kuwataka mashabiki wa Azam FC kuendelea kuwaamini na kuwapa ushirikiano zaidi katika msimu ujao ambao watashiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Ninafuraha sana, nashukuru tumekuwa mabingwa, nawaomba mashabiki wa Azam ambao wamekuja kutushangilia waendelee kutuamini, watupe sapoti na sisi tunaahidi kujituma katika kila mashindano tutakayoshiriki," alisema mshambuliaji huyo.

Katika Ligi Kuu Tanzania Bara, Azam FC imemaliza msimu wa 2018/19 ikiwa chini ya makocha, Abdallah Mingange na Iddi Cheche ikiwa katika nafasi ya tatu, nyuma ya mabingwa Simba na Yanga.

# Balora aziweka kiporo Biashara United, Namungo

**Na Mwandishi Wetu**

KIPA chaguo la kwanza wa Biashara United ya Musoma mkoani Mara, Nourdine Balora, amesema bado hajaamua klabu ipi ataitumikia katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Balora alisema amepokea ofa kutoka klabu mbalimbali hapa nchini ambazo zimevutiwa na kiwango chake, lakini bado hajafanya uamuzi wowote.

Balora ambaye ametajwa kutakiwa zaidi na Namungo FC itakayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao wa 2019/20, amesema atazingatia maslahi kabla ya kufikia uamuzi wa kusaini mkataba mpya.

**"Nina ofa mbalimbali, ikiwamo kutoka kwa timu yangu ya Biashara United, lakini narudi kwanza nyumbani, nitafikiria na kuamua nijiunge na klabu gani, ila nitazingatia maslahi kabla ya kusaini mkataba mpya," alisema kipa huyo.**

Alisema anataka kuona anaitumikia klabu ambayo ina uhakika wa kuwapa mishahara kwa wakati wachezaji wake kwa sababu anaamini hilo linachangia nyota kujituma na kupambana katika mashindano yote watakayoshiriki msimu ujao.

"Kikubwa naomba niseme nimefurahi kuona timu yangu imebaki Ligi Kuu, ni faraja sana, kwa sasa narudi nyumbani na nitaendelea kupokea ofa, itakayokuwa nzuri ndio nitasaini, inaweza kuwa Biashara United au timu nyingine," alisema golikipa huyo.

Aliongeza kuwa msimu wa ligi uliomalizika ulikuwa mgumu kwao, lakini kutokata tamaa ndiko kuliwasaidia waweze kubakia katika ligi hiyo ambayo tayari African Lyon na Stand United ya Shinyanga zimeshuka moja kwa moja.

Biashara United inayofundishwa na Amri Said ilimaliza msimu ikiwa na pointi 47 na kujinasua na janga la kushuka daraja.

# Michezo

Jumatatu Juni 3, 2019

Nipashe




## Klopp: Uefa imemaliza gundu, sasa mataji

HABARI UK 30

MWAKA WETU...




Nahodha wa Liverpool, Jordan Henderson, akisherehekea na wachezaji wenzake kwa kunyanyua juu Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kulitwaa juzi kwa kuifunga Tottenham mabao 2-0 kwenye mechi ya fainali iliyopigwa Uwanja wa Wanda Metropolitano jijini Madrid juzi. **PICHA: HABARI UK. 30**

# KAGERE ATOA MALENGO MAPYA SIMBA 2019/20

## ●●●Asema chanzo ni mashabiki, awaamsha wachezaji wenzake, Cecafa yawakatalia kujitoa...

**Na Somoe Ng'itu**

MFUNGAJI Bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu uliomalizika, Mnyarwanda Meddie Kagere, amesema anaamini msimu ujao ataifanyia "mambo makubwa" timu yake ya Simba kutokana na sasa kuifahamu vizuri ligi hiyo ya juu hapa nchini.

Kagere ambaye alitua Simba mwaka jana akitokea kwa mabingwa wa Ligi Kuu Kenya, Gor Mahia ameifungia timu yake mabao 23 na kutangazwa pia kuwa Mchezaji Bora wa mwaka wa klabu hiyo ya jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kagere, alisema amepata mapokezi mazuri kuanzia mwanzo wa msimu hadi mwisho, na ili kuwalipa mashabiki wa Simba, anajipanga kujituma zaidi katika msimu ujao.

Kagere alisema anamshukuru Mungu kwa kuisaidia timu yake kutwaa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara wakati huu ikilibeba kwa mara ya pili mfululizo na kufika hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku wakizifunga timu ngumu kwenye Uwanja wa Taifa.

Alisema haikuwa safari rahisi kufikia mafanikio hayo, lakini ushirikiano waliokuwa nao kuanzia wachezaji, viongozi na wanachama, ndio umefanikisha kuona wanakuwa na msimu bora zaidi.

"Nadhani tunatakiwa kujipanga vizuri ili msimu ujao tuweze kufanya vema, tunahitaji kufanya vizuri zaidi ya tulivyofanya msimu uliomalizika, bidii na juhudi zetu ndio zitasaidia kutimiza malengo, kila mmoja anatakiwa ahakikishe tunasonga mbele," alisema mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Rwanda maarufu Amavubi.

**CECAFA YAWATAMBUA**

Katibu Mkuu wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), Nicholas Musonye, amesema hana taarifa za mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara kujitoa katika mashindano ya Kombe la Kagame ambayo yanatarajiwa kuchezwa kuanzia Julai 7 hadi 21, mwaka huu jijini Kigali, Rwanda.

Musonye aliliambia Nipashe kuwa hana taarifa rasmi za uamuzi wa Simba kujitoa katika mashindano hayo ambayo bingwa wake huzawadiwa kitita cha Dola za Marekani 30,000 kutoka kwa mlezi wa Cecafa, Rais wa Rwanda, Paul Kagame.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, alisema kuwa sababu kuu ya kujitoa katika michuano hiyo ni ratiba yao kuwabana.

Magori alisema kuwa baada ya wachezaji wao walioko Timu za Taifa mbalimbali ikiwamo Taifa Stars kurejea nchini wakitokea Misri kwenye fainali za Kombe la Afrika wataanza maandalizi ya kwenda Marekani ili kujiandaa na msimu mpya.

Bingwa mtetezi wa mashindano ya Kombe la Kagame ni Azam FC ambaye juzi alifanikiwa kutwaa Kombe la FA Tanzania ambalo linampa tiketi ya kwenda kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika hapo mwakani.

## Samatta: Viatu vya Lukaku vinanitosha

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI akiwa anaongoza kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), kuanza mazoezi rasmi kujiandaa na fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019), mshambuliaji wa KRC Genk, Mbwana Samatta, amesema nafasi ya yeye kuendelea kuitumikia klabu hiyo kwa msimu ujao ni ndogo na kwamba sasa anaweza kuvaa viatu hata vya Romelu Lukaku wa Manchester United.

Samatta aliliambia gazeti hili kuwa ameshaanza mazungumzo ya kwenda kujiunga na klabu nyingine za Ulaya, hasa England na anaamini ana nafasi ya kupata timu mpya.

Mshambuliaji huyo alisema endapo mchakato huo utashindwa kufanikiwa, atarejea KRC Genk kwa sababu bado ana mkataba na klabu hiyo.

"Sioni nafasi ya kurejea tena Genk, tayari mchakato wa kuhamia katika klabu nyingine umeshaanza na ninaamini mambo yatakwenda vizuri, nina uzoefu wa kucheza soka Ulaya, ninajua nini ninatakiwa kufanya," alisema mshambuliaji huyo wa zamani wa African Lyon, Simba na TP Mazembe ya DR Congo. Aliongeza kuwa yupo tayari kucheza katika klabu yoyote ikiwamo Manchester United ambayo amekuwa akiishabikia kwa sababu ameshapata uzoefu wa kusakata kandanda Ulaya.

"Mpira ni ule ule, hata kuvaa viatu vya Lukaku (Romelu) pia ninaweza, kwa nini nishindwe, sana sana kule presha itaongezeka kwa sababu ni klabu kubwa, najua ninachotakiwa kukifanya nikiwa huko ili kuitumikia vema timu yangu," alisema Samatta.

Kuhusu kambi yao ya Stars, nahodha huyo alisema kila mchezaji ambaye ameitwa katika kikosi hicho anatarajiwa kuonyesha kiwango chake cha juu katika mashindano ya Afcon ambayo Watanzania wameyasubiri kwa muda mrefu.

"Tutakapokuwa kule wote tunakwenda na jambo moja tu la kupambana, tutakutana na Mane (Sadio) anatoka Liverpool na mimi natoka Lipuli, mwisho wa siku soka huwa na matokeo ya kushangaza, tunatarajia kwenda kufanya vema," Samatta aliongeza.

Stars inatarajia kuondoka nchini Ijumaa kuelekea Misri na ikiwa huko ili kujiimarisha itacheza mechi ya kirafiki ya kimataifa na wenyeji Juni 13, mjini Alexandria.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >